**26 JUNI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Hamsini na Tano – Tarehe 26 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023 *(The Finance Bill, 2023)*.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023 *(The Finance Bill, 2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**26 JUNI, 2023**

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, sasa aulize swali lake.

Na. 719

**Kupandisha hadhi barabara ya Kwinji - Kilindi Asilia hadi Kimbe**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapandisha hadhi barabara ya Kwinji - Kilindi Asilia hadi Kimbe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kwinji - Kilindi Asilia hadi Kimbe ina urefu wa kilometa 43.7, barabara hii inaanzia Kata ya Msanja, inapita Makao Makuu ya Kata ya Kilindi Asilia na kuunganisha Kata ya Kimbe.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007, Kifungu cha 11 na Kanuni za Usimamizi wa Barabara ya mwaka 2009 kifungu 43(1) na (2) na kifungu 44(1), kupitia Tangazo la Serikali Na. 21 ya tarehe 23 Januari, 2009 imeainisha vigezo vya utaratibu wa kuhamisha barabara ili iwe chini ya *TANROADS* ambapo barabara inaweza kupandishwa au kuteremshwa kutoka daraja moja kwenda daraja jingine. Mkoa unashauriwa kuwasilisha mapendekezo ya kupandisha hadhi

barabara hiyo kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa ili utaratibu ufuatwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri tu. Nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa sababu barabara hii inaunganisha Kata tatu. Kata ya Msanja, Kata ya Kilindi Asilia na Kata ya Kimbe, ni Kata ambazo zina uzalishaji mkubwa sana wa mahindi na kipindi cha mvua inakuwa ni shughuli kubwa magari kupita. Sasa kwa sababu suala hili liko Serikalini; Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuelekeza Mkoa sasa kufanya tathmini hiyo na iweze kupandishwa hadhi barabara hiyo?

Swali la pili ni kwamba barabara hii ina madaraja mengi na ina vivuko vingi sana na kipindi cha mvua haipitiki. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kutoa maelekezo kwa *TARURA* ili maeneo haya yaweze kurekebishwa na Wananchi wa Wilaya ya Kilindi waweze kupata huduma ya Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kigua, swali la kwanza kuhusu kuelekeza mkoa; kama nilivyokuwa nimesema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba, taratibu za kupandisha au kuteremsha barabara kuwa ya Mkoa ni taratibu za kisheria. Hivyo basi, ningeshauri Mkoa wa Tanga waanze kuchukua hatua stahiki za kupandisha barabara hii kwa kukaa Mheshimiwa Kigua kule Kilindi kupitisha kwenye *DCC* yao na ikitoka *DCC* iweze kwend *RCC* na baadaye kwenda kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa, kisha waweze kuandika kwa Waziri mwenye dhamana ya barabara ambaye ni Waziri wa Ujenzi ili na yeye aweze kutuma timu ya kufanya tathmini ili barabara hii iweze kupandishwa kuwa ya Mkoa. Nitakaa na Mheshimiwa

Kigua tuone tunafanya vipi na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi ili barabara hii iweze kuanza huu mchakato wa kupandishwa.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la madaraja na vivuko ambavyo vinahitajika sana. Ni kweli nikiri kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa uzalishaji na wananchi wa kule Kilindi kwa ajili ya kutoa bidhaa zao mashambani Mheshimiwa Mbunge amekuwa akilifuatilia sana, tutakaa naye vilevile kuona ni namna gani tutapata fedha kwenye bajeti ya *TARURA* hii inayokuja 2023/2024 ili kuweza kutengeneza vivuko zaidi kwa sababu tayari katika mwaka huu pekee wa fedha tunaoumaliza tulitengeneza boksi Kalavati 15, *drift* ndefu yenye mita 15 lakini imechongwa vilevile kilometa 21 kwenye barabara hii, lakini kwa sababu ina urefu wa kilometa 47 tutakaa tuone ni namna gani tunaendelea kutengeneza maeneo hayo yaliyosalia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 720

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Mtwango – Mufindi**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mtwango?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Sadan. Aidha,

Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya na itapeleka fedha kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mtwango pindi fedha zitakapopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarakani Jimbo la Mufindi Kusini haikujengewa kituo cha afya hata kimoja, wakati maeneo mengine yamepata fursa hiyo. Wananchi wa Mufindi Kusini wana uhitaji mkubwa.

Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya cha Mtwango?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga kituo cha afya Mtwango. Kwa hatua za mwanzo naomba nimuelekeze Mganga Mkuu wa Mkoa wa Iringa kutuma timu kwenye eneo la Mtwango na kufanya tathmini na kuona mahitaji ambayo yako katika Kata ile, baada ya kufanya tathmini hiyo aiwasilishe Ofisi ya Rais – TAMISEMI Ili tuweze kuona ni namna gani tunapeleka fedha.

Mheshimiwa Spika, nimtoe mashaka Mheshimiwa Kihenzile Serikali hii ya Awamu ya Sita imeweka kipaumbele cha kujenga vituo vya afya kwenye maeneo yote ya kimkakati nchini ikiwemo kule Kata ya Mtwango Jimboni kwake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya cha Nyambiti ambapo imekuwa ikiahidi kila mara tunapouliza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itapeleka fedha katika kituo hiki cha afya alichokitaja Mheshimiwa Kasalali Mageni kule Jimboni Sumve kadri ya uapatikanaji wa fedha, lakini tutatuma timu iweze kuangalia pia ukubwa wa eneo lililopo pia na majengo ambayo yanahitaji kufanyiwa upanuzi halafu tuweze kupata taarifa kamili na kutafuta fedha hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Mapinga katika Jimbo la Bagamoyo katika sensa ya mwaka huu ina watu 42,000 na haina kituo cha afya.

Je, Serikali ina mpango gani kujenga kituo cha afya katika kata hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutatuma timu katika Kata ya Mapinga kule Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kuweza kufanya tathmini na kuona kama vigezo vimefikiwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya, halafu tutatafuta fedha kwa ajili ya kujenga kituo hicho cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Kata ya Didia ni Kata ya kimkakati na ina idadi kubwa sana ya watu ukizingatia kwamba ni maarufu kwa zao la mpunga.

Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali hii ya Awamu ya Sita kuhakikisha inajenga vituo vya afya kwenye maeneo yote ya kimkakati nchini, ikiwemo Kata hii aliyoitaja Dkt. Christina Mnzava, tutafanya tathmini na kuona mahitaji yanayohitajika pale na kisha kuiweka kwenye mipango yetu ya kutafuta fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 721

**Kugawa Vijiji vya Wilaya ya Korogwe**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itavigawa Vijiji vya Makangara, Mkomazi, Mkalamo, Mwenga, Kwemasimba, Mkwajuni, Sekioga na Bungu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa maeneo ya utawala hutekelezwa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura Na. 287 na Na. 288 pamoja na mwongozo wa uanzishaji wa maeneo ya utawala wa mwaka 2014 ambao umeanisha utaratibu na vigezo vinavyopaswa kufuatwa. Miongoni mwa vigezo hivyo ni uwezo wa Halmashauri kujitegemea katika bajeti ya uendeshaji kutokana na mapato ya ndani, uwezo wa kutoa huduma za kijamii na kiutawala, upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na uwepo wa huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa kipaumbele kuboresha na kukamilisha miundombinu msingi kwenye maeneo yaliyoanzishwa

ili yaweze kutoa huduma kwa jamii na baadae kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali ambayo ni ya jumla sana, naomba kuuliza swali dogo moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yanataka kumegwa kutoka kwenye vijiji ambavyo nimevitaja ni maeneo makubwa na tayari pande zote za vijiji zina miundombinu muhimu kama vile shule na zahanati na kuna ahadi ya viongozi wakiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni lini, Serikali itavigawa vijiji hivi ili kurahisisha shughuli za maendeleo na kuwasogezea wananchi huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo ametoka kusema Mheshimiwa Mnzava hapa, kwamba kama maeneo haya tayari yana miundombinu muhimu kwa ajili ya kukidhi vigezo vile vinavyotakiwa kuwepo kwa ajili ya kugawa vijiji vipya, basi tutatuma timu katika maeneo hayo ili kuweza kufanya tathmini hiyo na kisha baada ya thathmini hiyo tutakaa na wataalam pale kwetu Ofisi ya Rais - TAMISEMI na kisha kuona ni namna gani tunaweza kuwapatia vijiji hivyo kwa sababu tayari maeneo hayo yameshakidhi vigezo vile vinavyotajwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Ni lini Serikali itaigawa Kata ya Mwangeza ambayo ina idadi ya watu 32,000 na hivyo huduma ni ngumu sana kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtinga ni kwamba, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuboresha maeneo yale ambayo tayari yameshagawanywa, kwa sababu tutapogawanya Kata mpya maana yake itabidi kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sekondari nyingine, ambapo nyinyi ni mashahidi Waheshimiwa Wabunge humu ndani, kwa sasa Serikali inapeleka fedha katika kila Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari na hivyo tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati kote nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi tukimaliza kupeleka vitu vya msingi katika Kata zilizopo ambazo ni mpya zilianzishwa mwaka 2010 na nyingine zilianzishwa mwaka 2015 Serikali ikikamilisha katika kuweka mazingira bora katika maeneo hayo tutaangalia vilevile katika Kata ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 722

**Utaratibu wa kutangaza ajira nchini**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza: -

Je, utaratibu gani unatumika kutangaza ajira nchini ili kuhakikisha Watanzania wote wanapata haki ya kupata taarifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,

naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, swali namba 722, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti ya Ajira Toleo Na. 2 la mwaka 2008, Sura ya Nne, Aya ya 4(2) ikisomwa pamoja na ya Kanuni 12(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, nafasi za ajira katika Utumishi wa Umma ni za ushindani na zinazingatia sifa, taaluma, uwazi na usawa.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, matangazo ya ajira kwa ajili ya kujaza nafasi wazi ndani ya Utumishi wa Umma hutolewa kupitia tovuti za taasisi husika, mitandao ya jamii, magazeti na mbao za matangazo katika ofisi husika. Maombi ya nafasi hizi hudumu kwa muda wa siku kumi na nne 14 kwa kada za masharti ya kawaida na siku 21 kwa waombaji wa nafasi za Watendaji Wakuu na nafasi za Uongozi za Taasisi za Kimkakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Ni kwa nini sasa Serikali inapoita vijana kwa ajili ya usaili isiangalie hizo sifa na vigezo kuliko hivi sasa pengine nafasi ni ishirini wanaitwa watoto 3,000 mpaka 5,000? Wanasababisha vijana wengi kuteseka hapa Dodoma wakati wa kusubiri huo usaili. *(Makofi)*

Swali langu la pili, ni kwa nini vijana wengi wamekuwa wakijitolea au kupewa nafasi za mikataba lakini inapotokea ajira hawa vijana hawapati kipaumbele, wamekuwa wakijitolea miaka minne, mitano kiasi kwamba zikitoka ajira wanaajiriwa wapya. Hii kwa kweli inaumiza sana na inaliza sana kwa vijana wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali maswali mawili ya Mheshimiwa Ritta Kabati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na nafasi chache wanaitwa wengi, katika maelezo ya msingi nilieleza kwamba nafasi za ajira kwa sasa kwa mujibu wa kanuni ambazo zimepitishwa na Bunge lako ni nafasi za kiushindani. Hivyo tunapotangaza matangazo matarajio yetu ni kwamba watajitokeza wengi ili waje kushindana kwa ajili ya kupata nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nakiri mbele ya Bunge lako kwamba malalamiko juu ya wingi wa wanaoomba na dhidi ya nafasi kuwa chache umeendelea kujitokeza. Serikali yako imeendelea kufanya juhudi za dhati kuhakikisha kwamba tunakabiliana na changamoto hii. Lakini kupitia Bunge lako maelekezo yalishatolewa na Ofisi ya Rais inayoshughulikia Utumishi imeyachukua na inakwenda kuyafanyia kazi na tutapokuwa tayari tutaleta majibu mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusu wale wanaojitolea halafu baadaye wanakuja kukosa ajira. Wakati naeleza katika swali la msingi, ajira za Serikali zinazingatia sifa, taaluma, uwazi na usawa, na ni maelekezo ya Bunge lako kwamba katika uwazi huo na usawa huo, ulielekeza kwamba ajira zinapotolewa waitwe watu wadahiliwe kwa usawa na uwazi, sasa inapotokea kwamba mtu aliyepo kazini anakosa kazi hili tena linakuwa niseme ni jambo la kiufundi zaidi na siyo jambo la mtu kuonewa. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wanaofanya kazi waendelee kuhakikisha kwamba wanashindana vizuri ili waendelee kupata kazi kama ambavyo wengine wamekuja kwenye ushindani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Waziri ametamka wazi kwamba nafasi hizi zinatolewa kwa ushindani, lakini kule vijijini ambako wanafunzi wengi ambao wanaomba hizi nafasi ndiko waliko, Magazeti hayafiki wala mtandao hakuna.

Je, huo ushindani wa haki unapatikanaje katika mazingira ya aina hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Shangazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, vilio vinekuwepo hasa katika maeneo ya kule vijijini kabisa, na ni maelekezo yetu kama Wizara kuhakikisha kwamba matangazo yote yanayoletwa ya ajira yanakwenda kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri na kuhakikisha yanafika kwenye vijiji husika, yafike kwenye ofisi za vijiji, yafike kwenye ofisi za kata na maeneo yote yaliyo muhimu kwa ajili ya wananchi kupata taarifa, ili ajira hizi ziendelee kukimbiliwa na Watanzania wote kwa usawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo la kuita watu wengi kwenye nafasi chache chache za usaili limekuwa ni jambo sugu na Serikali hamuwezi kulifanyia kazi; je, hamuoni sasa umefika wakati kuwapa posho angalau wale mnaowaita, ili waweze kujikimu wanapokuwa Dodoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo analosema la kutoa posho kwa wanaoomba, hili ni jambo la kibajeti, lakini pia ni jambo la kisera. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumejenga uwezo, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Wabunge wote basi nalo pia litaangaliwa, lakini kwa sasa niseme jambo hilo ni gumu kidogo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly Ntate, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunajua wanaotakiwa kuajiri Serikali Kuu ni Menejimenti hya Utumishi kupitia Sekretarieti ya Ajira; je, ni lini Serikali sasa itachukua hilo jukumu badala ya kuachia idara zinazojitegemea? Kuachia Wizara nyingine kuajiri watumishi wa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janejelly Ntate kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali iliamua kugatua baadhi ya mamlaka yake na kupeleka kwenye Taasisi na Wizara mbalimbali ili kupunguza lile lundo la watu wote kuja katika sehemu moja, lakini pia tukizingatia *professional* katika uajiri, lakini mawazo anayotoa Mheshimiwa Mbunge ni mawazo ambayo hata sisi ndani ya Wizara tunayaangalia, lakini nataka nikuhakikishie kwamba mambo yote haya yanakwenda kisera, kimkakati, na baada ya kujiridhisha kwamba tutakapoyachukua kuyarudisha Wizarani au kuendelea kufanya katika njia nyingine yatakuwa na tija kwa ajili ya kusaidia Watanzania inapofika kwenye jambo zima la ajira.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mawazo yako ni mazuri, na sisi kama Wizara tuyachukue na kuendelea kuyafanyia kazi na tutakuja kujulishana vizuri baadae. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mfumo wa ajira ulioko sasa una manung'uniko mengi; Serikali haioni iko haja sasa ya kupitia

mfumo wenyewe kwa ujumla ili uwe rafiki kwa vijana wetu walioko? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amandus kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati tunawasilisha bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, hoja anayoeleza Mheshimiwa Mbunge ilitolewa pia katika kikao kile na yalikuwa ni makubaliano ya Bunge lako kwamba tutayachukua mawazo mazuri yale na kwenda kuyafanyia kazi, na haya yote yatakapokuwa yamekamilika basi yatakuja kuonekana katika sera na sheria ambazo baadae nafikiri zinaweza zikabadilika kutokana na mawazo mazuri ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maagizo ya Bunge yanaendelea kufanyiwa kazi, na tutakapokuwa tayari tutakuja kuleta taarifa katika utaratibu wa vile vikao vyetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba sasa aulize swali lake.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Momba, naomba swali letu lipate majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Swali namba 723. Nakupa jina la swali, namba ya swali lako ili ulitaje, ni namba 723.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Momba, naomba Swali Namba 723 lipate Majibu ya Serikali.

Na. 723

**Vijiji visivyokuwa na umeme – Momba**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha zoezi la kuwasha umeme kwenye vijiji vilivyosalia katika Jimbo la Momba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili ambapo vijiji vyote visivyo na umeme vitafikiwa na huduma ya umeme. Mradi huu unahudumia vijiji 42 vilivyosalia katika Jimbo la Momba ambapo kati ya hivyo vijiji 22 vimekwishawashiwa umeme na vijiji 20 kazi mbalimbali zinaendelea. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Disemba, 2023. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nimesikia majibu ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika vijiji ambavyo vimesalia nguzo zimepelekwa maeneo hayo na zimeachwa kwa muda mrefu na wananchi wamechukulia kwamba nguzo hizi zimetelekezwa; je, ni lini shughuli itaendelea kwa ukamilifu kuona nguzo zinasimikwa na vijiji hivi vinawashwa umeme?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika vijiji ambavyo vimepatiwa umeme, umeme umekuwa sio toshelevu hivyo

wawekezaji kuvunjika moyo kushindwa kufanya shughuli zao zinazohitaji umeme mkubwa; je, ni lini Serikali itatuwekea *capacitor* au *booster* kwenye vijiji hivyo ikiwa ni sambamba na kujenga kituo cha umeme mkubwa kwenye Kata ya Nkangamo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Condester kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, kwenye hivi vijiji 20 ambavyo vimebaki kazi katika hatua mbalimbali zinaendelea. Mkandarasi anayefanya kazi katika Mkoa wa Songwe kwa ujumla anaitwa *DEM,* ni mkandarasi ambaye anaendelea kutekeleza kazi yake na katika mkoa yuko zaidi ya asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Condester kwamba kabla ya Disemba mwaka huu maeneo yote yatakuwa yamepatiwa umeme kwa sababu hatua ni moja moja kwenye maeneo tofauti tofauti, lakini nimhakikishe kwamba vifaa hivi ambavyo vimewekwa katika maeneo hayo ni vile ambavyo vitakuja kutumika katika maeneo hayo, havijatelekezwa na vitatumika kufanya kazi ambazo zinastahili kufanyika.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili, ni kweli kwamba kumekuwa kuna upungufu wa umeme katika maeneo mbalimbali na ni kwa sababu ya mahitaji kuwa makubwa na sisi kama Wizara ya Nishati tunaendelea kufanya *assessment,* na katika awamu hiiya kwanza ya Mradi wetu wa Gridi Imara tumetenga vituo vya kupoza umeme 15 katika maeneo mbalimbali kulingana na mahitaji makubwa yalivyo. Namhakikishia Mheshimiwa Condester pia kwamba nia ya Serikali ni kuhakikisha ifikapo angalau mwaka 2030 kila Wilaya iwe imepata kituo cha kupoza umeme kulingana na uwezekano wa upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini, ili kuhakikisha kwamba tunafikisha umeme wa kutosheleza katika maeneo yote, lakini nimuombe baada ya hapa tutawasiliana ili tuone hilo eeo ambalo ni mahususi analolisema lina upungufu

sana wa umeme saa hizi tulichukulie hatua mahususi na za haraka zaidi, ili kuwavutia wawekezaji zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, aah, Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kijiji cha Mgwashi, Kata ya Lukozi wamekata tamaa kabisa na upatikanaji wa umeme baada ya kuwa wameahidiwa mara nyingi kwamba umeme unakwenda kuwashwa kwenye Kijiji chao. Naomba *commitment* ya Serikali, ni lini hasa Serikali itaenda kuwasha umeme katika Kijiji cha Mgwashi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi nak ama ambavyo tumeeleza mara zote hapa, kabla ya Disemba mwaka 2023 vijiji vyote ambavyo havina umeme vitakuwa vimewashiwa umeme na Kijiji cha Mgwashi pia kitakuwa ni kimojawapo kitakachowashiwa umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kwamba kufika tarehe 30 Juni, wananchi wa Ikomba watakuwa wamefikishiwa umeme wa *REA,* leo ninavyoongea hata nguzo zilizokuwepo kule wameziondoa; je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki wananchi wa Ikombe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nimuahidi Mheshimiwa Jumbe kwamba, Mradi wa *REA III, Round II* unatakiwa kukamilika ifikapo Disemba, 2023. Yale maeneo ambayo bado hayajakamilika na nguzo pengine zimeenda zimepelekwa sehemu nyingine zitarudishwa zitapelekwa hapa,

lakini nia ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwezi Disemba, 2023 kila kijiji kimepata umeme na wananchi waweze kupata huduma hiyo, kwa hiyo, ahadi hiyo tutaitekeleza kwa kadri ilivyotolewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 724

**Tembo kuvamia wananchi – Lindi**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa uvamizi wa tembo kwa wananchi na mashamba katika Wilaya za Liwale na Nachingwea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kuwepo na changamoto ya wanyama wakali na waharibifu wakiwemo tembo. Kwa sasa Serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu wa mwaka 2020 – 2024. Wizara inaendelea kufanya yafuatayo; kutoa elimu juu ya kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu; kujenga vituo vya askari wanyamapori ili kusogeza huduma karibu na wananchi; kuwafunga mikanda tembo na kuanzisha timu maalum *(rapid response teams)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuwashirikisha wananchi kwa kutoa mafunzo kwa Askari wa Vijiji *(VGS)* ili kuongeza nguvu ya kudhibiti tembo katika maeneo ya wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna…

Waheshimiwa Wabunge, sasa sijui tutasikilizanaje kila mtu akigonga meza.

Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita nilitoa ushauri kwa Serikali kwa kuweka *solar electric fence* kuzunguka maeneo yote ambayo yana mbuga za wanyama. Je, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi wa kuchukua ushauri huo ili kuepuka wanyama kutoka kwenye mbuga za wanyama na kuzunguka hovyo, kuzurua na kuleta maafa na kuharibu mashamba ya watu kwa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, fidia zinazolipwa kwa wahanga ni kidogo sana, haziendani na hali halisi ya sasa; je, Serikali haioni haja ya kuongeza kiwango cha fidia zinazotokana na uharibifu wa wanyamapori?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge, maswali haya yameendelea kujitokeza katika Bunge lako hili, lakini swali la kwanza linalohusiana na kuweka *electric fence*, tayari Wizara imeshaanza mkakati huo na kuna maeneo ambayo tumeyatengea bajeti tutaanza kuweka *fence* kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye hili la pili la fidia, tayari mlishatupa maekekezo kupitia sheria hii na tuko kwenye hatua za

mwisho. Kwa hiyo, tutaileta na tutafanya marekebisho ili kiwango hiki kiweze kuongezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, Wabunge wote wenye matatizo ya tembo naona mmesimama hapa na kila mmoja ana swali lake. Maana swali la msingi linahusu uvamizi wa tembo kwa wananchi na mashamba, sio nje ya hapo. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri waliosimama ni wengi kuliko idadi ya maswali ambayo naweza kumpa acha kila mmoja ataje jambo lake, halafu utasema Serikali inasemaje kuhusu shida hiyo.

Mheshimiwa Mbunge wa Mikumi, Mheshimiwa Dennis Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, changamoto ya tembo kwenye vijiji ambavyo vinazunguka hifadhi ya Mikumi ni kubwa na Serikali imetoa ahadi nyingi; nini kauli ya Serikali kwa madhara makubwa ambayo wananchi wanayapata kutokana na uvamizi wa tembo katika vijiji vya Kilangali, Zombo, Ulaya na Iyombo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, wananchi wa Kata ya Ndungu, Kata ya Kalemawe na Kata ya Maore wanaishi kwa shida sana kwa sababu karibu kila wiki mwananchi anauwawa na mazao yanaharibiwa kwenye mashamba. Serikali niliiomba juzi wakati wa bajeti, Bunge likiisha niongozane na Waziri aende akaone hali yaenyewe, Mheshimiwa Waziri ananiambia nini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, alipokuja Mheshimiwa Waziri kutatua na kuzungumza na wananchi kuhusu masuala ya tembo aliahidi pia kwamba *TFS* na *TANAPA* watajenga madarasa katika Shule ya Sekondari ya Mkomanule na Shule ya Sekondari ya Mbunga. Je, ahadi hiyo ipoje mpaka sasa hivi, wananchi bado wanaisubiri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, hiyo ahadi ni kutokana na madhara ya tembo ndio badala ya yale madhara ya kuwalipa wananchi waliopata athari na mashamba, Serikali itajenga madarasa au ni vitu viwili tofauti? Ili nijue kama na lenyewe liwemo kwenye orodha ua hapana? Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, alipokuja lilikuwa ni suala la kutatua hilo suala la tembo, kwa sababu watu walikuwa wamekufa katika vijiji hivyo tofauti, na katika moja ya shida waliyoieleza wananchi wale, pamoja na tembo, waliomba pia wajengewe madarasa katika shule zao hizo na *TFS* na *TANAPA*.

**SPIKA:** Haya, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye hili la Mheshimiwa Vita Kawawa mimi nitakupa uhuru. Kama Serikali huwa inatoa hicho kitu alichokisema kama sehemu ya fidia utalijibu swali, kama sio sehemu ya fidia Mheshimiwa Vita Kawawa ataleta kama swali la msingi.

Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, wananchi wa Mkinga kwenye kata 13 wamepata athari kubwa ya tembo kutoka Mbuga ya Tsavo, Kenya na Mbuga ya Mkomazi na ili kukabiliana na tatizo hilo Serikali iliahidi kuweka kituo maalum Wilaya ya Mkinga. Lini Serikali itatimiza ahadi hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kata ya Ruaha Mbuyuni ambayo iko tu barabarani kabisa pale kwenye lami, Kijiji cha Msosa, Kijiji cha Ruaha Mbuyuni chenyewe na Kijiji cha Ikula kuna madhara makubwa sana yanayosababishwa na tembo kiasi cha kusababisha chakula kuwa pungufu. Serikali inachukua hatua gani katika kudhibiti tembo hao hasa kuongeza askari katika Kambi ya Mtandika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa; pamoja na tembo kuvamia maeneo mbalimbali hivi karibuni katika Kata ya Lyamigungwe na Kata ya Lupota simba wamevamia katika mifugo ya wananchi na wamekula mifugo ile na wananchi wana taharuki kubwa. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa huru? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tatizo la tembo, mamba na viboko ni kubwa sana katika Jimbo la Mwibara na imefikia kwamba wameuwa mpaka wananchi.

Sasa je, Serikali ina mpango gani au inachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba, hilo tatizo linakwisha?

**SPIKA:** Hao viboko wanavamia mashamba pia? Wanavamia mashamba na wananchi?

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, *yes,* yaani kwa sababu wanatoka majini kwenda kula vyakula huko nchi kavu.

**SPIKA:** Haya, sawa. Haya Mheshimiwa Zidadu Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Wilaya ya Tunduru imezungukwa na hifadhi ya wanyamapori na wananchi wa Tunduru wanategemea kilimo. Kutokana na uvamizi wa tembo uharibifu ni mkubwa pamoja na watu kupoteza Maisha, na Serikali inatumia kiwango kikubwa sana kulipa fidia kwa wananchi.

Je, Serikali sasa haioni haja ya kuwaajiri wale askari wa *VGS* ambao wako vijiji vyote na kuwatengea posho, ili kupunguza hizi athari na kutokana kwamba watumishi hawa wa wanyamapori wako saba tu Wilaya nzima? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, wanyama wakali wakiwadhuru binadamu kwa maana ya wakivunjika, wakapata ulemavu wanalipwa kifuta jasho cha shilingi 500,000 na wakiuwawa wanalipwa shilingi 1,000,000; wakiharibu mazao ekari moja shilingi 25,000.

Sasa ni kwa nini Serikali isi-*review* kanuni zao ili ije na uhalisia wa kuweza kutoa kifuta jasho ambacho kinakidhi ustahiki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hili la mwisho nadhani linalingana na yule aliyeuliza swali lake la msingi. Kwa hiyo, utatoa majibu hayo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimepokea maswali tisa ya nyongeza kwa Waheshimiwa mbalimbali na naomba niyajibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la Mheshimiwa Londo; ameuliza ni nini kauli ya Serikali? Kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi. Ni kwamba sasa hivi tunaangalia njia mbadala wakati huo huo tunaendelea kutatua migogoro hii ya wanyama wakali na waharibifu. Tunajenga vituo, tunaajiri *VGS,* lakini wakati huo huo tumeshaweka sasa mipango kwenye baadhi ya maeneo tuanze kuweka *fence* ya umeme ili kupunguza hii athari ya wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la Mheshimiwa Anne Malecela, naomba niahidi mbele ya Bunge lako hili Tukufu kwamba baada ya Bunge hili tutaongozana naye katika maeneo yale. Lakini pia tumeshaanza kuongeza nguvu kwake, tumepeleka askari na tutaendelea kuajiri *VGS* katika maeneo hayo ili tuweze kushirikiana pamoja. Kwa hiyo, wananchi wa Same kilio chenu kimeshasikika Bungeni na tutaongozana na Mheshimiwa Mbunge *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hili la Mheshimiwa Vita Kawawa, ni kweli Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi ya ujenzi wa madarasa katika jimbo lake, na huu ulikuwa ni mpango wa *CSR* si kwa ajili ya fidia ya wanyama wakali na waharibifu. Ni kwamba Mheshimiwa Waziri alifanya ziara katika jimbo hilo na akatoa ahadi ya ujenzi wa madarasa ili kuwafanya wananchi wanaoishi katika maeneo hayo tushirikiane pamoja katika uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee tu kuahidi kwamba ahadi ni deni, Wizara itatekeleza. Na kwa kuwa ilikuwa ni kauli ya Mheshimiwa Waziri basi tutafuatilia ili ahadi hii iweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dunstan, Mbunge wa Mkinga, yeye ameongelea kuhusu kituo; niahidi tu kwamba katika mpango wa fedha wa 2023/2024 uliopitishwa katika Bunge lako hili, tutapeleka kituo katika Jimbo la Mkinga ili tuongeze nguvu ya kudhibiti wanyama wakati na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Justin Nyamoga, madhara makubwa; naomba niahidi tu kwamba tutaendelea kufuatilia katika maeneo haya ili wananchi waweze kulipwa fidia inayotokana na wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Grace Tendega; naomba tu nilitaarifu Bunge lako, na kwa ridhaa yako, nipe tu nafasi kidogo nitoe ufafanuzi. Tumekuwa na changamoto nyingine imejitokeza katika Mkoa wa Iringa; kuna uvamizi wa simba kwenye baadhi ya maeneo, lakini naomba niwataarifu wananchi, nadhani wameona juhudi za Serikali toka uvamizi huu umejitikeza tumekuwa karibu na wananchi, tunatoa elimu.

Mheshimiwa Spika, naniendelee kutoa elimu kupitia Bunge lako hili, kwamba wakati huu ambapo tunawasaka hawa simba, wananchi wawe na tahadhari ya kutotembea usiku. Lakini pia wenye mifugo wawashe moto kuzunguka maeneo yale ya mifugo ili kuepusha simba wasisogee katika maeneo hayo tunajitahidi sana kulinda maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe Wanairinga, Serikali iko kazini na tumeshapeleka helikopta inazunguka usiku na mchana kuhakikisha tunawasaka hawa simba. Tuendelee kushirikiana pamoja ili kuhakikisha zoezi hili tunalikamilisha na simba hawa tunawachukua na kuwarudisha katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mheshimiwa Charles, Mbunge wa Mwibara; kumekuwa na changamoto ya viboko na tembo. Naomba niendelee tu kuahidi, nakumbuka tuliwasiliana na Mheshimiwa Mbunge na tukaongeza nguvu ya askari katika maeneo hayo. Tuendelee tu kuwasiliana, nguvu tutaongeza lakini pia tutaendelea kuajiri *VGS* ili waweze kusaidia pale inapotokea dharura katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ombi la Mheshimiwa Jimbo la Tunduru kwamba tuongeze *VGS* (askari wa vijiji). Tunaomba tulipokee hili na tutaweka *priority* katika eneo hili, tunajua hii changamoto ya wanyama wakali.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna shida moja ya mratibu ambaye alihamishwa. Nadhani maelekezo yameshatoka, atarudishwa katika eneo hilo ili aweze kushirikiana na wananchi kudhibiti wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Matiko tayari nimeshalijibu, kwamba tuko kwenye *process* ya ku-*review* hizi sheria na kanuni kuangalia sasa angalau tusogeze kiwango fulani ili wananchi nao waweze kuona umuhimu wa namna ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, una swali lingine. Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi kuzungumza kwa sauti ya chini, mkizungumza kwa sauti kubwa sana, humu ndani kwa sababu hii nyumba imefungwa kuna muda mtawaacha mzungumze halafu mjisikie wenyewe. Kwa hiyo, sauti inasikika hapa katikati halafu inasambaa inakuwa kubwa sana. kwa hiyo, jitahidi uzungumze kwa sauti ya chini. Najua mnaongea mambo ya msingi sana Wabunge, mnaomba mambo kwa Mawaziri, Mawaziri lazima wawajibu, na ninyi Wabunge mnashirikishana huko mambo ya

majimbo, lakini zungumzeni kwa sauti ya chini kwa sababu mkizungumza kwa sauti ya juu wlae kule juu wanasikia zaidi kuliko ninyi mnavyosikilizana humu ndani. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, sasa aulize swali lake.

Na. 725

**Sehemu ya Pori Mabwepande kutengwa kwa ajili ya sekondari**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza: -

Je, Serikali ipo tayari kutenga sehemu kwa ajili ya shule ya sekondari katika Pori Tengefu Mabwepande lililopo Kibesa, Jimbo la Kibamba?

**SPIKA:** Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Jimbo la Kibamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba Pande lenye ukubwa wa kilometa za mraba 15.39 limetengwa kwa sababu kuu zifuatazo; kufyonza hewa chafu *(carbon sink)* inayotokana na shughuli za kibinadamu ili isisababishe madhara kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, na kuhifadhi mimea na viumbe hai wengine kama wadudu na wanyamapori ambao ni muhimu katika kuhakikisha mifumo ikolojia ya maeneo husika inaimarika na kutoa huduma za kiikolojia. Aidha, eneo hilo pia linatumika kwa shughuli za utalii na kwa sasa Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya utalii ndani ya pori hilo ili kuvutia watalii wengi na kuongeza mapato yatokanayo na utalii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo na kuzingatia kwamba eneo hilo ni dogo, Wizara haioni busara kuendelea kumega eneo hilo kwa shughuli za kijamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, naomba niulize swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wale wa Kibesa sehemu ya Mpiji Magohe, wanatembea kilometa 8.2 kufuata sekodari pale *Mpiji Center.*

Je, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kuja ili uone ushuhudie ile adha ya wananchi wale wanayopata ili mimi na wewe tushirikiane kufuata taratibu, sheria na miongozo ili waweze kupewa hilo eneo katika sehemu ya hifadhi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Jimbo la Kibamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, eneo nalifahamu na nilishafanya ziara mara nyingi. Na ukiangalia jibu la msingi, nimejibu kiufasaha, kwamba maeneo ni machache na Jiji la Dar es Salaam linaendelea kukua, tukikosa maeneo ya kupumulia watu wanazidi kuongezeka lakini tukaendelea kunyima maeneo ambayo angalau watu wanapopumua…

**SPIKA:** Waheshimiwa mliosimama tafuteni mahali mkae. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba haya maeneo tunayatenga, si kwa sababu tu ya msuala ya utalii.

Serikali inatambua kwamba kuna umuhimu wa ku-*balance* ikolojia. Kuna maeneo kama Pugu tumetenga ile Kazimzumbwi na upande wa Kibamba na huku kaskazini tumetenga hili Pori la Mambwepande. Lakini lengo ni kuifanya Dar es Salaam ipate maeneo ya kupumulia kwa sababu watu wanazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu, kilometa za mradba katika eneo hili ni 15 tu, ni chace sana. tulitamani hata ziwe nyingi. Sasa tukiendelea kuzimega tena, kwanza tunawafanya wana-Dar es Salaam wakose pa kupumlia; cha pili, ni kufanya sasa maeneo mengi ambayo tunajitahidi kuyatunza kwa ajili ya ku-*balance* ikolojia yatakuwa yanazidi kupungua zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 726

**Fidia kwa wananchi wa Kahe/Chekereni – Njiapanda**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza: -

Je, lini Serikali italipa fidia kwa maeneo ya Kahe/Chekereni na Njiapanda yaliyochukuliwa na *TANROADS* mwaka 2013?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekwenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 Serikali ilifanya na kukamilisha uthamini kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi 146 watakaoathirika na ujenzi wa mradi wa vituo vya ukaguzi wa

pamoja wa magari ya mzigo *(One Stop Inspection Station)* ambapo kiasi cha shilingi bilioni 5.048 kilihitajika kuwalipa waathirika hao lakini hawakulipwa kutokana na Sheria Na. 7 ya Mwaka 2016 ya Uthamini na Usajili.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANROADS* Mkoa wa Kilimanjaro, inarudia zoezi la uthamini ulioanza tarehe 10 Mei, 2023 ambapo zoezi hilo lipo kwenye hatua za mwisho kukamilika. Baada ya zoezi hilo kukamilika waathirika watalipwa fidia zao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili licha ya majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inaweza ikanihakikishia kwamba wananchi wa Uchira, ambao nao walipisha ujenzi wa upanuzi wa barabara hii inayotoka Arusha – Moshi kwenda Holili, je, nao watalipwa chini ya mchakato huu ulioanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, lini sasa barabara hii itaendelezwa toka pale ilipoishia Tengeru, eneo la Arusha kuja Moshi, Himo mpaka Holili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, swali lake la pili sijalipata vizuri, kuhusiana na hii *One Stop Inspection Station,* swali la pili la nyongeza aliloliuliza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kuhusu uendelezwaji wa barabara hii kutoka pale iliyoishia; Tengeru – Himo – Holili. Hii barabara ni ya muhimu sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba Mheshimiwa Dkt. Kimei kwa kweli suala la malipo ya fidia kwa hawa wananchi limekuwa ni suala ambalo kila tunapokutana na kuja ofiini analifwatilia, lakini tumelitolea majawabu na kwamba sasa tunakamilisha.

Mheshimiwa Spika, swali lake kuhusu wananchi ambao pia watapisha ujenzi, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa tulifanya tathmini siku za nyuma, tutarudia ku-*review* zile tathmini ili ziendane na muda wa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Tengeru kuja huku Holili; *JICA* walishakubali, tumelijibu mara kadhaa, tutajenga hiyo barabara kwa kusaidiana na wenzetu wa Japan, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale wanapenda kujua upembuzi yakinifu kuhusu barabara yao kutoka Kahama – Nyang'hwale mpaka Busisi, Sengerema utakamilika lini? Leo takribani miaka mwili tunaulizia jambo hili hatupati majibu, naomba majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita nilijibu pia hili swali. Hii barabara inahusisha mikoa takribani mitatu; Shinyanga, Geita na Mwanza. Upande wa Mwanza wanafanya Mkoa wa Mwanza, lakini kwa upande wa Shinyanga na Geita wanaosimamia

upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ni *TANROADS* Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba walishakamilisha taratibu zote za kumpata Mhandisi Mshauri. Kwa hiyo, kazi inategemewa kuanza kwa sababu ni utekelezaji wa bajeti hii na wataendelea pia katika mwaka ujao wa fedha kuhakikisha kwamba wanakamilisha kuunganisha hiyo mikoa mitatu kupitia hiyo barabara aliyoitaja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 727

**Ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi wa Magari – Manyoni**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi wa Magari cha Muhalala – Manyoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Muhalala Manyoni ulisimama kutokana na mkandarasi kusitisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo hicho tarehe 11 Septemba, 2018 ukiwa umefikia 60.1%.

Mheshimiwa Spika, kusitishwa kwa ujenzi wa mradi huo kulisababisha mkandarasi kuingia katika mgogoro wa kimkataba na Serikali. Hivi sasa Serikali iko katika hatua ya kukamilisha

makubaliano ya stahili za pande zote mbili kati ya Serikali na mkandarasi. Aidha, kwa kuwa Mkataba wa Ufadhili chini ya Jumuiya ya Umoja wa Ulaya *(EU)* bado unaendelea, Serikali itaendelea na mchakato wa kutafuta mkandarasi mwingine atakayemalizia kazi zilizobaki mara baada ya makubaliano ya stahili kukamilika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, na kwa kuwa mradi huu umechukua miaka sita sasa tangu ulipositishwa, ninayo maswali mawili ya nyongeza: -

Mheshimiwa Spika, je, ni lini sasa Serikali itakamilisha mchakato wa kupitia hasara zilizosababishwa na kusimamishwa kwa mkataba huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kumpata mkandarasi mpya ili kazi ya ujenzi wa mradi wa Mhalala uweze kuanza? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyonyeza ya Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza, Benki ya Maendeleo ya Ulaya iko tayari, na fedha zipo kwa ajili ya kuendeleza. Kilichokuwa kinachelewesha ni kwamba baada ya kuingia mgogoro wa kimkataba ilikuwa ni lazima Serikali ihakikishe kwamba wanakaa pamoja na mkandarasi huyu ili waweze kukamilisha changamoto zote zilizokuwepo, wakishakubaliana sasa ndiyo waingie mkataba kutafuta mkandarasi mwingine wa kukamilisha.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni imani ya Serikali kwamba kwa mwaka tunaoanza wa

fedha tutahakikisha kwamba mkandarasi anapatikana, na kazi iliyobaki, Kituo cha Ukaguzi hiki cha Muhalala pamoja na kile cha Nyakanazi, kwa sababu vyote vilisimama kwa pamoja vinaanza kujengwa na kukamilika kwa sababu ni muhimu sana kwa ajili ya kulinda barabara zetu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 728

**Kuboresha miundombinu ya Chuo cha *VETA* Kitangari**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaboresha miundombinu ya Chuo cha *VETA* Kitangari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza baadhi ya majengo yanayokosekana katika Chuo cha *VETA* cha Kitangari ili kuimarisha uwezo na ufanisi katika kutoa mafunzo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* imetenga fedha kiasi cha shilingi 666,904,745.01 kwa ajili ya kukiimarisha Chuo cha *VETA* Kitangari ikiwemo ujenzi wa

mabweni, jiko, bwalo la chakula, madarasa na nyumba za watumishi. Ujenzi wa majengo hayo umeanza mwezi Mei, 2023, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, *VETA* Kitangari inahudumia majimbo mawili; Newala Mjini pamoja na Newala Vijijini, kwa hiyo, inasababisha usafiri wa wanafunzi kutoka kwenye maeneo yao kwenda katika eneo *VETA* ilipo ni mbali. Ujenzi ambao umetajwa na Serikali hauhusishi bweni la wavulana katika *VETA* hii.

Je, ni lini Serikali itaweka kwenye mpango ujenzi wa bweni la wavulana katika *VETA* ile ya Kitangari ili kuleta urahisi wa usafiri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; linahusu watumishi, katika fani za umeme, ushonaji na uhazili, kuna mwalimu mmoja mmoja kiasi kwamba akipata dharura wanafunzi wale hawasomi.

Je, lini Serikali itapeleka walimu katika fani hizo, angalau mmoja mmoja, ili kuleta ufanisi na usomaji mzuri kwa wanafunzi katika *VETA* Kitangari? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtanda, Mbunge wa Newala kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha eleza kwenye majibu ya swali la msingi, kwamba katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi milioni hizo 666 na katika fedha hizi tayari tumeshapeleka milioni 304 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa baadhi ya majengo. Kwa hiyo nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli ujenzi wa bweni ukawa bado kutokana na fedha

iliyopelekwa. Lakini naomba nimhakikishie fungu lililobaki kati ya ile milioni 666 tutakapopeleka fungu hili la pili, ujenzi wa bweni hilo utakuwa umeanza na tutaendelea nao kwa kadri ya fedha tutakavyokuwa tunapeleka.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili la watumishi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu; Mheshimiwa Rais alitoa kibali cha kuajiri watumishi 514 katika mwaka huu wa fedha na mpaka sasa tumeshaajiri watumishi 169. Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na eneo la Newala lakini tunafahamu tuna vyuo vya zamani na tuna vyuo vipya 25 vile vya Wilaya, vinne vya Mikoa tunakwenda kuwapangia walimu maeneo haya ili kuhakikisha kwamba taalum hii inaweza kutolewa katika maeneo hayo kwa uhakika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilayani Rombo kwa kuwa Halmashauri imeshatoa eneo na wataalam wa ardhi wameshafanya uchambuzi na kuona linafaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Zuena kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa vyuo 68 vya wilaya zilizobaki, Rombo ni miongoni mwa Wilaya ambayo inakwenda kujengewa chuo hicho. Kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kazi kule Rombo tayari imeshaanza. Tumefanya *geo technical*, *topographical, environment impact assessment,* na tayari tumeshatambua eneo na shughuli zimeshaanza katika mwaka huu wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

Na. 729

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA*- Busanda**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* Busanda ili kiweze kutoa elimu ya uchimbaji madini na hatimaye kuongeza tija kiuchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Vyuo vya Ufundi Stadi nchini ili kuwapatia ujuzi wananchi utakaowawezesha kutekeleza shughuli za kiuchumi katika maeneo yao. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilipeleka fedha kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni 4.2 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Geita kilichojengwa katika Halmashauri ya Mji wa Geita. Ujenzi wa Chuo hiki upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Busanda ipo katika Wilaya ya Geita, Serikali inaomba wananchi wa Busanda kutumia chuo hicho cha Mkoa kilichojengwa katika Wilaya ya Geita ambapo elimu ya uchimbaji wa madini itatolewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bryceson Magessa swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali

la kwanza, kwa kuzingatia idadi kubwa ya wananchi katika Jimbo la Busanda ambayo ni takribani laki saba.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kujenga Chuo cha *VETA* kwenye maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, kwa vile jibu la msingi linathibitisha kwamba Chuo hicho kimejengwa Geita Mji na sisi tuko Geita Vijijini.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Chuo cha *VETA* Geita vijijini badala ya Geita Mji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tumaini Magessa kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha eleza kwenye maswali ya msingi kwamba tuna chuo ambacho tumejenga pale Geita; lakini ni sera ya Serikali kwa Awamu hii ya Kwanza kujenga vyuo hivi katika ngazi za Wilaya, na tutakapokuwa tumekamilisha ujenzi huu katika ngazi za Wilaya ambapo mnafahamu Waheshimiwa Wabunge wote katika mwaka huu Mheshimiwa Rais ametoa zaidi ya bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo katika zile Wilaya ambazo tumekosa na katika Mkoa mmoja wa Songwe ambao ulikuwa hauna chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kukamilisha awamu hii, tutafanya tathmini na kuona maeneo yapi yana idadi kubwa ya wananchi au ya wakazi na kuweza kuangalia namna gani tunaweza tukasogeza huduma hii karibu na maeneo hayo likiwemo na hili eneo la Busanda. Vile vile tunaweza kuzingatia katika Halmashauri au Wilaya ambazo zina Majimbo au Halmashauri zaidi ya moja kuweza kuwafikishia huduma hii katika Halmashauri hizo kulingana na upatikanaji wa fedha lakini vile vile na kukidhi kwa sifa za maeneo hayo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona mliosimama lakini muda wetu umekwenda sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani Mbunge wa Nkasi Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 730

**Mchakato wa kutoa maji Ziwa Tanganyika**

**MHE. AIDA J. KHENANI** atauliza: -

Je, mchakato wa mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika umefikia wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Mary Prisca Mahundi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika kuwapatia wananchi wa Mkoa wa Rukwa huduma ya majisafi na salama. Usanifu kwa ajili ya kuwapatia wananchi maji katika vijiji 40 vya pembezoni mwa ziwa umekamilika na tayari wananchi kwenye vijiji tisa wanapata maji na miradi inaendelea kutekelezwa kwenye Vijiji vilivyobaki hatua kwa hatua. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itaajiri mtaalam mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa miradi ya maji kupitia chanzo cha Ziwa Tanganyika ili kunufaisha maeneo mengi zaidi Mkoani Rukwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesikia majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ninazungumzia kata 97 za Mkoa wa Rukwa ambazo hazina maji kutoka Ziwa Tanganyika na hapa wanasema wamejiandaa kwa mwaka wa fedha kumwandaa mtaalam mshauri.

Je, ni lini utaratibu wa kumpata huyo mtaalam mshauri na *process* kuanza mpaka mradi kukamilika kuanza kutoa maji kwa Mkoa wa Rukwa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, mwaja jana kata tano za Jimbo la Nkasi Kaskazini, tulinunua maji ndoo moja shilingi 800 mpaka 1,000.

Je, mna mkakati gani wa dharula wa kuweza kupeleka maji kwenye hizo kata wakati tunasubiri mradi mkubwa wa Ziwa Tanganyika ambao ndio suluhisho la jambo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Aida Khenani, amefuatilia hili suala kwa muda mrefu na sisi kama Wizara tunakupongeza na hatutakuangusha na hatutakuwa kikwazo. Hizi Kata zote tutakuja kuhakikisha zinapata maji safi na salama. Lakini kwenye hizi kata tano za swali lako la pili, mkakati wa Wizara kwenye maeneo ya aina hii ni kutumia vyanzo vya maji rafiki vilivyokaribu, ikibidi kuchimba visima. Na kwa sababu tayari tuna magari basi tutachimba na kuweza kujenga vichotea maji na kuwasambazia wananchi ili kupunguza adha ya maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba sasa aulize swali lake.

Na. 731

**Mgogoro wa ardhi wa Shamba la Kambenga**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza: -

Je, lini mgogoro wa ardhi wa Shamba la Kambenga utatatuliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angelina Mabula majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Kijiji cha Namwawala ilimpatia Ndugu Kassim Seif Kambenga ardhi yenye ukubwa wa ekari 1,000 mwaka 1989. Mgogoro uliibuka miaka ya 2000 baada ya Serikali ya Kijiji cha Namwawala kugawa ekari 900 kati ya 1,000 kwa wananchi wengine kutokana na ndugu Kambenga kufanya upimaji wa awali na kukamilisha umilikishwaji wa ekari 100 tu. Mgogoro huu ulifikishwa kwenye vyombo vya sheria hususan Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kupitia Shauri Na. 2/2007 na Mahakama Kuu (Kitengo cha Ardhi) kupitia Shauri Na. 2/2012 ambapo Kassim Seif Kambenga alipewa ushindi kuwa ni mmiliki halali wa shamba lenye ekari 1,000.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mahitaji ya ardhi ya wananchi wanaozunguka shamba hilo, Serikali kupitia uongozi wa Wilaya na Mkoa inaendelea na mazungumzo na familia ya ndugu Kassim Seif Kambenga ili akubali kumega kiasi cha shamba lake kwa ajili ya kuwapatia wananchi. Hivyo, wananchi wanaombwa kuwa na subira wakati Serikali inapoendelea kushughulikia suala hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa msingi wa maamuzi wa Mahakama unatokana na *offer* iliyotolewa tarehe 2 Julai, 1990 na *offer* hiyo ilikuwa ni ya miaka 33 mpaka leo tukihesabu ndugu Kambenga hana umiliki tena wa shamba hilo;

(a) Je, Serikali pamoja na nia njema ya mazungumzo yanayoendelea haioni sasa imefika wakati wa kurejesha shamba hilo kwa wananchi?

(b) Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi kwenda kusikiliza wananchi hawa ili asikilize kilio chao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kunambi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na *offer* ya miaka 33 na *offer* ikaisha haimnyimi uhalali kama ameomba tena kuendelea kulimiliki, na wakati huo huo kama hakuna mwombaji mwingine ambaye ameomba maana yake lile eneo linaweza likawa liko wazi kwa ajili ya wengine. Mpaka sasa tunavyoongea mwenye shamba hilo bado analitumia kwa hiyo tunaweza kusema kwamba bado anayo haki yake kwa ajili ya kumiliki eneo lile kwa sababu mpaka sasa hakuna mwombaji mwingine yeyote aliyeomba eneo lile.

Mheshimiwa Spika, suala la pili la lini niko tayari kuambatana naye, tutaangalia ratiba kwa sababu tayari tukimaliza Bunge hili tumeshajipangia ratiba ya kuzunguka katika Mikoa, tutaangalia Morogoro iko lini na tutafika kama iko kwenye awamu hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 732

**Malipo ya mafao kwa watumishi wa Kiwanda cha Magunia Moshi**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa mafao yao watumishi waliokuwa Kiwanda cha Magunia Moshi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipokea madai ya waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Magunia Moshi na kuyashughulikia kwa kuunda Kamati ya Uhakiki. Taarifa ya Kamati hiyo ilibainisha kuwa Watumishi hao walishalipwa mafao yao na kujulishwa kwa barua yenye Kumb. Na. CKB.87/406/02/C/80 ya tarehe 3 Mei, 2019. Hata hivyo, pamoja na kuwajibu, wadai wameendelea kuandika barua kwenda kwenye Taasisi mbalimbali za Serikali kuwasilisha malalamiko yao; na kwa upande wetu tumekuwa tukiwajibu na kutoa ufafanuzi kuwa walalamikaji hao walilipwa stahiki zao ipasavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa majibu ya Serikali, lakini nina ushahidi kupitia kwa Mwenyekiti na Katibu wa Wastaafu hawa, na pia wamepeleka vielelezo vyao kwa Waziri Mheshimiwa Ndalichako kwamba mpaka sasa hawajalipwa stahiki zao;

Je, nini kauli ya Serikali kuweza kuwalipa wastaafu hawa haki zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, hii Kampuni ya Magunia mwaka 1996 baada ya kuona haiendeshwi kwa faida iliamua kuwapumzisha au kuwastaafisha wafanya kazi hao lakini pia mwaka huo huo iliingia mkataba wa hiari kwa watumishi hao baada ya kukubaliana kustaafu kwa maana ya kupata mshahara wa mwezi mmoja, malimbikizo ya likizo, malimbikizo ya mishahara, gharama za kusafirisha mizigo na malimbikizo ya michango mingine baada ya kuingia mkataba wa hiari kwamba watalipwa kama vibarua kwa siku shilingi 1,000 na wangelipwa marupurupu mengine kama kiwanda kingepata faida.

Mheshimiwa Spika, lakini kiwanda hiki baada ya kuona kinashuka faida mwaka 1998 kilibinafsishwa kwenda kwenye kampuni ya *TPM* ambayo ni Kampuni tanzu ya *Mohamed Enterprises*. Kwa hiyo, maana yake madai haya nadhani ndio hayo ambayo walidhani watalipwa kama kiwanda hiki kingeweza kupata faida kwa wakati huo, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 733

**Kuvutia wawekezaji wa Viwanda vya Chumvi – Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvutia Wawekezaji wa Viwanda vya kuchakata Madini ya chumvi Wilayani Kilwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Serikali kuvutia wawekezaji katika sekta ya Chumvi unaendelea ikiwa ni pamoja na kutenga eneo lenye ukubwa wa hekta 168 katika Wilaya ya Kilwa kwa ajili ya wawekezaji wenye nia ya kuchakata madini ya chumvi.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Serikali imeendelea kutoa vivutio mbalimbali vya kikodi na visivyo vya kikodi kwa uratibu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* kwa kushirikiana na Taasisi husika ili kufanikisha azma ya kuwekeza katika sekta husika kwa maana ya sekta ya madini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, na ahsante sana Serikali kwa kunijibu swali langu vizuri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, napenda kuiuliza Serikali; kwa kuwa biashara ya wazalishaji wetu wa chumvi katika Mkoa wetu wa Lindi imekuwa ikiathiriwa na waagizaji wa chumvi kutoka nje ya nchi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia hawa wafanyabiashara wadogo wadogo waanze kufanya biashara ya chumvi kwa ufanisi?

(b) Je, Serikali sasa haioni wakati umefika wa kuweza kuwa na bei elekezi kwa zao hili la madini ya chumvi kwa Mkoa wetu wa Lindi ili kuhakikisha kwamba hawa wafanyabiashara wa chumvi katika Mkoa wetu wananufaika na biashara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto katika sekta hii ya chumvi kwa maana ya baadhi ya viwanda kuagiza malighafi ya chumvi kutoka nje badala ya kuchukua chumvi inayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tulishatoa maelekezo na hili ni agizo la Serikali, kwamba wenye viwanda wote wanaozalisha chumvi hapa nchini watumie malighafi kwa maana ya chumvi inayozalishwa nchini, kwa hiyo tulishatoa marufuku kuagiza chumvi kutoka nje ya nchi kwa ajili ya viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu bei elekezi, tunashukuru kwa sababu tunadhani biashara zinatakiwa ziende kwa uhuru, kwa maana ya *supply and demand,* lakini pale inapotokea hoja mahsusi muhimu kama hii tutangalia ikiwa kuna ulazima wa kuweka bei elekezi kwa ajili ya kuona wananchi wa Tanzania, na hasa wanaozalisha chumvi ghafi, waweze kupata bei nzuri inayouzwa kwenye viwanda vya Tanzania, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta tangazo la wageni nililonalo hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika, ninao wageni kutoka BAKWATA Mkoa wa Singida na hawa ni Alhaj Bumham Mohamed Amri Mlau, Mzee Juma Hamis, Mzee Ramadhan Isango, Mzee Omary Mugheny, Ndugu Athumani Shumbi na Sheikh Jumanne Maghasi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni kutoka BAKWATA Mkoa wa Singida ni wageni wangu, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile yupo Ndugu Harris Kapiga, mfanyakazi wa *Clouds Media* na Mchungaji wa Kanisa la Ahadi kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine ambao ni wageni wa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambao ni mke wake Neema Mwigulu Nchemba ameambatana na mtoto wake Gracious Nchemba, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 83 wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na hawa ni Ndugu Jonathan Mabiaya, Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro; Ndugu Anthony Tesha - Mwenyekiti wa CCM kutoka Rombo; Ndugu Mary Sule - Katibu wa CCM Rombo; Ndugu Gilbert Tarimo - Mwenyekiti Halmashauri ya Rombo na huyu kama ni Mwenyekiti bila shaka ni Mheshimiwa Diwani, lakini hapa naona imeandikwa ndugu; na yupo pia Ndugu Ladslaus Maunga - Mwenyekiti *AGAPE Group,* Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Exaud Kigahe ambaye ni Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara na hawa ni Viongozi wa UVCCM kutoka Mufindi, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Neema Mgaya ambao ni wafanyakazi wa *Mizani Financial Consultancy Limited* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Esther Malleko ambao ni familia yake wakiongozwa na mama yake mzazi, Saphia Islam kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mtaalam wa *IT* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni viongozi wa UWT kutoka Babati, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Ghati Chomete kutoka Tarime, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi kutoka Ubalozi wa Japan. Pia Mheshimiwa Chumi anao wageni wengine wanne ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambao ni viongozi wa BAKWATA kutoka Manyoni, Mkoa wa Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Husna Sekiboko ambao ni watoto wake kutoka Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Biumrah Sekiboko, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga ambao ni Wachungaji wa *Church of God* kutoka Mbogwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 39 wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa John Noya na Mkurugenzi wa Halmashauri Bi. Anna Mbogo, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri mnaozungumza siwaelewi ni kwamba mimi ndio sieleweki ama ninyi ndio hamuelewi? Waheshimiwa Wabunge ambao huwa

mnazungumza na simu humu ndani nitaanza kutaja mmoja baada ya mwingine na tusilaumiane.

Pia ninyi mnaozungumza nikiwa nimesimama nitakuwa nawataja ili wengine wasijisikie vibaya kwamba narudia matangazo hayo hayo kila wakati. Kwa hiyo, ni vizuri wafahamike wanaozungumza na simu pamoja na Spika kukataza ni akina nani? Wanaopiga kelele pamoja na Spika kukataza ni akina nani? Kwa sababu wakati mwingine tunawalaumu walimu bila sababu za msingi ikiwa sisi wenyewe humu ndani tunashindwa kuelewana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Latifa Juwakali ambao ni Wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa kutoka Mkoa wa Kusini, Unguja wakiongozwa na Mwenyekiti wao wa UVCCM, Mkoa wa Kusini Unguja, Ndugu Phidelist Daniel, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Kamati ya Utendaji UVCCM, Wilaya ya Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava ambaye ni Katibu wa UVCCM, Kata ya Makumba Wilaya ya Korogwe, Mkoani Tanga, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham ambao ni familia yake, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoka Jimbo la Chalinze, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa Salim Mussa Omar ambao ni wanafunzi na walimu wa *Genius Kids* kutoka Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 19 wa Mheshimiwa Francis Mtinga, Makatibu wa CCM wa Kata za Wilaya ya Mkalama, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni wafanyakazi kutoka *Simba Sport Club*, karibuni sana *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Cecil Mwambe, walezi na watoto kutoka Jimbo Katoliki la Lindi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Santiel Kilumba ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 55 na walimu watano kutoka Shule ya Awali na Msingi *Great Vision* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni asubuhi hii, lakini liko tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Fedha na Mipango itaendesha semina kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Kazi wa *FATF* pamoja na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Waheshimiwa Wabunge, Semina hii itafanyika leo siku ya Jumatatu tarehe 26 Juni, 2023 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana. Semina hii itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa katika semina hii na ni muhimu sana sote tuhudhurie.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI**

**26 JUNI, 2023**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**
**na**
**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza miaka miwili ya uongozi wake makini unaoleta mageuzi makubwa kielimu, kisiasa, kijamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na Naibu wake na watendaji wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu nauelekeza kwenye mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuangalia sekta mbalimbali. Nampongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maendeleo anayozidi kuyatoa kwani shilingi bilioni 1.0 zimewekwa kwenye mfuko wa walemavu kwa ajili ya kusaidia vifaa vinavyohitajika, pia fedha hizo zitatumika kwa Mfuko wa Wabunge wa Kundi la Watu Wenye Ulemavu mchango kwa watoto wanaolelewa kwenye vituo maalum.

Mheshimiwa Spika, tunaomba makampuni binafsi kuchangia mfuko huu kwa kusaidia makundi haya maalum pamoja na programu zinazotolewa chini ya *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu naipongeza Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutengeneza jambo la kihistoria kwa kuwafutia ada wanafunzi wa kidato cha tano na sita na kufanya wasome kwa utulivu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga fedha ya kugharimia programu hiyo ambapo hadi mwezi Aprili, 2023 jumla ya shilingi bilioni 661.9 zimetolewa. Pia kutokana na mabadiliko ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 Toleo la mwaka 2023 na mabadiliko ya mitaala yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita Serikali imepanga kutoa elimu ambayo itamuwezesha mwanafunzi kujiajri au kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu kuondolewa kwa ada ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kupangiwa na Serikali kujiunga vyuo vya ufundi vya *Dar es Salaam Institute, DIT, MUST* na *ATC* ili kuongeza idadi ya wataalam wenye ujuzi na elimu inayohitajika katika zama hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji; ongezeko la bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294.0 mwaka 2021 mpaka shilingi bilioni 954.4 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kufikia shilingi bilioni 970.8 kwa mwaka wa fedha 2023 ongezeko hilo limesababisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo na kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo na kuanzishwa kwa mashamba makubwa ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imeendelea kusimamia usalama wa chakula kwa kujenga maghala 16 na vihenge 20 kwa ajili ya kuhifadhj mazao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi

wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha ubunifu wa ukusanyaji mapato na usimamizi mzuri wa matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa miradi ya kimkakati na pia utayari wetu wa Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu." Pia mapendekezo haya yanazingatia dhima ya bajeti 2023/2024 ambayo ni kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kuhimili na kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi, na kuimarisha sekta za uzalishaji ili kuboresha hali ya maisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za uchumi katika nchi nyingi duniani yakiwemo mataifa makubwa, Tanzania imefanya vizuri katika kusimamia ukuaji wa pato la Taifa lilikua kwa asilimia 4.7 ukilinganisha na wastani wa asilimia 3.9 kwa nchi za Afrika zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara; mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo kwa mwaka 2022 ulikuwa asilimia 4.3 ukilinganisha na wastani wa asilimia 11 kwa nchi za Afrika Mashariki; na thamani ya shilingi ta Tanzania dhidi ya dola imeendelea kuwa tulivu ambapo kwa mwaka 2022 ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,314.50 kutoka shilingi 2,309.2 kwa mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, pia pamoja na upungufu wa fedha za kigeni, bado akiba ya fedha za kigeni ilikuwa USD milioni 5,177.2 sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.7 kutoka akiba ya USD milioni 6,386 ya mwezi Desemba, 2021 sawa na miezi 6.6 ya uagizaji. Upungufu wa fedha za kigeni kwa kiasi kikubwa umesababishwa na mfumuko wa bei katika soko la

dunia, ulipaji wa madeni ya nje, pamoja na kugharamia miradi ya kimkakati. Hali hii imepelekea kuongezeka kwa nakisi ya urari wa malipo kufika USD milioni 4,414.2 kwa mwezi Julai, 2022 kutoka USD 2,516.1 kwa Julai, 2021.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa fedha za kigeni, napendekeza Serikali iendelee kwa kasi na jitihada za kununua na kutunza dhahabu kama sehemu ya fedha za kigeni. Ununuzi ulenge pia kununua dhahabu toka kwa wachimbaji wadogo hata kwa bei ya ushawishi ili kuzuia utoroshaji unaosababisha kupunguza mapato ya fedha za kigeni. Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi kidunia, Benki Kuu nyingi duniani zimeanza kuwekeza zaidi kwenye dhahabu na hii ni ishara nzuri kwa bei ya dhahabu kuendelea kuimarika kwenye soko la dunia ambapo kwa mwezi Aprili, 2023 bei imepanda kwa zaidi ya asilimia 11 ukilinganisha na bei za Desemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua nzuri za kurudisha Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji Wanaozalisha Bidhaa kwa Soko la Nje *(Export Credit Guarantee Scheme)* ambayo itachochea kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje. Pamoja na uanzishwaji wa mfuko huu, Serikali isimamie uzalishaji wa tija na pia kusaidia kupata masoko ya nje ili bidhaa zetu zipate bei ya kiushindani.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kulipa fidia ya wananchi wanaopisha Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Baada ya fidia, napendekeza Serikali kuchukua hatua za kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa chuma *(Liganga Iron Ore)* ikiwa ni pamoja na makaa ya mawe *(The Mchuchuma Coal Mining and Power Projects)*. Mradi wa Liganga na Mchuchuma unatarajia uwekezaji wa zaidi ya US$ bilioni tatu na kuzalisha ajira zaidi ya 30,000.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya Niobium ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha Ferroniobium *(FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,*

kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya Niobium ambayo yanapatikana *Panda Hill* Wilaya ya Mbeya, na mahitaji ya Ferroniobium *(FeNb end product)* yanaendelea kuwa makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji kujiwekekea mikakati ya haraka *(quick wins)* ili kuhakikisha inaimarisha uchumi ikiwemo kupunguza urari wa malipo ambao umefika USD milioni 4,414.2 kwa Julai, 2022 kutoka USD 2,516.1 kwa Julai, 2021. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini yakiwemo ya chuma, makaa ya mawe, na Niobium, kuna fursa ya kuvutia uwekezaji wa nje *(FDI)* ambao ni zaidi ya USD bilioni tatu katika kipindi cha miaka miwili mpaka mitatu. Pamoja na fursa ya ajira ya zaidi ya 30,000 kwa Liganga na Mchuchuma kuna fursa ya kuvutia uwekezaji *(FDI)* wa zaidi ya USD bilioni tatu, wakati huo huo Niobium ina fursa ya uwekezaji wa zaidi ya USD milioni 200 na kuzalisha ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs* 7,000.

Mheshimiwa Spika, mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(Modern Manufacturing Plant and Smelter)*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki wakati dunia inapambana na changamoto za kiuchumi, napongeza hatua za Serikali kwa kuwasilisha Muswada wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya *PPP,* Sura 103 na ambayo yamepitishwa na Bunge tarehe 13 Juni, 2023. Serikali imeonesha utayari wa kujenga reli ya Kusini ya Mtwara – Mbambabay na reli ya Kaskazini (Tanga-Arusha-Mara) kwa njia ya ubia baina ya Serikali na sekta binafsi *(PPP)*.

Napendekeza pia kuharakisha ujenzi wa barabara ya Kibaha – Morogoro (kilometa 205) na baadae Morogoro hadi Dodoma ili iweze kutekelezwa kwa utaratibu wa *PPP,* na iende sambamba na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma (kilometa 112.3).

Mheshimiwa Spika, pamoja na *PPP* napongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara saba zenye jumla ya urefu wa kilometa 2,035 zenye gharama ya takribani shilingi trilioni 3.7 kujengwa kwa kutumia mfumo wa *Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC+F).* Katika barabara hizo saba ni pamoja na barabara ya *TANZAM* kipande cha Igawa – Songwe – Tunduma (kilometa 218) pamoja na barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe (kilometa 48.9).

Mheshimiwa Spika, kutokana na fursa za uzalishaji mkubwa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, napendekeza muendelezo wa uboreshaji wa barabara za Mbalizi – Shigamba – Isongole kutokana na uzalishaji wa mazao ya kilimo; barabara ya Mbalizi – Galula – Makongolosi kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na madini; na pia barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete ambayo ni muhimu sana katika kusafirisha mazao ya kilimo ikiwemo maua, parachichi na viazi kwa soko la nje.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea kwa kasi ile ile na pia napongeza jitihada za kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya masharti nafuu kugharamia ujenzi huo. Pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, Serikali imefanya maboresho makubwa ya miundombinu na huduma katika bandari zetu hususana Bandari ya Dar es Salaam ili kukabiliana na ushindani mkubwa wa bandari zingine za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam inakumbana na ushindani mkubwa toka Bandari za Mombasa (Kenya), Beira (Msumbiji), Nacala (Msumbiji), Durban (Afrika Kusini), Lobito (Angola) na Walvis Bay (Namibia). Maboresho ya bandari zetu yaendane na kuondoa changamoto zingine ambazo zinasababisha gharama kubwa za usafirishaji kwa bandari zetu na

kusababisha kupoteza biashara ya usafirishaji kwa bandari shindani.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa bandari unategemea pia maboresho ya barabara, Reli ya Kati *(TRL),* Reli ya *TAZARA,* utendaji wenye tija wa wadau wote wa bandari na hata watumishi ili kupunguza gharama za usafirishaji kwa wateja wa bandari zetu. Kwa sasa karibu asilimia 70 ya mzigo wote wa nchi za nje unasafirishwa kwa kupitia *Dar es Salaam Corridor* ambapo *DR Congo* ni asilimia 38, Zambia asilimia 26 na Malawi asilimia sita. Pamoja na fursa za kijiografia ya bandari zetu, mzigo unaopita sasa kwenye Bandari ya Dar es Salaam, ni chini ya asilimia 50 ya biashara yote ambayo kwa sasa sehemu kubwa inashikiliwa na bandari shindani.

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali kwa maboresho ya uwanja wa ndege wa Songwe, na kutokana na maboresho hayo napendekeza kujengwe maghala *(cold rooms)* kwa ajili ya kuhifadhi mboga mboga, matunda, nyama na samaki kwa soko la nje. Uwanja wa ndege wa Songwe upo kimkakati kwa kuhudumia wafanyabiashara wa hapa nchini na pia nchi jirani za Zambia, DRC na Malawi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *ATCL* iboreshe muundo wake wa utumishi kulingana na biashara iliyopo ya usafiri wa anga ili kupunguza mzigo wa gharama na kuongeza ufanisi. Pia *ATCL* ianzishe njia za safari za ndani na za nje zenye fursa ya kuongeza biashara kama vile safari za moja kwa moja za Mbeya – Dodoma, Mbeya – Lilongwe, Mbeya Lubumbashi na Mbeya – Lusaka.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iangalie upya mapendekezo ya kuboresha muundo wa mfuko wa asilimia 10 kwa ajili ya mikopo kwa vijana, wakina mama na makundi maalum. Napendekeza mfuko huu uboreshwe na uwe sehemu ya mpango wa kuwawezesha kiuchumi makundi lengwa kwa misingi ya huduma za kifedha shirikishi *(financial inclusion).* Msukumo uwe kwenye elimu ya ujasiriamali na kuwasimamia kwa karibu wakopaji ili kuongeza tija na pia kuboresha uchumi wa wakopaji na Tanzania kwa ujumla.

Napendekeza pia kujumuisha huu mfuko uwe kitaifa na uendeshaji uwe katika misingi ya taasisi za kifedha, lakini kwa masharti nafuu ikiwemo bila riba na Serikali iunganishe mifuko yote ya makundi maalum na yaunde taasisi moja imara chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kupongeza hotuba nzuri ya bajeti ikiwa ni pamoja na hatua kadhaa ambazo zimeelezwa kama vile kurejesha *retention* ya 20% ya kodi za ardhi na majengo kwa Halmashauri zetu, kuanzishwa kwa *Single Window Payments System* pamoja na Taarifa ya Kamati ya Bajeti ikiwa ni pamoja na maoni, mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mchango wangu baadhi nimerejea mchango wangu wa Bunge la Novemba wakati Kamati zikiwasilisha taarifa za Kamati na mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya ninayorejea ni umuhimu wa Taifa letu kuhusu namna ambavyo itanufaika na fedha za mifuko ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi duniani. Zipo fedha kwa ajili ya *grants* ku-*support* nchi zinazoendelea katika kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi. Fedha hizi zingeweza kusaidia katika kujenga miundombinu ambayo itasaidia wakulima kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi. Mifuko kama *Green Climate Fund, Climate Investment Funds, Adaptation Fund* na *Global Environment Fund* baadhi ya hii mifuko inatoa mikopo ya riba nafuu au ku-*support* miradi ambayo inasaidia kupunguza ongezeko la *carbon.* Kwa mfano Rwanda wamepata *pound* milioni 24.5 ambazo zilisaidia kuanzisha *Rwanda Green Fund* ambayo imewezesha kutoa *renewable energy* kwa kaya 57,500 na ilizalisha *so called Green jobs* 137,500.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo nashauri mapendekezo ya kutoza shilingi 20 kwenye *cement* iondolewe na mbadala

wake iwe ni hizi fedha za mifuko niliyotaja kwa sababu nyingi kati ya fedha hizo ni *grants.*

Kuhusu *ATCL,* napongeza jitihada zote za kuongeza ndege, nashauri yafuatayo; pawepo *route* ya kutoka Dodoma kwenda kwenye Kanda Kuu kama vile kwenda Mwanza kwa maana ya *Lake Zone,* kwenda Mtwara kwa maana ya *Southern,* kwenda Mbeya kwa maana ya *Southern Highlands,* kwenda *KIA* na pia kwenda Kigoma. Ilivyo sasa kama abiria atatoka Dodoma anataka kwenda Mbeya, lazima kwanza aende Dar, akifika Dar anaanza upya safari na tiketi mpya kwenda Mbeya, hii sio sawa, tutafute namna ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, niliwasilisha mchango wangu wa kwanza kwa Maandishi na pia nilipata nafasi ya kuchangia kwa kuongea tarehe 21 Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu wa awali, naomba kuwasilisha tena mchango wangu wa maandishi kwa masuala kadhaa, kwanza ni kuhusu Mradi wa *REGROW;* Mradi huu wa kuimarisha utalii Kusini ulisainiwa Februari, 2018 na Mheshimiwa Rais wakati huo akiwa Makamu wa Rais. Lengo la mradi huu ambao ni mkopo wa Benki ya Dunia wa USD milioni 150 ni kuboresha utalii Kusini, ikihusisha kuimarisha miundombinu ya kuwezesha kuinua utalii kama vile *upgrading of 14 airstrips,* barabara kama kilometa 2000 ndani ya mbuga, njia za kutembea kwa miguu kilometa 350, ujenzi wa Kituo cha Taarifa za Kitalii pale Kihesa, Kilolo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni mradi ambao ulipaswa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano, lakini utekelezaji wake kwa kweli ni wa kusuasua. Nafahamu suala hili lipo Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini Wizara ya Fedha ndio mshiriki mkuu wa mijadala ya masuala yote ya mikopo na misaada, na mpaka kupatikana kwa fedha hizi USD milioni 150. Kwa hiyo inao wajibu wa kujua je, fedha hizi zinatumika kadri ya malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; kwa kuzingatia kwamba jitihada za kutangaza utalii kuanzia filamu ya *Royal Tour* zinaendelea kuongeza idadi ya watalii, ni muhimu sana mradi wa

*REGROW* kasi ya utekelezaji ikaongezeka na kwa kuwa kupatikana kwa fedha hizi Hazina ilihusika, ni vizuri pakawepo mfumo wa kuitaka Wizara ya Kisekta kutoa taarifa ya utekelezaji ya miradi husika. Kwa hiyo, natamani kuona Serikali ikitueleza suala hili linaendeleaje.

Kuhusu suala la kodi kwa magari ya abiria; katika ukurasa wa 101 wa hotuba ya bajeti, imependekezwa kuwa magari ya abiria yatozwe viwango kadri ya idadi ya abiria. Hata hivyo nashauri kodi hii itizame pia umbali ambao gari inasafiri. Kwa mfano yapo mabasi makuukuu yanayosafiri mikoani ndani ya Wilaya, kwa mfano hapa Dodoma, yapo mabasi yanatoka mjini yanaenda vijijini kama vile Mvumi, Mlowa Bahi na kadhalika. Yapo mabasi huko mikoani ambayo yanatoka makao makuu ya Wilaya yanaenda vijijini umbali usiozidi kilometa 100 na yanapita katika barabara ambazo wakati wa masika hazipitiki kwa wepesi, kwa hakika basi la aina hii linaweza kusafiri wiki moja, wiki ya pili lifikie gereji, ni yale mabasi tunayoyaita spana mkononi.

Mheshimiwa Spika, sasa basi kama hili ambalo nauli kutokana na umbali unaweza kukuta nauli ni shilingi 5000 kwa kiwango cha juu. Kwa mabasi ya abiria 65 ni sawa na makusanyo ghafi shilingi 325,000, hapo bado mafuta na gharama nyingine za uendeshaji kama vile *spare* na tozo mbalimbali, je ni sawa basi kama hili kutozwa shilingi 2,200,000 kwa mwaka?

Mheshimiwa Spika, nashauri viwango hivi vitizamwe upya na ikibidi vizingatie masuala kama uchakavu wa gari na umbali linalosafiri, na suala hili lizingatiwe pia kwenye magari ya mizigo.

Mheshimiwa Spika, magari ambayo yameanza kuchoka, kodi isiwe sawa na magari ambayo bado hayajachoka. Kwa mfano tuangalie umri wa gari kama moja ya kigezo, kwa sababu gari ambayo imeanza kuchoka, kwanza inatumia mafuta mengi hii inafanya gari hilo kununua mafuta mengi na hivyo Serikali inapata *fuel levy,* na pia gari la aina hiyo ambalo ni spana mkononi pia linatumia *spare* mara kwa mara ambapo pia Serikali inapata kodi kupitia kodi mbalimbali kutokea kwa wauza *spare*.

Kwa hiyo ushauri wangu kodi hii itazamwe na ikibidi izingatie umri wa gari na umbali inaosafiri kwa upande wa mabasi ya abiria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sewa ya ukaa, naomba Serikali irejee mchango wa Mheshimiwa Kakoso siku ya tarehe 20 Juni, 2023 kuhusu namna ambavyo tunaweza kunufaika kama Taifa na utajiri wa misitu kupitia biashara ya hewa ya ukaa. Hii ni biashara kubwa, lakini inayohitaji utaalam wa juu sana kwa sababu inataka sio tu umakini, lakini imejaa ulaghai mkubwa miongoni mwa makampuni. Kwa mfano sisi watu wa Mufindi, Kampuni ya *Green Resources Limited-GRL* walinunua maeneo mengi ya vijiji na wananchi katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Njombe, wamepanda miti na wanalipwa fedha za hewa ya ukaa, lakini wananchi na wanavijiji hawapati kitu.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu kwa Wizara ya Makamu wa Rais-Mazingira nimeshauri kwamba tuliwekee mkazo eneo hili kwa kushirikisha sekta binafsi na *NGOs,* hili ni eneo ambalo Serikali hatujalitizama kwa kina, kuna fedha nyingi sana na Mheshimiwa Rais ushiriki wake kwenye *COP 26 Glasgow* ulithibitika kwa sababu alikuwa jasiri akayaeleza mataifa makubwa kwamba yanapaswa kuheshimu ahadi zao za kutoa fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kwa sababu mataifa makubwa yanaongoza kuchafua mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, nashauri ndani ya Serikali tuweke mkakati maalum, tuwe na timu ya wataalam hata kwa kulipia, tuijue habari hii ya biashara ya hewa ya ukaa na masuala mazima yanayohusu mabadiliko ya tabia nchi, fursa zilizopo na kadhalika. Tusiwaze kupanda tu miti, zipo fursa nyingi, tujifunze Wilaya ya Tanganyika kwa kuanzia lakini tutumie Balozi zetu kama Ubalozi wetu wa Brasilia kujua nchi kama Brazil imefanikiwa vipi kunufaika na biashara ya ukaa na msisitizo wangu ni kushirikisha sekta binafsi, tusijifungie ndani kwa sababu ukweli ni kwamba utaalam wa suala hili ni wa kipekee, kwa hiyo, wakati huu tufanye ushirikishwaji, pia wakati huo huo kama ambavyo tuliwahi kuwa na mipango mahususi wa kuzalisha vijana wetu kwa ajili ya sekta ya *oil and gas* basi tutumie mfumo ule kuwekeza katika elimu kwa vijana wetu kwa ajili ya suala zima la

mabadiliko ya tabia nchi na yatokanayo ikiwemo biashara ya hewa ya ukaa.

Mheshimiwa Spika, naamini Serikali ikikaa na Mheshimiwa Kakoso na baadhi ya wataalam itaona wapi pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa uweza wake na napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu kwa kazi kubwa na nzuri inayoendelea kufanyika na hata zile alizoziibua kwa miaka hii miwili yote inaendelea kwa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi kwa jopo la Mawaziri wote na Naibu Mawaziri kwa kuungana na Rais Samia na Makamu wa Rais Mheshimiwa Mpango na Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa katika kuendeleza mpango mzima wa kuendeleza nchi yetu. Kazi Iendelee.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia jambo la *VAT* kuongezwa kiwango ndio itapelekea ukwepaji wa kodi na pia ndio inaleta kufanya mazungumzo kati y muuzaji na mnunuzi ya na risiti au bila ya risiti bila kuwa na uelewa wa ukusanyaji *VAT* bado ugumu wa ukusanyaji wa *VAT* utakuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, hapa tuangalie zaidi kuongeza wafanyabiashara, ni lazima kuhakikisha wigo unaongezeka ili kuhakikisha idadi ya walipakodi inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 70 wa hotuba ya Waziri wastani wa walipakodi kulingana na ukuaji wa wananchi na ongezeko la mahitaji kwa mwaka 2021/2022 walipakodi waliosajiliwa ni 4,455,028 lakini wenye *TIN* kati yao ni 1,641,173 ndio maana wafanyabiashara wengi wanakwepa *TIN* kwa kuona ni usumbufu wa tozo za Serikali.

Mheshimiwa Spika, niiombe Wizara iangalie mfumo mzuri wa malipo, kuwe na sheria inayosimamia malipo yaani angalau kuwe na muda maalum wa malipo kwa Serikali mfano malipo ya

*SDL*/*PAYE*/*WCF*/Mifuko ya Jamii/*VAT* na kadhalika. Pia iwepo tarehe maalum kila mwezi na usipolipa kwa muda kuwe na riba adhabu italipwa na muhusika wa kampuni iliyochelewesha malipo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho niishukuru Serikali yangu kwa miradi yote waliyoleta jimboni Temeke; vituo vya afya, shule za ghorofa, barabara za *TARURA* na kadhalika, lakini zaidi sana Mradi wa *DMDP* unaokwenda kuanza mwezi wa Aprili, 2024.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Temeke tunamshukuru sana Rais na wasaidizi wake wote, Mungu Ibariki Tanzania Kazi Iendelee.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila jambo, pia aniwezeshe kutoa mchango wangu kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe pamoja na kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge letu tukufu, hakika wewe ni Spika wa viwango, Mwengezi Mungu azidi kukumulikia mwanga wa mafanikio, wewe ni hazina kubwa ya nchi yetu. Hakika Mungu amekuibua kwa sababu, kwani Taifa linahitaji mtu kama wewe wakati huu. Pia nampongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna wanavyoliongoza Bunge letu tukufu.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea, nachukua fursa hii kwa dhati ya nafsi yangu kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia nampongeza kwa namna ambavyo anaiendesha nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa anavyotuongoza. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake na moyo wake wa kuwatumikia wananchi. Nampongeza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba - Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na viongozi wote wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi kwenye hoja hii ya Bajeti Kuu ya Serikali. Naipongeza Serikali kwa bajeti nzuri ambayo inatoa faraja na matumaini mema kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea nauelekeza mchango wangu kwenye madawati ya jinsia; naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuweka madawati ya jinsia nchini. Madawati haya lengo lake kubwa ni kuwasogezea huduma karibu wananchi wanaopata changamoto za kifamilia zikiwemo, udhalilishaji, ubakaji, ukatili, utelekezaji wa watoto pamoja na wanaokinzana na sheria.

Mheshimiwa Spika, madawati haya kama yalivyoundwa ipo haja ya kuyafanya yaweze kufanyakazi kama ikivyokusudiwa, kwani kinyume chake itakuwa ni kuzidisha changamoto badala ya kupunguza. Baadhi ya madawati haya yanakabiliwa na ukosefu wa vitendea kazi kama vile usafiri, kompyuta, karatasi, vifaa kwa ajili ya kuchezea na kutuliza akili za watoto wakati wa kuhojiwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa vitendea kazi hivyo vinachelewesha au kukwamisha kushughulikia mashauri yanayopelekwa na kupelekea wananchi kuona hakuna haja ya kwenda kwenye dawati, pia hupelekea wananchi kuchoka wakati mwingine wanakosa hata nauli pale inapotokea kuitwa mara nyingi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuweka mkakati maalum wa kuyawezesha madawati haya kwani ni mkombozi wa wananchi wanyonge wanaopata unyanyasaji hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa inayofanya, pamoja na kazi kubwa inayofanywa wapo watu wanambeza na kumsema vibaya Rais wetu, hii sio sawa kabisa hasa kutumia ukabila, udini au anakotoka. Rais wetu hana ubaguzi kwa nini yeye abaguliwe. Naiomba sana Serikali kutunga sheria ya kumlinda Rais dhidi ya watakaomsema vibaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda nimeshindwa kusema mengine ambayo nilitamani niyaseme katika mchango wangu katika bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maliasili na Utalii bado kuna tatizo la mpaka kati ya *ANAPA* na Kitongoji cha Momela na eneo lenye mgogoro lilikuwa sehemu ya mashamba Na. 40 na 41 na ukubwa wake ni ekari 604. Walikuja kwangu akina mama kutoka eneo husika wakilia na kulalamika wameolewa na kuishi eneo hilo kwa takribani miaka wamezaa na watoto wao kuolewa na sasa wanaambiwa wahame bila kuelekezwa waende wapi na Meru hakuna tena ardhi iliyo wazi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Rais kwa huruma yake kama mama aruhusu wananchi wale waendelee kuishi kwenye makazi yao hata kama ni kwa masharti ya kihifadhi kama *WMA*.

Pili ni kuhusu Ujenzi na Uchukuzi; ahadi za Rais; Arumeru Mashariki tuna ahadi kadhaa za viongozi wakuu ambazo hazijafanyiwa kazi; kwanza barabara ya Kingori kuanzia Malula Kibaoni hadi Ngarenanyuki kujengwa kwa kiwango cha lami ni moja ya ahadi alizotoa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyoitoa mwezi Oktoba, 2020 pale Usa River mbele ya maelfu ya wananchi wa Arumeru. Nakumbuka Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan - Rais wa Awamu ya Sita katika hotuba yake kwa Baraza lake la Kwanza la Mawaziri aliahidi kutekeleza yote yaliyokuwa kwenye mipango ya mtangulizi wake aliyerehemika akiwa kazini ikiwa ni pamoja na ahadi zote alizotoa kwa Watanzania, naomba tamko la Serikali kuhusu ahadi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Rais; naomba kwanza nianze kwa kumpogeza sana

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia uchumi wa Tanzania.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na maarifa ambapo leo Waheshimiwa Wabunge ni zaidi ya miezi mitatu tuko hapa kujadili na kuamua bajeti iliyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge na timu yake kwa namna mlivyotuongoza vyema katika kipindi chote cha kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali, pia nashukuru upande wa Serikali wakiongozwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa namna walivyojibu maswali na kutolea ufafanuzi wa hoja zetu hapa Bungeni, asanteni sana.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuvipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambavyo ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Usalama wa Taifa kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda amani na usalama wa nchi yetu, kulinda mipaka, kulinda raia na mali zao kazi ambayo inafanywa na vyombo vyetu usiku na mchana kwa uzalendo na kwa kujitoa kwa kiwango cha juu na kuifanya nchi yetu iendelee kuwa kisiwa cha amani.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru na kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoingoza Serikali na kuhakikisha maendeleo kwa Watanzania yanapatikana ambapo tumeshuhudia miradi mingi ikikamilika na mingine mingi ikiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwemo miradi ya Ikulu ya Chamwino, ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba, bomba la mafuta kutoka Uganda, Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, reli ya *SGR,* mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia wa *LNG,* Daraja la Tanzanite, Daraja la JPM-Kigongo Busisi, ujenzi wa meli ya Mv Mwanza - Hapa Kazi Tu, ujenzi uwanja wa ndege wa Kimataifa Msalato, ununuzi wa ndege mpya ya mizigo na miradi mingine ya elimu, afya, maji, barabara pamoja na kuanzishwa kwa Tume ya Taifa Mipango na

kadhalika haya sio mambo madogo kama Taifa tuna kila sababu ya kujivunia.

Pia niwapongeze Watanzania wote wakiwemo wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisesa kwa namna mnavyojitoa kwa hali na mali kulijenga Taifa letu katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nimepitia Mpango wa Maendeleo, Hali ya Uchumi na hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2023/2024, pia nimepitia Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; kwa ujumla hotuba hizi zimetoa takwimu na taarifa muhimu kutuwezesha Wabunge kutoa michango yetu. Aidha, nampongeza Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamad Hamis Chande, Katibu Mkuu na timu yote ya watumishi wa Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake za *BOT, TRA, NBS* na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG), PPRA* na kadhalika, pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kazi nzuri mliyofanya.

Mheshimiwa Spika, mambo ya kiujumla; baadhi ya ibara katika hotuba ya Waziri wa Fedha zinahitaji ufafanuzi wa kina au kuondolewa kabisa kwenye hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa kuwa zinakwenda kinyume na Kanuni za Bunge pamoja na Sheria za nchi. Naomba kupitia mambo ya kiujumla katika vipengele vinne kama ifuatavyo:-

(i) Naunga mkono pendekezo la Kamati ya Bajeti la kutoa muda wa kutosha kuwasilisha na kujadiliwa Muswada wa Sheria ya Fedha *(Finance Bill)* walau mwezi mmoja badala ya siku saba ilivyo sasa ili kutoa nafasi ya kutosha kwa wadau na Waheshimiwa Wabunge kupitia kwa makini kabla ya kuupitisha.

(ii) Kamati ya Bajeti kutokuwasilisha bango kitita linalooonesha hoja 17 zilizoibuliwa katika Kamati za Kisekta na majadiliano Bungeni, bango kitita hilo lingeeleza hoja, majibu ya Serikali na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti badala ya maelezo waliyoyatoa na Kamati kuwa walikubaliana na Serikali bila

kueleza walikubaliana nini na kulifanya Bunge lisielewe hoja zake zimeshughulikiwaje.

(iii) Waziri wa Fedha, kutumia vibaya jina la Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa dhihaka kinyume na Kanuni za Bunge kwa kumsingizia kuwa alianza Urais mwaka 2008, huku ni kutumia vibaya jina la Mheshimiwa Rais. Kauli hii inatolewa kwenye hotuba ya Serikali Ibara ya 9 ukurasa wa tano wa hotuba ya Waziri wa Fedha huku akijua fika kuwa wakati huo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa wakati huo mwaka 2008 alikuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, imekuwaje Waziri aweke taarifa ya aina hii? Naomba kunukuu; "Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilianza mchakato wa kufanyiwa tathmini ya uwezo wa kukopa na kulipa madeni *(sovereign credit rating)* mwaka 2008 ambapo zoezi hilo halikukamilika kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mdororo wa uchumi pamoja na kuyumba kwa soko la fedha duniani" mwisho wa kunukuu.

(iv) Kupiga marufuku ufungaji wa biashara kwa sababu zozote zile Waziri wa Fedha katika Ibara ya 126 ya hotuba anapendekeza kutofunga biashara kwa sababu zozote zile kuanzia tarehe 1 Julai, 2023 huku akijua kuwa kufunga biashara ni sehemu ya takwa la kisheria inapobidi kufanya hivyo, mfano mgodi au kiwanda kinapokutwa kinatiririsha maji machafu na yenye kemikali za sumu kwenda kwenye makazi ya wananchi na kwenye vyanzo vya maji na kuhatarisha maisha ya watu na viumbe hai wengine.

Je, mamlaka za udhibiti zifanye nini, ziache watu wafe ili kulinda biashara? Mfanyabishara anakutwa hana vibali, hana leseni, hana nyaraka yoyote, anauza bidhaa *fake*/bandia na zilizokwisha muda wa matumizi zenye athari za kiuchumi na kiafya kwa binadamu na viumbe hai wengine, ashtakiwe yeye halafu bidhaa zake ziendelee kuuzwa kwa wananchi? Hata wafanyabishara wa dawa za kulevya, fedha haramu na biashara haramu zingine nao waachwe waendelee na biashara zao wasifungiwe?

Kauli hii ya Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba inaleta mkanganyiko mkubwa wa kisheria na mifumo ya udhibiti nchini, lakini pia inarudisha nyuma jitihada za Serikali zinazofanywa na Mamlaka za Udhibiti katika kusimamia ustawi wa Taifa na wananchi kwa upande mwingine wataelewa kwamba Serikali imekuwa ikiwaonea.

Aidha, ifahamike kuwa ada na tozo zinazotozwa na mamlaka za udhibiti zipo kwa mujibu wa sheria na zilikubalika kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha hivyo sio sahihi kusema kwamba usimamizi wao makini unasukumwa na kuongeza mapato ya taasisi husika. Lakini pia ni muhimu kuthamini kazi nzuri inayofanywa na mamlaka zetu za udhibiti katika kulinda biashara, usalama wa afya za walaji na uchumi wa nchi, taasisi kama *TBS, NEMC, TMDA, TPRI, OSHA,* Polisi, *TRA, DCEA, LATRA, EWURA, BOT, TCRA, eGA, TCAA, FIU, WMA, NACTVET, FCC, BRELA, PPRA* na kadhalika zinapaswa kupongeza kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, Waziri alipaswa kulieleza Bunge hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji nchini *(blueprint),* lakini pia Waziri angeeleza hatua zilizochukuliwa dhidi ya watumishi wachache wasio waaminifu ambao wamekuwa wakikiuka sheria na taratibu na kujihusisha na vitendo vya rushwa na kuwanyanyasa wafanyabishara badala ya kuzituhumu kiujumla taasisi za udhibiti ambazo zimekuwa zikifanya kazi nzuri kwa mujibu wa sheria na kwa ustawi wa Taifa letu.

Kuhusu ukusanyaji wa mapato ya Serikali; mapato ya kodi, yasiyo ya kikodi na ya halmashauri yamekuwa yakiongezeka kila mwaka lakini ongezeko hilo haliendani na kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Wastani wa pato la Taifa kwa makusanyo ya kodi kwa mwaka 2022 ilikuwa ni asilimia 12.3; uwiano huu ni chini ya uwiano kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ambao ni asilimia 15. Zipo changamoto nyingi zinazotufanya tushindwe kukusanya kodi stahiki.

(i) Malimbikizo ya kodi yenye mapingamizi Mahakamani taarifa ya *TRAB* na *TRAT* kuishia Aprili, 2023 inaonesha kuwa mashauri 1,155 ya rufani za kodi yenye thamani ya shilingi trilioni

7.35 yalipokelewa na kusajiliwa katika Mahakama za Rufani za Kodi za *TRAB* na *TRAT* ambapo mashauri 423 yenye thamani ya shilingi bilioni 849.8 yaliamuliwa sawa na 11.5% ya mashauri yote. *TRA* ilishinda mashauri 344 yenye thamani ya shilingi bilioni 824 sawa na 81% na walipakodi walishinda mashauri 79 yenye thamani ya shilingi bilioni 25.7 sawa na 19%. Mtiririko unaonesha kuwa nafasi ya kushinda kesi kwa *TRA* ni wastani wa 81%, hii ina maanisha kuwa endapo kesi zote zingesikilizwa kwa wakati *TRA* ingekusanya takribani shilingi trilioni sita kwa kipindi husika na kuongeza mapato ya Serikali. Hapa unaona kuwa mapato mengi ya Serikali yameshikiliwa katika mapingamizi ya kikodi bila sababu za msingi.

Je, nini kinachoifanya Serikali ishindwe kuweka mikakati ya kuzifanya Mahakama za *TRAB* na *TRAT* kuamua mashauri haya kwa wakati? Tunaacha kukusanya mapato haya ya wazi na badala yake tunakimbilia kuweka tozo na kodi kwa kuwakamua watu maskini. Nashauri iundwe Tume ya Bunge ili kubaini ukweli uliojificha na kuwezesha kukusanya mapato ya Serikali pamoja na kuondoa usumbufu ambao wafanyabishara wanaupata kwa kukaa na kesi muda mrefu.

(ii) Utakasishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi; taarifa ya Waziri inaeleza kuwa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu *(FIU)* kuishia Aprili, 2023 kimeripoti ongezeko kubwa la taarifa shuku, kutoka taarifa shuku za fedha taslimu na usafirishaji kwa njia ya kielektroniki 724; Aprili 2021 taarifa shuku 12,651 zenye thamani ya shilingi trilioni 122.85; Aprili, 2022 hadi kufikia taarifa shuku 16,035 zenye thamani ya shilingi trilioni 280; Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 130. Aidha, Kitengo kimechambua miamala shuku 769 na kuandaa taarifa fiche 314 sawa na asilimia 40 ya miamala shuku iliyofanyiwa kazi na kuwasilisha kwenye taasisi za utekelezaji wa sheria kwa hatua za uchunguzi Aprili, 2023.

Mheshimiwa Spika, ni vigumu kwa Serikali kukusanya mapato stahiki katika mazingira ya namna hii ambapo taarifa shuku za fedha taslimu na usafirishaji wa fedha kwa njia ya kielektoniki zimeongezeka na kufikia trilioni 280 sawa na asilimia 130, hii inatupa ishara kuwa kuna ukwepaji mkubwa wa kodi

unaofadhiliwa na mbinu mbalimbali ikiwemo biashara za magendo, wizi, rushwa, ufisadi, utoroshaji wa fedha na rasilimali nje ya nchi *(Illicit Financial Flows), Transfer Pricing,* uhamishaji wa mitaji *(Capital Flight)* na kadhalika. Hapa kuna maswali mengi ya kujiuliza:-

a) Kwa nini *FIU* ifanye uchambuzi wa miamala shuku 769 tu kati ya miamala shuku 16,035 ambayo ni asilimia tano tu ya miamala yote kwa mwaka mzima?

b) Serikali inachukua hatua gani za dharura kushughulikia taarifa shuku za utakasishaji wa fedha haramu zilizofikia shilingi trilioni 280 ili kuzuia ukwepaji mkubwa wa kodi na utoroshaji wa fedha nje ya nchi unaondelea nchini.

c) Ni fedha kiasi gani zilizoshikiliwa na *FIU* kutokana na taarifa shuku za fedha taslimu na usafirishaji kwa njia ya kielektoniki hadi sasa?

d) Kwa nini *FIU* isiwe mamlaka kamili badala ya kuwa kitengo chini ya Wizara ya Fedha kama ilivyo sasa? Pamoja na taarifa hizi za *FIU* kutishia uchumi, mapato ya Serikali na usalama wa nchi yetu, lakini hakuna mkakati madhubuti uliowekwa na Serikali kupambana na matukio haya ya uhalifu, leo tunazungumzia taarifa shuku 16,035 zenye thamani ya shilingi trilioni 280 lakini zilizofanyiwa uchambuzi ni taarifa shuku 769 tu sawa na asilimia tano kwa mwaka mzima. Hivi sasa nchi yetu inatekeleza Mpango Kazi wa Kikosi Kazi cha Kifedha cha Kimataifa *(Financial Action Task Force – FATF),* matukio ya utakasishaji fedha haramu yanazidi kuongezeka kila mwaka licha ya mikakati na hatua zilizochukuliwa na Serikali kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 18 ya hotuba ya Waziri. Lakini pia sijaona mkakati wa uwezeshaji, uratibu na kufanya kazi kwa pamoja kwa taasisi zinazosimamia utekelezaji wa sheria katika hatua ya kukamata, kuchunguza na kuendesha mashtaka kwa mamlaka zinazohusika za *FIU, DCI, PCCB, DCEA* na *DPP*.

(iii) Biashara za magendo na utoroshaji wa rasilimali za Taifa nje ya nchi; tumeshuhudia matukio mengi ya kushamiri kwa

biashara za magendo ambapo bidhaa nyingi za magendo zinaingia nchini lakini pia kuna utoroshaji mkubwa wa rasilimali kama madini, nyara za Serikali, mazao ya misitu, mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi hali ambayo inaathiri kwa kiwango kikubwa uchumi, ukusanyaji wa mapato ya Serikali, mfumuko wa bei na ugumu wa maisha. Magendo haya yameshamiri katika maeneo ya mipakani na kwenye bandari bubu zinazofikia 693. Licha ya Serikali kupoteza mapato mengi katika hili eneo hakuna mifumo madhubuti ya udhibiti iliyowekwa na kulifanya tatizo hili kuwa sugu. Tunao vijana waliohitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na wengine wakiendelea kujitolea katika Kambi zetu JKT na Jeshi la Akiba (mgambo) waliandaliwa uzalendo na moyo wa kujituma tuwatumie kudhibiti maeneo yote tete na kuongeza mapato ya Serikali.

(iv) Mifumo ya TEHAMA; Taarifa ya Wizara ya Fedha imeonesha kuwa kuna kasi ndogo ya ujengaji na maboresho ya mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali ikilinganishwa na kasi ya mabadiliko ya TEHAMA duniani na hivyo kuhatarisha ufanisi na usalama wa mifumo ya usimamizi wa fedha za umma. Kifungu cha 24(1) na (2) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019 *(e-Government Act No. 10 of 2019)* inazitaka taasisi za umma kutekeleza miradi ya TEHAMA kwa namna ambayo itahakikisha manufaa yanayotarajiwa kupatikana na hatari zinapunguzwa kwa kuzingatia viwango na miongozo ya kitalaamu kama ilivyoagizwa na mamlaka. Aidha, hairuhusiwi kuanzisha na kutumia mifumo ya TEHAMA bila kupata kibali *(clearance)* cha Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA)*.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mifumo ya TEHAMA yamesaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi ya Serikali kwa kiwango kikubwa, baadhi ya mifumo hiyo ni *GePG, GIMIS, TTMS, TANCIS, ITAX, EFDMS, TAUSI, HCMIS, TANePS, MUSE, LUKU* na kadhalika ingawa pia zipo changamoto zinazopunguza ufanisi kama ifuatavyo:-

(i) Miundombinu ya mifumo ya TEHAMA kuhujumiwa; baadhi ya watendaji wa Serikali kwa maslahi binafsi wamekuwa wakiharibu miundombinu ya TEHAMA ili kuficha ukweli unaowekwa wazi na mifumo katika kuzuia wizi na ubadhirifu wa

fedha za umma. Mfano kuzima *scanner* bandarini, mifumo kutosomana, mtandao uko chini na kadhalika.

(ii) Baadhi ya Wizara na Taasisi za Umma zimeanzisha na kutumia mifumo ya TEHAMA bila kibali cha *eGA* mfano Wizara ya Kilimo (Mfumo wa Mbolea ya Ruzuku) na *TANESCO* (Mfumo wa Mipango wa Rasilimali za Biashara – *ERP)* na kadhalika.

(iii) Kukosekana kwa uunganishwaji wa mawasiliano *(connectivity)* kutokana na baadhi ya maeneo hawajafikiwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, minara ya simu na umeme hivyo mifumo kutofanya kazi.

(iv) Kutokuzingatia viwango na miongozo iliyowekwa na *eGA,* kukosekana ushirikiano wa kitaasisi na baadhi ya taasisi kuamini zaidi wataalamu na mifumo ya kutoka nje ya nchi kupata suluhisho la changamoto za mifumo yao.

(v) Baadhi ya taasisi za Serikali kutokuwa na watalaamu wabobezi wa mifumo ya TEHAMA na hivyo kupelekea ufanisi mdogo wa mifumo na kadhalika. Serikali itatue changamoto zinazokabili ufanisi wa mifumo ya TEHAMA na kuwekeza kikamilifu katika wataalamu wabobezi wa TEHAMA, pamoja na changamoto nilizozitaja nchi yetu ya Tanzania imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazopiga hatua kubwa katika matumizi ya TEHAMA kwa kushika nafasi ya 26 kidunia na ya pili Barani Afrika baada ya Mauritius kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia *(WB)* mwaka 2022 kuhusu ukomavu wa matumizi ya teknolojia duniani katika utoaji wa huduma za Serikali na ushirikishwaji wa wananchi *(GovTech Maturity Index)*.

(vi) Kushindwa kukusanya mapato kwa mujibu wa mikataba na sheria; baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali zimeshindwa kukusanya mapato yatokanayo na faini, tozo na *CSR* katika utekelezaji wa mikataba na zingine zimeshindwa kukusanya malipo baada ya kushinda mashauri mahakamani. Mfano Wizara ya Nishati na *TANESCO* kushindwa kukusanya faini shilingi bilioni 655 na *CSR* shilingi bilioni 270 kutoka Kampuni ya *Arab Contractors* na malipo kutoka Kampuni ya *IPTL* kiasi cha shilingi bilioni 342 ambapo jumla ni kiasi cha shilingi trilioni 1.268,

Wizara ya Katiba na Sheria na *DPP* kushindwa kukusanya shilingi bilioni 170 kutokana na malipo ya kesi za *plea bargain.* Kwa mifano hii michache hatujakusanya jumla ya shilingi trilioni 1.438 bila sababu za msingi, tulimsikia Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Makamba eti kutokukusanya fedha hizo za umma alitumia hekima na busara, hizo hekima na busara tunazipimaje katika fedha za umma ambazo ziko kisheria na kwa mujibu wa mkataba. Mawaziri wetu wanageuka kuwa mawakili wa makampuni halafu leo tunaenda kuweka tozo ya ushuru wa barabara na mafuta ya shilingi 100 kwa mafuta ya petroli na dizeli ili zitumike kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambapo itaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 381.8, tozo hii inakwenda kuwakamua wananchi masikini, inafikirisha sana, hapa nasema bila kumung'unya maneno Serikali haiwatendei haki wananchi katika hii tozo.

(vi) Malimbikizo ya kodi yasiyo na kesi mahakamani; malimbikizo ya kodi yasiyo na kesi mahakamani yalifikia kiasi cha shilingi trilioni 7.54 mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo ilionesha uwezo mdogo wa 10% wa *TRA* kukusanya mapato hayo. Taarifa ya Waziri wa Fedha haijaonesha malimbikizo ya kodi yasiyo na kesi mahakamani yalifikia kiasi gani mwaka wa fedha 2021/2022. Kama *assessment* ya kodi ilifanyika na hakuna mapingamizi nini kilichowafanya *TRA* washindwe kukusanya mapato hayo? Eneo hili hata tungeweza kukusanya 50% tu tungepata kiasi cha shilingi trilioni 3.77. Nashauri iundwe Tume ya Bunge ili kubaini ukweli uliojificha na kuwezesha kukusanya mapato ya Serikali.

(vii) Malimbikizo ya Kodi za Madini (Makinikia) mwaka wa fedha 2020/2021 inaonesha miongoni mwa kesi za rufani zilizoisha ni kesi 45 zenye thamani shilingi 5,594,675,387,242.40 ambazo zipo katika mazungumzo kati ya Serikali na kampuni za madini ambayo ni *North Mara Gold Mine, Pangea Minerals Limited, Bulyanhulu Gold Mine* na *ABG Exploration.* Kati ya kesi hizo jumla ya deni la shilingi trilioni 343.5 lilirejeshwa kusikilizwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Hotuba ya Waziri wa Fedha haijaeleza hitimisho ya suala hili la malimbikizo ya kodi ya kiasi cha shilingi trilioni 5.594 ambapo Mamlaka za Rufani za Kodi za *TRAB* na *TRAT* ziliona Serikali inastahili kulipwa madai hayo. Pamoja na maelezo ya Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba kuwa madai hayo

yalifutwa na sherehe ikafanyika Ikulu hadi leo ameshindwa kuleta uthibitisho na sababu za msingi za kufutwa kwa madai hayo. Kwa mujibu wa kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Fedha za Umma Bunge linaweza kwa Azimio la Bunge kutoa idhini kwa Waziri wa Fedha kufuta hasara na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali, madai ya kodi pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi. Bunge halijawahi kupitisha Azimio hilo. Kwa msingi huo wa kisheria bado naamini hakuna mamlaka yoyote iliyofuta madai ya kodi ya malimbikizo ya kodi za Makinikia kutoka kwa makampuni ya madini kiasi cha shilingi trilioni 5.594 na inashangaza kuona kwa nini Serikali haijakusanya mapato hayo hadi sasa.

Nashauri iundwe Tume ya Bunge ili kubaini ukweli uliojificha na kuwezesha kukusanya mapato ya Serikali.

(viii) Kuweka misamaha ya kodi kwenye kundi la watu wachache kupitia *Finance Bill* ya mwaka 2022 tuliamua kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kumpa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha mamlaka ya kusamehe kodi hizo kwa wawekezaji mahiri maalum. Kuweka misamaha ya kodi kwenye kundi la watu wachache maarufu kama wawekezaji mahiri maalum, maamuzi haya yanainyima Serikali mapato pasipo sababu za msingi, kodi za namna hii ni za kibaguzi na zinaondoa ushindani wa haki, misamaha ya kodi sio kivutio pekee cha uwekezaji, kunufaisha kundi la wachache na kuwakamua wananchi masikini kwa kuwawabebesha mzigo wa tozo na kodi kubwa kufidia mapato ya Serikali yanayopotea mfano malalamiko ya wafanyabishara kule Kariakoo na maeneo mengine nchini, Waziri atuambie tangu kuanza utaratibu huo Serikali imevutia wawekezaji wangapi na imepoteza mapato kiasi gani?

Waheshimiwa Wabunge, tuamue leo kupitia *Finance Bill* ya mwaka 2023 kufuta utaratibu huu ili kuleta usawa katika ulipaji kodi na kuokoa mapato ya Serikali yanayopotea bila sababu za msingi. Ni hatari kwa Taifa kuwa na mfumo wa kodi wa aina hii hususan katika kipindi ambacho Taifa linavutia uwekezaji na kuingia mikataba mikubwa ya rasilimali za nchi mfano miradi ya

kuchakata na kusindika gesi asilia *(LNG),* madini, gesi, mafuta, makaa ya mawe na kadhalika na kuikosesha mapato Serikali.

(ix) Kuondoa faini kwenye miamala ya *transfer pricing* kupitia *Finance Bill* ya mwaka 2021, Waziri wa Fedha alifanya marekebisho ya Kanuni Na. 15 ya Ukokotoaji wa Kodi za Kimataifa *(Transfer Pricing Regulations)* kwa kufuta kifungu kinachoweka adhabu ya asilimia 100 kwa kushindwa kutekeleza matakwa ya sheria. Lengo la hatua hii ni kuwaondolea walipakodi adhabu kubwa ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na kuvutia uwekezaji nchini. Uamuzi huo aliufanya Waziri wa Fedha huku akijua kuwa *TRA* ina uwezo mdogo wa kukagua miamala ya *transfer pricing* katika Makampuni ya Kimataifa *(MNCs)* na Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi kupitia miamala ya Kimataifa *(Transfer Pricing)* uamuzi huu unahamasisha uvunjaji wa sheria yaani makosa yafanyike halafu hatua zilisichukuliwe kwa wahusika na kuikosesha Serikali mapato bila sababu za msingi.

Bunge limuagize Waziri wa Fedha kuirejesha kanuni hii ili kudhibiti ukwepaji wa kodi unaofanywa na *MNCs.* Jitihada za Serikali za kuimarisha udhibiti na kuzuia upotevu wa mapato katika vihatarishi vilivyopo katika miamala ya uhamishaji wa bei ya mauziano ya bidhaa na huduma baina ya makampuni ya *kimataifa (transfer pricing)* hazitazaa matunda kama sheria ndani ya nchi haina meno ya kudhibiti wahalifu. Hatua kubwa iliyopigwa na Serikali kupitia *TRA* ni pamoja na kununua kanzidata ya *Orbis* kwa ajili ya kupata taarifa za kusaidia kufananisha bei za miamala ya kimataifa ili zisaidie kujenga hoja wakati wa ukaguzi unaofanywa kwenye kampuni za hapa nchini. Pia Tanzania imejiunga na Jukwaa la Kimataifa la Ubadilishaji wa Taarifa za Kikodi kwa lengo la kuhakikisha nchi yetu inajenga uwezo wa kubadilishana taarifa za kikodi na nchi nyingine na Serikali inatarajia kusaini mkataba ujulikanao kama *Multilateral Convention on Mutual Administrative Assistance in Tax Matters* ambao utaiwezesha *TRA* kupata taarifa mbalimbali kutoka katika nchi 146 duniani ambazo zitasaidia katika kuongeza ufanisi wa ukaguzi wa miamala ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika hili eneo la ukusanyaji wa mapato Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi zingine

za Serikali zinazohusika na ukusanyaji wa mapato zinapaswa kujipanga vizuri kwa kuweka programu na mikakati madhubuti ili kuweza kukusanya mapato kwa ufanisi mkubwa na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali. Wigo mdogo na ulegevu wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali unapelekea kuanzisha kodi na tozo kubwa kwa wananchi masikini, kuchochea mfumuko wa bei na ugumu wa maisha. Mfano kwa uchambuzi wangu mdogo katika vipengele tisa nilivyovitaja Serikali ingekusanya mapato ziadi ya shilingi trilioni 15. Kiasi hiki cha fedha kingewezesha kugharamia miradi yote ya kimkakati na ya maendeleo bila kuchukua mkopo kokote.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mikopo ya *ECF* na *LTP* kutoka *IMF* na *WB;* utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za mikopo katika kipindi cha miaka mitatu ambapo mkopo kutoka dirisha la *Extended Credit Facility (ECF)* kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* wa miaka mitatu wenye jumla ya shilingi trilioni 2.4 na Mkopo wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki ya Ardhi *(LTP)* kutoka Benki ya Dunia wa dola za Marekani milioni 150 sawa na shilingi bilioni 350. 65 Kamati imeeleza kuwa mikopo ya *ECF* na *LTP* kiasi cha shilingi trilioni 2.75 kimeelekezwa katika shughuli ambazo hazina manufaa ya muda mrefu. Fedha hizo zimeelekezwa katika mafunzo, ununuzi wa vifaa vya ofisi, utekelezaji wa shughuli zisizo na tija na kutokuwa na mpango wa uendelevu wa miradi pindi mkopo utakapokoma.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa nchi yetu ni kutochukua mikopo kwa ajili ya matumizi ya kawaida bali mikopo yote iwe ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, Waziri wa Fedha alipata wapi kibali cha kuchukua mikopo isiyo na tija na alifanya kwa manufaa ya nani? Katika siku za hivi karibuni deni la Serikali limekuwa likiongezeka kwa kasi kubwa mfano katika kipindi cha Aprili, 2022 hadi Aprili, 2023 deni la Serikali limeongezeka kwa shilingi trilioni 9.84 sawa na ongezeko la 14%; huu ni ukuaji mkubwa sana wa deni la Serikali. Kila tukiuliza tunajibiwa deni ni himilivu na kwamba linaongezeka kwa sababu ya kugharamia miradi ya kimkakati ya *SGR,* Bwawa la Mwalimu Nyerere, Daraja la Kigongo Busisi lakini leo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeweka wazi ukweli uliokuwa unafichwa kwa nguvu kubwa na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba amekwenda kufanya makubaliano na kukopa mikopo ya isiyo na tija ya zaidi ya shilingi trilioni 2.75, ni Waziri huyu huyu kwenye Taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 ambaye amekopa zaidi ya trilioni 1.285 nje ya bajeti na bila kibali cha Bunge, lakini pia ni Waziri huyu huyu amechukua misaada na mikopo ya nje yenye masharti nafuu ya shilingi trilioni 2.531 ambayo haikupitia Mfuko Mkuu wa Serikali kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, Bunge liitake Serikali kuwasilishwa mchanganuo wa mpango wa matumizi na mgao wa fedha hizi za mikopo ili Bunge liweze kuchukua nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, ufadhili wa miradi kupitia utaratibu wa *EPC+F*; kupitia mpango wa maendeleo, hotuba ya Waziri wa Fedha na hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ilielezwa kuwa mwaka 2022/2023 Wizara ilianza taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata makandarasi wa kujenga barabara saba kwa kiwango cha lami kwa kutumia utaratibu wa *Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F).* Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kuwa makandarasi wa miradi yote saba wamepatikana na mikataba ya kazi za ujenzi imesainiwa tarehe 16 Juni, 2023 ambapo makandarasi wanne wamepewa kazi hiyo ya barabara saba zenye urefu wa kilometa 2,035 kwa gharama ya shilingi trilioni 3.7.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kujenga barabara zenye jumla ya kilometa 2,035 maeneo mbalimbali nchini ikiwemo barabara inayopita Jimbo la Kisesa ya kutoka Karatu-Mbulu-Sibiti-Meatu-Lalago-Maswa ni jambo la kupongezwa kwani mtandao huo wa barabara utaleta tija kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo na uchumi wa nchi kwa ujumla. Hapa unazungumzia nchi kuingia mkopo wa trilioni 3.7 lakini nimepitia taarifa zote za Serikali hakuna maelezo ya kina namna miradi hii itakavyotekelezwa na makampuni yaliyopewa zabuni ya ukandarasi wa ujenzi yatakavyorejesha fedha zake na fedha hizo zitarejeshwa kwa kipindi gani.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa miongoni mwa Wabunge waliohudhuria hafla ya utiaji saini mikataba hiyo lakini hakuna

ufafanuzi wa kina uliotolewa kuhusu suala hili na kuacha maswali mengi ya kujiuliza kama ifuatavyo:-

(i) Gharama za mradi *(project costs)* huandaliwa na mfadhili na baadaye shughuli za ujenzi na manunuzi hufanywa na mfadhili mwenyewe na hivyo si rahisi kwa Serikali kujiridhisha na thamani halisi ya mradi *(value for money)* kwani mzabuni haimzuii kufanya upandishaji wa bei na gharama. Je, nafasi ya Serikali itakuwa wapi katika usimamizi wa gharama na ubora wa miradi wakati mfadhili analipa moja kwa moja kwa Makampuni yake? Kwa nini haielezwi kilometa moja ya barabara inajengwa kwa shilingi ngapi ikilinganishwa na gharama ya kilometa moja tunazojenga barabara za lami nchini hivi sasa.

(ii) Fedha hizi haziingii kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwani mfadhili analipa moja kwa moja kwenye makampuni yake ya ujenzi. Je, nafasi ya *CAG* na Bunge katika usimamizi wa miradi ya aina hii itakuwaje? Na kuna hatari miradi hii ikatumika kama uchochoro wa ubadhirifu wa fedha za umma, mfano fedha trilioni 3.7 hazimo kwenye bajeti ya Wizara - sekta ya ujenzi Fungu la 98.

(iii) Tulishaweka ukomo wa mikopo katika bajeti ya Serikali mwaka 2023/2024 hizi fedha za *EPC+F* ziko kwenye fungu gani? Hii inaweza kuwa njia ya kutanua goli la kuchukua mikopo nje ya utaratibu maalum uliowekwa kisheria ambao unaweza kulipelekea Taifa letu kutumbukia kwenye mzigo mkubwa wa madeni yasiyolipika.

(iv) Hapa ulinzi wa ajira za Watanzania uko wapi? Kazi zote zitafanywa na mfadhili ku-*design* mradi, ununuzi wa vifaa vya ujenzi, kuajiri makandarasi na kadhalika. Miradi ya aina hii inavunja mnyororo wa thamani na ni hatari kwa Taifa ambalo lina vijana wengi wanaohitimu katika vyuo mbalimbali wakiwa na tatizo kubwa la ajira. Mwisho wa siku huu ni mkopo ambao kama Taifa tutalazimika kuulipa na hivyo ni lazima tujue ukweli wa masharti ya mikataba hii na Serikali iache kuweka siri katika jambo hili na iweke wazi faida itakayopatikana ya mradi huu ikilinganishwa na mikopo ya kawaida, huko nyuma tumekuwa tukikataa mikopo ya utaratibu wa *EPC+F* kutokana na masharti magumu na yasiyozingatia maslahi ya Taifa. Serikali ilete maelezo

ya kina juu ya miradi hii ikibainisha masharti yote ya mikataba na mchanganuo wa gharama kwa kila mradi na muda wa kukamilisha miradi ili Bunge lichukue nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi *(PPP)*; nimesoma mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024 na hotuba za Mawaziri kuhusu maeneo ya miradi itakayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia na sekta za umma na sekta binafsi *(PPP)* baadhi ya miradi hiyo ni kama ifuatavyo; kuanza ujenzi wa barabara ya Kibaha – Chalinze - Morogoro hadi Dodoma yenye urefu wa kilometa 461 kwa utaratibu wa *PPP* na barabara ya tozo *Mbeya Bypass* (Uyole – Sogwe kilometa 48.9).

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri kuhusu ujenzi wa barabara kwa kutumia utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi *(Public Private Partnership - PPP),* Wizara inaendelea na manunuzi ya makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa *expressway* kutoka Kibaha – Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilometa 205. Hadi sasa kazi inayoendelea ni uchambuzi *(evaluation)* wa makandarasi watano walioonesha nia *(expression of interest)* ya kutekeleza mradi huu kwa sehemu ya kutoka Kibaha – Chalinze yenye urefu wa kilometa 78.9. Kwa sehemu ya Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilometa 126.1, Mshauri Elekezi anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu. Utaratibu wa *PPP* ni mzuri katika kuunga mkono jitihada za Serikali katika ujenzi wa barabara kwa kuwa mara nyingi huwa kuna njia mbadala *(alternative roads/competing roads)* ambayo sio ya kulipia, lakini hapa nina wasiwasi mkubwa juu ya masharti ya mkataba utakaoingiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inajenga reli ya *SGR* kutoka Dar es Salaam - Dodoma hadi Mwanza ili kurahisisha usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo na pia kupunguza msongamano wa magari katika barabara hiyo lakini pia kuwepo kwa barabara shindani isiyo ya kulipia. Hii inanipa mashaka na maswali mengi kama ifuatavyo:-

(i) Barabara hii inakwenda kujengwa wapi kwenye eneo la hifadhi ya barabara iliyopo sasa *(road reserves)* au itakwenda kununua maeneo yake mengine mapya kwa ajili ya ujenzi wa

barabara hiyo? Hapa tunaambiwa mchakato wa manunuzi uko hatua za mwisho, lakini mambo muhimu yanayohusu ardhi za wananchi hayawekwi wazi kwenye taarifa zote za Serikali kuhusu mradi huu.

(ii) Je, mkataba unaoingiwa hauzuii ukarabati, maendelezo au upanuzi wa barabara iliyopo? Kwani mara nyingi mikataba ya aina hii imekuwa ikiweka mazuio, hatuwezi leo kufanya maamuzi makubwa kiasi hiki ya kuzuia uendelezaji wa barabara zetu kwa manufaa makubwa ya kiuchumi ya wananchi na Taifa letu kwa ajili ya kumnufaisha mwekezaji.

(iii) Nani atakayekuwa mwamuzi wa gharama za matumizi ya barabara hizo Serikali au mwekezaji? Mikataba ya *PPP* ya aina hii hupelekea barabara za bure zinazotumiwa na wananchi kutelekezwa na pengine eneo ambalo lingetumika kufanya upanuzi kuchukuliwa na wawekezaji na hivyo kupelekea ulazima wa kila mmoja kupita kwenye barabara ya kulipia hali itakayosababisha ugumu wa maisha, gharama kubwa za usafiri na usafirishaji, *double taxation* na anguko kubwa la uchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali wakati wa kuhitimisha hoja yake ilete maelezo ya kina juu ya masharti ya mikataba ya *PPP* ya ujenzi wa barabara, usiri mkubwa ulioko sasa utatuletea matatizo makubwa, upanuzi wa barabara za njia nane Kibaha hadi Kimara umepunguza kwa kiasi kikubwa foleni na Serikali inaweza kuendelea na upanuzi huo polepole kupunguza msongamano uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iwasilishe Bungeni masharti yote ili yapate ridhaa ya Bunge kabla ya mkataba kusainiwa.

Kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato; kila mwaka tunaanzisha, tunafuta na kupunguza kodi, tozo na ada mbalimbali lakini Serikali imekuwa haileti tathmini ya utekelezaji wa maamuzi hayo kabla ya kupendekeza maboresho ya mwaka wa fedha unaofuata hali hii inawaweka Wabunge na wananchi kutokujua kama malengo na madhumuni ya uamuzi huo yamefikiwa. Tujiulize katika maeneo

ambayo tulipunguza kodi, tozo, ushuru na ada bei za bidhaa zilipungua? Mapato ya Serikali yaliongezeka? Hivi tujiulize haya maamuzi huwa tunayafanya kumnufaisha nani? Na kwa nini Serikali haitaki kuleta tathmini ya mabadiliko ya kodi yanayofanyika kila mwaka ili iwe msingi wa maamuzi ya mwaka unaofuata, kuna uwezekano eneo hili la mabadiliko ya kodi limeingiliwa na baadhi ya maamuzi yanafanywa kwa maslahi binafsi kwani ukipima huoni tija yake.

Mheshimiwa Spika, pia napongeza hatua ya Serikali kuondoa ada kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kupangiwa na Serikali kujiunga na vyuo vya ufundi, kuongeza kima cha usajili kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani kinachotakiwa kwa mfanyabiashara kusajiliwa kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 200, kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kufanya marekebisho katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

(i) Serikali inapendekeza kufuta adhabu ya asilimia 15 ya thamani ya bidhaa inayotozwa na Shirika la Viwango Tanzania kwa bidhaa zinazoingia nchini bila ya kuwa na Cheti cha Uthibitisho wa Ukaguzi wa Ubora *(Certificate of Conformity - CoC)*. Aidha, bidhaa hizo zisizo na Cheti cha Uthibitisho wa Ubora zitafanyiwa ukaguzi wa ubora zinapofika nchini na kulipiwa gharama za ukaguzi pekee. Nchi yetu ilianzisha mfumo wa ukaguzi wa bidhaa kabla hazijasafirishwa kuja nchini *(Pre-shipment Verification of Conformity-PVoC)* ambapo baada ya ukaguzi huo hupewa cheti cha ubora *(Certificate of Conformity-CoC),* utaratibu huu ulianzishwa ili kuhakikisha kuwa kuna ubora wa bidhaa na usalama wa afya za watumiaji, kuhifadhi mazingira na kukataa Tanzania kugeuzwa kuwa dampo la bidhaa *fake* na bandia, au zilizokwisha muda wa matumizi.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Waziri wa Fedha wa kuondoa faini ya asilimia 15 kwa bidhaa zinazoingizwa nchini bila cheti cha *CoC* inamaanisha kuwa amefuta utaratibu wa *PVoC* ambapo sehemu mbalimbali duniani *TBS* imeweka watoa huduma *(service*

*provider)*. Waziri wa Fedha amefanya utafiti wa kutosha wa kuwa na mbadala wa *PVoC* ili kuhakikisha nchi yetu haigeuzwi kuwa dampo la bidhaa zisizo na ubora, *fake*, bandia au zilizokwisha muda wa matumizi ambazo ni hatari kwa afya na maisha ya Watanzania, kuua ushindani, kuua ajira na uchumi wa Watanzania, lakini pia nchi yetu inaweza kuingia kwenye migogoro ya kimataifa kwa kushindwa kuzingatia viwango.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu ulifikiwaje na Serikali? Kitendo cha Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba kuondoa faini ya cheti cha *CoC* na kuondoa *PVoC* bila kujiridhisha na uwezo wa Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* kivifaa, kirasilimali watu na fedha ni kitendo cha usaliti kwa nchi ambacho kitalingiza Taifa kwenye matatizo makubwa ya kugeuzwa kuwa dampo la bidhaa zisizo na ubora. Pendekezo hili lisikubaliwe na Bunge, lakini itafutwe namna bora itakayorahisha na kuondoa kero wanazopata wafanyabiashara kwa sasa kupitia utaratibu huu.

(ii) Waziri wa Fedha anapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220 kwa kuongeza Ushuru wa Barabara na Mafuta kwa kiasi cha shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli ambayo itaiwezesha Serikali kukusanya shilingi bilioni 381.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, bei za nishati ya mafuta bado ziko juu sana nchini na tozo nyingi zimewekwa na Serikali, pendekezo hili linakwenda kuongeza gharama za usafiri na usafirishaji, kupanda kwa bei za bidhaa na kuchochea mfumuko wa bei na ugumu wa maisha kwa wananchi masikini. Yapo maeneo mengi ya kukusanya kodi na kufidia eneo hili. Pendekezo hili lisikubaliwe na Bunge.

(iii) Waziri wa Fedha kupendekeza kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 20 kwa kila kilo moja ya saruji inayotoka nje ya nchi na inayozalishwa ndani ya nchi ili kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi bilioni 147.549. Vifaa vya ujenzi ikiwemo saruji bei zake ziko juu hivyo kuweka ushuru wa bidhaa wa shilingi 20 kwa kilo ni kuongeza gharama za ujenzi kwa wananchi,

mapato haya yanaweza kufidiwa katika maeneo mengine. Pendekezo hili lisikubaliwe na Bunge.

(iv) Waziri wa Fedha anapendekeza kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotambulika kwa *HS Codes* 8702.10.99 na *HS Codes* 8702.20.99 yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa mabasi hayo ili kurahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi. Pendekezo hili linapunguza mapato ya Serikali bila sababu za msingi hivyo lisikubaliwe na Bunge.

(v) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 500 kwa kila tani moja ya ujazo *(metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho *(refined),* hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.258. Pendekezo la kushusha Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 hadi asilimia 25 linaondoa ulinzi wa viwanda na kuua bei na soko la wazalishaji wa ndani wa mazao ya mbegu ikiwemo alizeti, Bunge lisikubali pendekezo hili. Uchambuzi zaidi kwenye eneo hili utafanyika kipindi cha kuujadili na kupitisha *Finance Bill*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuadimika kwa dola za Marekani; taarifa ya Waziri na ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeeleza sababu za kuadimika kwa dola za Marekani na hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali, lakini wananchi na wafanyabishara wanalalamika juu ya kuadimika kwa dola za Marekani, kupanda kwa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni na kusababisha kushindwa kuhudumia mahitaji ya malipo ya uagizaji bidhaa nje ya nchi. Pamoja na sababu zilizotajwa lakini sababu kubwa ya kuadimika kwa dola za Marekani inalotokana na kukosekana kwa mifumo imara ya udhibiti na usimamizi hafifu wa Sera za Fedha na Bajeti *(Fiscal and Monetary Policy)* ambapo kumesababisha mahitaji na matumizi makubwa ya dola za Marekani nchini kama ifuatavyo:-

(i) Hakuna mkakati madhubuti uliowekwa na Serikali wa kuzuia uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi zinazozalishwa nchini hali inayosababisha uhitaji na matumizi ya dola pasipo na sababu za msingi. Mfano kuruhusu biashara holela ya kuuza na kuingiza mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi nje nchi. Pia bidhaa za misitu na kadhalika, ununuzi wa chanjo za mifugo nje ya nchi wakati nchi yetu ina kiwanda kinachozalisha chanjo cha *Hester Biosciences Africa Limited* na Kiwanda cha *TVI* Kibaha na kuagiza dawa za kuogesha mifugo nje ya nchi wakati ndani ya nchi tuna kiwanda cha *Farm Base Ltd.*

(ii) Serikali kuajiri wazabuni na wakandarasi kutoka nje ya nchi hata kwa miradi ambayo ingeweza kutekelezwa na Watanzania ambapo hulazimika kulipa dola za Marekani badala ya shilingi ya Tanzania. Mfano ukarabati wa Kivuko cha Mv Magogoni (shilingi bilioni 7.5), Mkataba wa *Tech Mahindra* na *TANESCO* (shilingi bilioni 70) kujenga mfumo wa TEHAMA, ujenzi wa barabara ya *bypass* huko Maswa (shilingi bilioni 12) na miradi mingine mingi ya barabara, umeme, TEHAMA, maji, madaraja na kadhalika.

(iii) Kukosekana kwa mikakati thabiti ya kudhibiti soko haramu la kubadilisha fedha za kigeni ambapo kumepelekea soko kubwa lisilo rasmi la kubadilisha fedha za kigeni nchini *(black-market)*.

(iv) Utoroshaji wa fedha nyingi za kigeni kwenda nje ya nchi na utakasishaji wa fedha haramu hali inayopelekea matumizi na mahitaji makubwa ya dola nchini. Taarifa *FIU* ya kuishia Aprili, 2023 inaonesha taarifa shuku za fedha taslimu zenye thamani ya shilingi trilioni 56.65 na usafirishaji fedha kwa njia ya kielektroniki zenye thamani ya shilingi trilioni 222.81 ikijumuisha usafirishaji wa fedha taslimu na hati za malipo kupitia mipakani. Hii ni ishara kuwa kuna ukwepaji mkubwa wa kodi na utoroshaji wa fedha nje ya nchi. Hotuba ya Waziri wa Fedha haina suluhisho juu ya changamoto hizi, ninashauri Serikali kupitia bajeti hii iimarishe mifumo ya udhibiti na uzingatiaji wa sera za fedha na bajeti ili kuimarisha hali ya uchumi na upatikanaji wa dola nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa fedha za umma; usimamizi dhaifu wa fedha za umma ni kikwazo kikubwa cha utekelezaji wa bajeti nchini, mamlaka za ukaguzi na uchunguzi za *CAG, PPRA, FIU* na *PCCB* na Mbio za Mwenge zimekuwa zikitoa taarifa za ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma hali inayoonesha kuwa hatuko vizuri katika usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za umma. Maeneo ambayo yanaripotiwa ni pamoja na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi, matumizi nje ya bajeti, ukopaji holela wa mikopo, matumizi yasiyo na vielelezo, kushindwa kukusanya mapato ya Serikali bila sababu za msingi na wizi na ubadhirifu wa fedha za umma. Mfano Wizara ya Kilimo ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 150 kwa ajili ya ununuzi wa mbolea ya ruzuku, lakini hadi kufikia Aprili, 2023 ilikuwa imetumia kiasi cha shilingi bilioni 218 zaidi ya shilingi bilioni 68 ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Lakini pia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na *TRC* kufanya manunuzi kwa kuacha bei ya ushindani na kutumia *single source* na kuisababishia hasara Serikali ya takribani shilingi trilioni nne.

Mheshimiwa Spika, licha ya matukio hayo ya ubadhirifu, wizi na ufisadi wa fedha za umma, hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa na badala yake wahusika kuendelea kuwa katika Ofisi za Serikali na wakiendelea kutumia nguvu kubwa kila leo kujisafisha mbele ya umma. Utekelezaji wa mapendekezo na maazimio ya Bunge kuhusu hoja za *CAG* nao umekuwa wa kusuasua ambapo hadi sasa taarifa ya utekelezaji ya hoja za mwaka 2020/2021 na mwaka 2021/2022 hazijawasilishwa. Mamlaka za kuchukua hatua zote zimekaa kimya juu ya ripoti ya *CAG* na zingine kurushiana mpira mfano Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba kupitia hotuba yake Ibara ya 63 anazilaumu mamlaka zingine kwa kujidogosha na kushindwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya watuhumiwa wa ubadhirifu na ufisadi wa fedha za umma. Haya ni maneno mazuri kutoka kwa Waziri kuona Mamlaka za *DCI,* TAKUKURU na *DPP* hazichukui hatua ingawa yeye binafsi akiwa mhusika mkuu hajaeleza amechukua hatua gani?

Aidha, awali wakati nikichangia Bungeni hotuba ya Waziri Mkuu nilieleza kuwa kwenye uchambuzi wangu wa ripoti ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 nilibaini ubadhirifu wa zaidi ya trilioni 30 lakini hadi leo hakuna taarifa yoyote iliyotolewa dhidi ya hatua

zilizochukuliwa kwa wahusika. Lakini pia jambo lingine la kushangaza zaidi CAG ameshindwa kutumia mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 47(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 *(The Public Audit Act)* kuwafikisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP)* watuhumiwa aliojiridhisha pasipo mashaka kuhusika na ubadhirifu na ufisadi wa fedha za umma kwa ajili ya kuwafikisha mahakamani.

Kuhusu mikataba; (i) kwa nini Serikali inaendelea kuingia mikataba ya raslimali za Taifa kwa usiri mkubwa kinyume cha Sheria ya *The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act, 2015* na Sheria ya *The Natural Wealth and permanent Sovereignty Act No. 5* ya mwaka 2017 ambazo zinataka kuweka uwazi wa masharti ya mikataba kwenye hatua za awali na kupata kibali cha Bunge. Mfano Mkataba wa *LNG,* Mkataba wa *IGA* wa Bandari na Mkataba wa Mradi wa barabara wa *PPP*.

(ii) Je, kwa nini jedwali la mikataba yenye thamani ya trilioni 91 iliyofanyiwa upekuzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali halijawasilishwa ili lisomwe pamoja na Mpango wa Maendeleo na hotuba ya Bajeti ya Serikali?

Waheshimiwa Wabunge, eneo hili tusipoliangalia vizuri Serikali inaweza kuingia kwenye mikataba ambayo hatujakubaliana, haimo kwenye bajeti wala kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano. Pia Serikali inaweza kuingia kwenye mikataba ambayo nchi haina uwezo wa kiuchumi kuihudumia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta binafsi; (i) kuimarisha sekta za uzalishaji bidhaa za kuuza nje ya nchi ambapo Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji Wanaozalisha Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi *(Export Credit Guarantee Scheme - ECGS)* na Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati *(Small and Medium Entreprises Credit Guarantee Scheme - SMECGS)* kutengewa zaidi ya shilingi bilioni 600. Hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa ingawa fedha zilizotengwa kwenye eneo husika ni kidogo na haziwezi kukidhi mahitaji, lakini pia lazima kujipanga na usimamizi wa fedha hizi ili ziwafikie walengwa na kuleta tija iliyokusudiwa, kwani uzoefu uliopo fedha za aina hii

hutumika vibaya. Mfano mabilioni ya JK, fedha za kufidia hasara iliyosababishwa na mtikisiko wa uchumi duniani *(financial crisis),* na asilimia 10 ya Halmashauri kwa ajili ya makundi maalum.

(ii) Utoaji wa mikopo, riba na dhamana katika mabenki; viwango vya riba vimepungua kwa kasi ndogo kutoka asilimia 16.31 Aprili, 2022 hadi kufikia asilimia 15.91 Aprili, 2023 hali inayopelekea gharama za biashara na uwekezaji kuendelea kuwa juu ingawa hatua zinazochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* zinatia matumaini. Niipongeze Benki ya *CRDB, NMB, TIB, TCB, AZANIA, TADB, BOA, PASS* na kadhalika kwa namna zinavyoendelea kutoa mikopo nchini na kuwezesha upatikanaji wa mitaji na fedha za uwekezaji. Serikali ichukue hatua zaidi za kushusha viwango vya riba ili kupunguza gharama za biashara na uwekezaji na ugumu wa maisha, pia kuwezesha Watanzania kupata dhamana ya mikopo mikubwa ili waweze kushiriki katika zabuni na kandarasi kubwa za barabara, umeme, maji na kadhalika.

(iii) Malimbikizo ya *VAT refunds* imekuwa ni tatizo linalolamikiwa na walipa kodi wengi nchini hali inayosababisha kuua mitaji, ajira na kudhoofisha biashara na uwekezaji nchini. Kufikia Machi, 2023 Serikali ilikuwa imelipa kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 836 hii ni hatua nzuri na ya kupongeza ingawa Waziri hajaeleza ni malimbikizo ya shilingi ngapi ya *VAT refunds* yanadaiwa na walipa kodi nchini. Nini mkakati wa Serikali kupitia bajeti hii wa kumaliza tatizo la madai ya marejesho ya kodi?

(iv) Malimbikizo ya madeni makubwa ya wakandarasi na wazabuni; eneo hili limekuwa na malalamiko ya muda mrefu hali inayosababisha kuua ajira, mitaji, kufisilika na wengine kupoteza maisha. Kufikia Aprili, 2023 Serikali ilikuwa imelipa kiasi cha shilingi trilioni 1.2 hii ni hatua nzuri ingawa Waziri hajaeleza hadi sasa Serikali inadaiwa madeni ya kiasi gani? Nini mkakati wa Serikali kupitia bajeti hii wa kumaliza tatizo hili la madeni ya muda mrefu? Kulimbikiza madeni ni kinyume cha kifungu cha 52(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pamoja na Waraka Namba 4 wa Mlipaji Mkuu wa Serikali wenye Kumb. CBA187/355/01/15 wa tarehe 31 Disemba, 2014.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya kuishia tarehe 30 Juni, 2022 inaonesha madeni ya wazabuni na wakandarasi ya muda mrefu yalifikia trilioni 3.4. Ucheleweshaji wa malipo na uhakiki wa madeni usio na mwisho umekuwa ukikera sana wananchi huku upande wa wazabuni na wakandarasi wa kutoka nje ya nchi wakilipwa kwa wakati na hata wakicheleweshewa malipo yao wanalipwa pamoja na faini. Mwaka wa fedha 2021/2022 malipo ya tozo za riba ya ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi, wazabuni, bima na mifuko ya hifadhi ya jamii bila sababu za msingi ilikuwa shilingi bilioni 418.5. Nini kinachosababisha malimbikizo ya madeni hayo wakati fedha zimeidhinishwa katika mwaka husika?

(v) Katakata ya umeme na migao isiyoisha ya umeme imekuwa kikwazo kikubwa cha biashara na uwekezaji nchini pamoja na uwekezaji mkubwa unaofanyika katika sekta ya nishati na kuongeza uzalishaji wa umeme katika Gridi ya Taifa bado tatizo la mgao wa umeme ni kubwa na linaathiri uzalishaji. Majibu yanayotolewa na Wizara ya Nishati yanakinzana na hayana ukweli, lakini pia Vituo vya Miito ya Simu *(Unified Call Centre)* kuunganishwa na kuendeshwa na kampuni binafsi umeshusha viwango vya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; bajeti iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha haitoi suluhisho la tatizo la mfumuko wa bei na ugumu wa maisha unaowakabili wananchi kwa sasa, udhibiti hafifu wa viwango vya riba na viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni. Bajeti imeshindwa kuimarisha mifumo ya usimamizi na udhibiti hali itakayopelekea kuimarika kwa biashara za magendo, biashara haramu na utoroshaji wa raslimali za taifa nje ya nchi. Bajeti haina mkakati madhubuti wa kudhibiti upotevu wa mapato na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, lakini pia bajeti hii haitoi ulinzi wa ajira za Watanzania, viwanda na wawekezaji wa ndani. Hivyo bajeti hii kama itapita kama ilivyowasilishwa pamoja na *Finance Bill* italisababishia Taifa matatizo makubwa. Bajeti hii sio *pro-poor budget.*

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema kubwa ya

kutuwezesha kuwa hapa kwa ajili ya kupigania maslahi mapana ya Taifa letu. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa maandalizi ya bajeti hii yenye maono makubwa yanayoelekea kustawisha ukuaji wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimeisoma bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri mbele ya Bunge lako tukufu na nimeona nichangie mambo machache; moja ni suala la ulipaji kodi; nchi yetu inao uwezo mkubwa wa kujiendesha kibajeti kwa kuwa ina maeneo mengi ya kukusanya kodi hususan kupitia nyanja mbalimbali za biashara, za uzalishaji, lakini jambo kubwa linalokosekana ni elimu, utayari, sheria na msukumo wa uhakika katika suala la ulipaji kodi. Ni ukweli usiopingika kuwa wananchi wengi hawana utayari wa kusimamia masuala ya kikodi hususan utoaji risiti, jambo hili linaturudisha nyuma.

Pili ni suala la makubaliano yasiyo rasmi katika ulipaji kodi, kumekuwa na tabia ya wafanyabiashara wasio waaminifu kufanya makubaliano ya kulipa kodi nje ya utaratibu na kuwanufaisha watumishi wachache wasio waaminifu wa mamlaka za mapato huku wao wakilipa kiasi kidogo cha kodi. Kupitia mwenendo huu Serikali inapoteza mapato mengi na kupelekea uhafifu wa kutekeleza malengo ya Serikali.

Tatu ni saula la mikopo kwa wazawa, kumekuwa na mwenendo wa wawekezaji au wataalam wazawa kukosa sifa za kiushindani katika masuala ya uwekezaji kutokana na kutokuwa na mitaji ya kutosha. Ni muhimu Serikali iweke sera ya kipaumbele juu ya wazawa kupatiwa mitaji kupitia mikopo inayotolewa na mabenki yetu. Kwa kuweka umuhimu wa jambo hili kundi la wanawake ni moja ya eneo ambalo Serikali inaweza kuwekeza mtaji na kuwa na uhakika wa matokeo chanya.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni sera ya uwekezaji wa viwanda vya ndani na kilimo katika mazao ya kimkakati hususan chikichi, ngano na alizeti, ni lazima Taifa letu litoke kwenye mfumo wa kutegemea bidhaa kutoka nje na badala yake tuwe wazalishaji ambao kazi yetu itakuwa kutafuta masoko ikiwa tumeshajitosheleza. Hivyo nashauri maeneo haya muhimu yapewe kipaumbele ili kuweza kujitegemea kupitia soko la ndani

na kuokoa fedha nyingi inayokwenda nje kwa ajili ya kuagiza bidhaa ikiwemo mafuta na ngano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/2024 kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha anawezesha vyema utekelezwaji wa bajeti ya Serikali. Nakupongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Katibu wa Bunge na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuendelea kufanya kazi kwa weledi mkubwa. Nampongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamad Chande na Mawaziri wote na watendaji wote wa Wizara za Serikali kwa kazi kubwa wanazozifanya katika kufanikisha malengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshmiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inayokwenda kuwagusa wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuendelea kuimarisha utendaji kazi katika utumishi wa umma ambapo imeanzisha mifumo miwili, ambapo mfumo wa kwanza ni wa usimamizi wa utendaji kazi wa utumishi wa umma *(PEPMIS)*, na mfumo wa pili ni wa usimamizi wa utendaji kazi kwa taasisi za umma *(PIPMIS)*, pia imeanzisha mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara *(HCMIS)*. Mfumo huu umeunganishwa na mifumo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba taasisi mbalimbali zinaweza kubadilishana taarifa kwa mfano imeunganishwa na *PSSF, HESLB,* Sekretarieti ya Ajira, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*, Mfumo wa Malipo ya Serikali *(MUCE)*, mfumo wa mahudhurio, mifumo ya kibenki mbalimbali ili kufuatilia mikopo ya watumishi,

*PEPMIS* na *HCMIS* lengo ni kurahisisha huduma za watumishi na pia mifumo yote inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuja na mkakati wa kulinda majanga ya kimtandao mwaka 2022, pia imekuja na mwongozo wa matumizi bora, sahihi na salama ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), naipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa sana inazozifanya na pia kati ya taasisi 522 za umma, taasisi 433 zimeweza kuunganishwa na mfumo wa kiutumishi na mishahara.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa taasisi 134 tu za umma ndiyo zimeweza kuhifadhi mifumo ya taarifa kwenye vituo vikuu vya kuhifadhi taarifa na mifumo ya Serikali *(Government Data Centers)* vyenye usalama na uhakika kwa upatikanaji wa taarifa za Serikali, hivyo tunaishauri Serikali katika bajeti ijayo ya mwaka 2023/2024 iwezeshe Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora kutenga fedha za kutosha kuwezesha taasisi zingine kuhifadhi taarifa zao kwa ajili ya usalama wa taarifa za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha uliopita yaani 2022/2023 naipongeza Serikali imeweza kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi 116,792 yenye thamani ya zaidi ya bilioni 199, imetoa vibali vya ajira mpya 7,499 na ajira mbadala 6656. Pia zaidi ya taasisi 62 zimeweza kuandaa na kuhuisha miundo na mgawanyo wa majukumu na imeidhinishwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia miundo 63 ya maendeleo ya utumishi na mishahara ya taasisi za umma imehuishwa na kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imebuni Daftari la Huduma za Serikali Tanzania *(GST)* ambao mpaka sasa hatua za usanifu wa mfumo zimefanyika na taarifa kutoka kwenye taasisi 51 zimekusanywa. Naishauri Serikali katika bajeti ijayo iwezeshe Wizara hii kukamilisha huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika nia yake ya kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi, imeanzisha vituo viwili vya huduma katika majengo ya Ofisi za Posta katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam, mwananchi akifika katika vituo hivyo

anaweza kupata huduma katika taasisi za *NIDA, RITA,* Uhamiaji, *NHIF, BRELA,* Polisi, *NSSF* na *PSSF*. Jambo hili limekuwa na matokeo chanya sana kwa wananchi, naishauri Serikali katika bajeti ijayo yam waka 2023/2024 iongezewe pesa ili vituo zaidi viweze kuongezwa katika mikoa mbalimbali ili kusogeza huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika huduma za jamii, nimekuwa nikichangia mara nyingi eneo la afya, lakini nakumbusha tena bajeti inapotengwa katika Wizara yoyote hususani ya afya tunaomba pesa ifikishwe kwa wakati kwani maradhi huwa hayasubiri, mfano bajeti inapitishwa mwezi Julai, 2023 lakini inafika kwenye hospitali husika mwezi Septemba, hii haileti tija kwa kuwa ugonjwa hausubiri. Hivyo ninashauri bajeti inapotengwa, iwe inafika kwa wakati ili iweze kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kujali suala zima la elimu ya Mtanzania kwa ujumla, kuongeza mikopo na kuendelea kugharamikia mpango wa elimu bila malipo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo naunga mkono hoja mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/2024.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa hotuba nzuri ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa na ile ya Bajeti Kuu ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, michango yangu itajikita kwenye mambo yafuatayo nikianza na migogoro ya Ushirika Mkoani Kilimanjaro; kumekuwepo na migogoro mingi inayohusisha uporaji wa mashamba au matumizi mabaya ya mashamba yanayomilikiwa na vyama vingi vya ushirika mkoani Kilimanjaro. Mengi ya mashamba haya ni yale yaliyotaifishwa na Serikali kufuatilia kuanzishwa ka Azimio la Arusha na kukabidhiwa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, migogoro hii inasababishwa na viongozi wa ushirika na imezidi kutafuna wananchi masikini hususani wakulima wa kahawa mkoani Kilimanjaro. Kwa kiasi kikubwa migogoro hii husababishwa na viongozi wa bodi za vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, utafiti niliofanya unaonesha kuwa katika Wilaya za Siha, Hai, Rombo na Moshi kuna migogoro ambayo Serikali inapaswa kuweka jicho ili kulinda mali za wakulima maskini ambao wanatapeliwa mashamba yao na wajanja wachache. Kwa mfano, katika Wilaya ya Siha upande wa *West Kilimanjaro* kuna shida kubwa na wananchi wanaishi kama wakimbizi kwa sababu ardhi imehodhiwa na watu wachache kinyume cha matakwa ya wanaushiriia wengi.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ichukue hatua ya makusudi kuyanusuru mashamba haya kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu ukataji holela wa miti ya asili na uharibifu wa vyanzo vya maji mkoani Kilimanjaro; huku mkoani Kilimanjaro katika Wilaya za Siha, Hai, Moshi na Rombo kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa kukata miti ya asili kama vile Mikufi katika maeneo ya mtoni ambako kuna vyanzo vya maji. Majangili hutumia *chainsaw* kuangamiza rasilimali za asili za Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limekuwa ni changamoto inayosababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na tayari limesababisha mito kukauka na kuathiri upatikanaji wa maji ya kunywa na ya kumwagilia mashamba. Ninaishauri Serikali ichukue hatua kali mapema za kulinda maeneo haya. Katika jambo hili kubwa sheria za nchi zizingatiwe ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua kali kwa wale watakaobainika kusababisha uharibifu kwa kuzishirikisha idara za misitu, mamlaka za maji na jeshi kulinda na kutunza vyanzo hivyo.

Kuhusu migogoro katika vyanzo vya maji mkoani Kilimanjaro; baadhi ya maeneo ya Jimbo la Moshi Vijijini yanakabiliwa na shida kubwa ya majisafi na salama ya kunywa. Juhudi kubwa

zimefanywa na mamlaka husika kuwapelekea wananchi maji kupitia miradi inayofadhiliwa na Serikali mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kwamba baadhi ya wananchi walio karibu na vyanzo vya maji katika maeneo ya Moshi Vijijini (Kimochi, Oldmoshi Mashariki, Kibosho Kati) wanapinga miradi hiyo isijengwe pamoja na wenzao kukabiliwa na shida kubwa ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upotoshaji mkubwa sana kuhusu umiliki wa rasilimali hizi za maji. Kuna wanaofikiria hizo rasilimali ni mali zao binafsi na si za Taifa kama sheria inavyotamka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, kumekuwepo na changamoto kwenye ujenzi wa miradi ya maji. Kwa makusudi, baadhi ya wananchi wenye nia ovu wamekuwa wa kuzuia na kuhujumu ujenzi wa miradi katika maeneo niliyotaja. Kwa mantiki hii, ninaishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu rasilimali za maji na umuhimu wa kushirikiana ili kulinda na kupeleka huduma ya maji kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazokikabili Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka; kuna changamoto zinazokikabili Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka ambazo kwa kiwango kikubwa zimeshusha hadhi yake ya kuwa Chuo cha Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto hiyo ni kupungua kwa idadi ya wanafunzi wa kigeni wanaojiunga na Chuo hicho kila mwaka. Changamoto iliyopo ni ile ya masharti magumu kwenye mfumo wetu yanayosababisha baadhi ya masomo yanayotolewa na nchi nyingine yasitambuliwe chuoni hapo kwa wanafunzi wanaotoka nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hili, ni vyema vyombo vyetu vya udhibiti na usimamizi wa elimu hapa nchini *(TCU na NACTE)* viangalie namna ya kurekebisha kanuni ili kuruhusu wanafunzi kutoka mataifa ya nje kuja na kupata elimu hapa nchini. Hii ni pamoja na kutambua sifa, vyeti na masomo

yanayotolewa na nchi nyingine katika udahili hapo chuoni Mweka.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliiweka mezani mnamo tarehe 15 Juni, 2023 ambapo niliwasilisha katika Bunge lako Tukufu Hali ya Uchumi kwa mwaka 2022, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/2024 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kwenda mbali niombe niseme neno moja. Leo nilikuwa na wageni Waheshimiwa Madiwani wenzangu kutoka Iramba, sijui kama tangazo lilifika na kama wapo wasimame kwa ruhusa yako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tafadhali huruhusiwi kusimamisha watu humu ndani. Huruhusiwi, endelea na kuhitimisha hoja yako tafadhali. Litakapokuja tangazo la wageni mimi nitawatangaza. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda kukushukuru wewe mwenyewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kuendesha mjadala huu kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu hoja mbalimbali za Wabunge, napenda kutumia fursa hii kupaza sauti tena kwamba Mama apewe maua yake kwa sababu ya kazi nzuri anazowafanyia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale ambao hawajazoea kufuatilia mambo yanavyofanyika wanaona Waheshimiwa Wabunge

wanaposimama kusifia kazi nzuri, wanafanya tu hivyo kama ni utamaduni. Hata hivyo, naomba dakika chache tu niseme baadhi ya mambo kwa ufupi.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazokwenda kwenye shughuli za maendeleo kwenye Wizara zetu, mikoa yetu, wilaya zetu, majimbo yetu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, ni kiwango kikubwa cha fedha ambacho hakijawahi kutokea tangu uhuru.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizokwenda *TARURA* kutengeneza barabara za mijini na vijijini ili wakulima waweze kupitisha mazao yao, watoto wanaokwenda shule wasisombwe na maji mvua zinaponyesha, akinamama wajawazito wasifariki njiani kwa sababu ya kukosa barabara za kuwafikisha kwenye vituo vya afya ni fedha nyingi kuliko zilizowahi kutokea tangu *TARURA* ianzishwe. Hivyo ndivyo Mama anavyowajali Watanzania na anavyowajali wananchi wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zilizokwenda kutengeneza barabara zinazosimamiwa na *TANROADS* na hivi juzi tumesaini mikataba ya barabara zile saba pamoja na ya nane ikiwa imekaribia kukamilika, ni barabara zenye urefu mkubwa kuliko barabara zilizowahi kusainiwa Afrika kwa mara moja tangu Nchi zote za Afrika zipate uhuru. Hivyo ndivyo Mama anavyowatumikia Watanzania. Mama apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zinazokwenda kwenye Elimu bila Malipo, Mikopo ya Elimu ya Juu, Miundombinu kuanzia Shule ya Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu, ni fedha nyingi ambazo zimewahi kwenda kwa mara moja katika mwaka wa fedha tangu nchi hii ipate uhuru. Hivyo ndivyo Mama anavyowajali watoto wa Watanzania maskini.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazokwenda kwenye afya, kwenye kazi za Sekta ya Afya, Miundombinu ya Sekta ya Afya, vitendea kazi kwenye Sekta ya Afya ni fedha nyingi Kwenda katika mwaka wa fedha kuliko kipindi chochote kile.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazokwenda kwenye kilimo. Fedha zinazokwenda kwenye miundombinu ya umwagiliaji, mbegu bora, maghala ya uhifadhi wa chakula, fedha zinazokwenda kwenye kuendeleza vijana katika ku–*modernize* kilimo, ni fedha nyingi zilizowahi kutolewa katika Sekta ya Kilimo kwenye mwaka wa fedha kuliko kipindi chochote tangu tupate uhuru. Hivyo hivyo, katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi na hivyo hivyo katika sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, hata fedha ambazo zimekwenda kwenye Sekta ya Maji. Usambazaji wa maji, magari ya kuchimba visima, mitambo ya kuchimba mabwawa, fedha zilizokwenda kwenye kujenga miundombinu ni fedha nyingi zilizowahi kwenda katika mwaka wa fedha kwa mara moja kuliko kipindi chochote tangu tupate uhuru. Hivyo ndivyo Mama anavyowajali Watanzania. Mama yuko kazini, Mama apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zinazokwenda kwenye utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati. Reli, Bwawa la Mwalimu Nyerere, fedha zinazokwenda kwenye kutekeleza miradi mingine kama mafao ya wastaafu, mtakumbuka mwaka 2022 tuliweka hati fungani zaidi ya trilioni mbili. Maslahi ya watumishi wa umma, kukuza sekta binafsi, kuvutia uwekezaji pamoja na uboreshaji wa vyombo vya ulinzi na usalama, ni fedha nyingi kuliko kipindi chochote katika mwaka wa fedha wowote utakaoutaja.

Mheshimiwa Spika, nimetaja tu sekta chache, lakini kuna sekta nyingine huu ndio utaratibu na hivyo ndivyo fedha zilivyokwenda. Pia, hapa ndipo Watanzania wajiulize, kuna Watanzania wengi sana ambao wamekuwa wakiwaaminisha watu wengine kana kwamba kumekuwa na wizi mwingi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, hivi fedha kama zimwekwenda nyingi hivyo kwenye miradi ya maendeleo na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kila jimbo limepata fedha nyingi kuliko kipindi chochote kile. Hivi kama wizi umeongezeka, katika kipindi ambacho wizi haukuwepo hizo fedha zilikuwa zinakwenda wapi? Kama sasa

zimekwenda nyingi kuliko kipindi chochote, katika kipindi ambacho wizi haukuwepo hizo fedha zilikuwa zinakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, Watanzania watofautishe na tusichanganye uwazi katika matumizi ya Serikali kuongezeka, ni tofauti na wizi kuongezeka. Nirudie tena kusema kwamba, haya niliyoyasema ni kwenye baadhi ya sekta tu, lakini maendeleo yametokea katika sekta nyingi na Watanzania wote ni mashahidi. Hata Yanga kufika fainali na kuchukua vikombe vyote ni hatua ya maendeleo ambayo haijawahi kufikiwa. Hata lile la mataifa walilichukua kwa sababu chanya moja na chanya moja ziko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru tena wewe pamoja na Naibu Spika wako kwa jinsi ambavyo mmendesha vikao vizuri. Vile vile, niwashukuru Wenyeviti na nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Daniel Baran pamoja na Mheshimiwa Omari Kigua ambaye ni Makamu Mwenyekiti pamoja na Kamati nzima ya Bajeti. Pia, napenda kuwashukuru Mawaziri wote ambao walitoa ufafanuzi wa hoja za kisekta siku ya Ijumaa.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa viwango kabisa na ananisaidia vema katika kutekeleza majukumu haya. Vile vile, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Natu Mwamba, Daktari Bingwa kabisa wa masuala ya uchumi pamoja na timu yote ya wataalam ambao wanasaidia katika shughuli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imeanzisha Mafungu mapya matatu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mipango, uwekezaji na ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi. Mafungu hayo ni :-

(i) Ofisi ya Rais Uwekezaji;

(ii) Tume ya Mipango; pamoja na

(iii) Kituo cha Ubia kati ya Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, hivyo, napenda kutoa taarifa kwamba bajeti za mafungu haya zimetengwa kupitia kasma ya Matumizi ya Kitaifa *(National Expense)* iliyopo Fungu 21 Hazina. Kwa muktadha huo Sheria ya Matumizi ya mwaka 2023 *(Appropriation Bill, 2023)* itajumuisha bajeti za mafungu haya baada ya Serikali kukamilisha taratibu zote.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye ufafanuzi wa mafungu nitaomba uridhie niende kwa hoja kwa sababu ya wingi wa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea kuhusu masuala ya maendeleo kwenye Majimbo yao yanayohusisha sekta zao, wameongelea kwenye maji, wameongelea kwenye elimu, wameongelea kwenye afya, wameongelea kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hoja zenu zote hizo tumezipokea na mara tutakapoenda kuna zile ambazo mmeziwasilisha kwa maana ya udharura na ulazima katika maeneo hayo. Wizara ya Fedha tutakaa na Wizara za Kisekta ili tuweze kuona utekelezaji wake tunaweza tukaufanya namna gani. Liliongelewa kwa sauti kubwa suala la Uwanja wa Ndege wa Mwanza Ndugu yetu Musukuma alilisema na bahati nzuri Uwanja wa Ndege wa Mwanza hiyo *center* wote tunaijua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge tumelipokea tutakaa na Wizara ya Kisekta taratibu za kutafuta fedha ni taratibu endelevu tutaendelea na tutaweka uzito unaostahili katika jambo hilo na Mheshimiwa Mbunge uliongelea kushika shilingi hata usishike shilingi, Uwanja wa Ndege wa Mwanza hata mimi naupenda na ni nyumbani kwetu, kwa hiyo tutakaa na Wizara za Kisekta tuweze kuangalia ili tuweze kuona namna ya kulitekeleza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili Mheshimiwa Rais alishalielekeza siku nyingi, nakumbuka alipokuwa ziara kule katika Nchi za Umoja wa Ulaya ni moja ya maeneo ambayo alikuwa anayasisitiza kila wakati sisi Wizara ya Fedha tuweze kukaa na wenzetu tuweze kuyafanyia kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, yaliongelewa masuala barabara Ndugu yangu Mheshimiwa Taletale, Mheshimiwa Mwenyekti Kihenzile, Mheshimiwa Bilakwate, Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri mwenzangu Jafo, Ndugu yangu Mheshimiwa Asenga, Ndugu yangu Mheshimiwa Kamamba tumepokea barabara zote ambazo waheshimiwa Wabunge mmeziwasilisha. Waheshimiwa Wabunge barabara zingine mlisema zimetengewa fedha kidogo, tunapoweka fedha kidogo hatuna maana kwamba katika mwaka huo tutatekeleza mradi wa barabara kwa kutumia fedha hizo, fedha zingine ni kwa ajili ya upembuzi lakini maeneo ambako upembuzi ulishafanyika kama kule Nyororo tumeweka fedha kwa sababu zoezi la kutafuta fedha ni endelevu, tunaendelea kukamilisha masuala ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuliweka fedha kwa ajili ya kushikilia kifungu ili wakati wa kutekeleza kuwe na kifungu ambacho kilipitishwa kwenye bajeti. Kwa maana, hiyo barabara zote ambazo zitatekelezwa kwa *P4R* ni kwamba fedha zitakapatikana zitaendelea kutoka kadri utekelezaji unavyoendelea. Kwa hiyo, hatuna maana kwamba tutatekeleza kwa kiasi kidogo kile ambacho kimewekwa, kile kinashikilia kifungu ili tutakapokwenda kutekeleza tuweze kutekeleza kwa kutumia kifungu ambacho kilipitishwa na kwa utaratibu wa *P4R* ambapo fedha inaendelea kutoka kufuatana na utekelezaji wa mradi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge miradi yote ile mliyoitaja ya barabara, miradi ya maji, miradi ya afya tumeipokea tutakaa na Wizara za Kisekta kama ambavyo Mawaziri wa Kisekta walizisema siku ile wakati wanahitimisha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niwapongeze Wabunge wote ambao walihimiza wananchi pamoja na viongozi kwenye suala la kulipa kodi. Suala hili la kulipa kodi ndilo linalotutambulisha kuhusu kujitegemea, ndilo linalojitambulisha kuhusu uhuru wetu, ndilo linalotutambulisha sisi kuhusu uwezo wetu wa kutekeleza miradi ya maendeleo. Mheshimiwa Bilakwate ulisema kabisa ulikpokuwa unaomba ilikuja hiyo kama ndoto na ilikuja ikakuelekeza hivyo nilimsikia Mheshimiwa Kwagilwa, Mheshimiwa Matiko, Mheshimiwa Mnzava, Mheshimiwa Subira, Mheshimiwa Riziki Mama yangu na Wabunge wote ambao mmeongelea kuhusu hamasa hii.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge, twendeni tukawaelimishe wananchi wetu, tukawahamasishe kwamba jambo la kulipa kodi ni jambo letu sisi sote, ni jambo la Watanzania, ndiyo maendeleo yetu na jambo hilo kama wananchi wote wataitikia mwito huo nchi yetu itashusha viwango vya kodi.

Mheshimiwa Spika, leo hii viwango vya kodi ni vikubwa kwa sababu wanaolipa kodi ni wachache, maana yake mzigo wa maendeleo, mzigo wa huduma za jamii unabebwa na wachache. Kwa maana hiyo twendeni tukawahamasishe na kama kila mmoja atalipa kodi, kila mmoja atatumia mashine za kilektroniki, kila mmoja atadai risiti, kila mmoja atatoa risiti, anapouza maana yake tunaianza safari ya kupunguza viwango vya kodi. Leo hii kila mfanyabiashara anaona viwango vya kodi ni vikubwa lakini hii *vicious cycle* inatakiwa kukatwa kwa kuanzia kila mmoja alipe kodi ndipo tutakapoweza kupunguza viwango hivyo vya kodi.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye hoja nyingine ambayo iliongelewa kwa kiwango kikubwa na Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni hoja ya ngano. Na nilimsikia Mheshimiwa Mbunge wa Makete akiongea kwa sauti kubwa sana pamoja na Wabunge wengine wote ambao waliongelea suala la ngano. Waliona kama vile Wizara ya Fedha imeshusha kiwango cha kutoka asilimia 35 kwenda asilimia kumi.

Mheshimiwa Spika, nikuambe kwamba jambo hili tumekaa na Wizara ya Kisekta tuko na sauti moja kwenye jambo hili, kinachotokea hiyo ni *terminology* ambayo inatumika kwenye masuala hayo ya kikodi. Kama ambavyo huwa tunafanya kwenye sukari, ile sukari ya *gap sugar* inapoagizwa, pale ambapo huwa tuna upungufu ama wazalishaji au waagizaji huwa wanapewa nafuu kwa hiyo hata hii *duty remission* ni lugha ya kitaalamu inayomaanisha kwamba wale wote ambao watanunua ngano ya ndani. Ngano ya ndani ikishaisha anapewa ruhusa ya kuagiza Ngano ya nje kwa bei iliyo nafuu.

Mheshimiwa Spika, hicho ndicho kilichofanyika hakijapunguzwa ili aagize nje aache ngano ya ndani, ila

anapewa nafuu pale atakapokuwa amenunua. Kwa hiyo, anapewa motisha ya kununua ngano ya ndani, kwa maana hiyo atakapokuwa amenunua ngano ya ndani ikaisha anapewa ruhusa ya kuagiza Ngano ya nje kwa kiwango ambacho kiko chini ya kile cha kawaida, mtu mwingine yeyote yule ambaye hanunui ngano ya ndani hanufaiki na hiyo *duty remission*. Kwa maana hiyo, hii ni motisha ambayo sisi Wizara ya Fedha pamoja na wenzetu wa Wizara ya Kilimo tuko na sauti moja na uagizaji wake utaratibiwa na Wizara ya Kisekta ya Kilimo kwamba yule ambaye amemaliza kununua ngano ndiye ambaye atapewa hiyo *duty remission* kama motisha ya wale ambao wananunua ngano ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo niwaombe mkubali hilo pendekezo liko sawa na huo ndiyo utaratibu ambao ni *standard* na ile ni lugha ya kitaalam ambayo imetumika. Hatujapunguza ili tuue wakulima wa ndani, tumepunguza kumpa motisha yule atakayenunua ngano yote ya ndani, ile iilikuwa ilitolewa kwa sababu kuna wakati watu walikuwa wanapendelea kununua ngano za nje ngano za nje, kwa hiyo, ikaleta unafuu kama motisha kwa yule ambaye atanunua ngano ya ndani, hiyo ndiyo maana ya *duty remission*

Mheshimiwa Spika, kuna Wabunge wengine waliongea kwa sauti kubwa kuhusu upande wa mafuta ya kula. Tumeliangalia jambo hili na kwa jinsi ambavyo tumeliangalia tumeenda kutoa unafuu kwa wale wazalishaji wa ndani ili mafuta ya ndani yasije yakazidiwa na yale mafuta ya nje, kwa hiyo tutaleta kwenye *schedule of amendment* nafuu ambayo tumeitoa kwa wazalishaji wa ndani kama motisha ya kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana ndani ya Serikali kwamba jambo hili tutaendelea kulifuatilia kwa ukaribu, lakini kingine ambacho ndani ya Serikali tunakubaliana tukasema tuanze nalo hilo kwa uzito mkubwa ni kudhibiti uingiaji wa mafuta kwa njia ambazo siyo rasmi, ambao ndiyo ambao unaleta hiyo *flooding* ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeiongea kwa sauti kubwa. Tumepokea nakumbuka ndugu yangu Mheshimiwa William aliongea na Mheshimiwa Kunti na wengine wote akina Mheshimiwa Musa na wengine wote wanaotokea katika maeneo

ya wakulima wa alizeti, tumeyapokea na tutakaa na wazalishaji tutakaa na vyombo kuhakikisha kwamba uingiaji wa mafuta kiholela unadhibitiwa ili kuondoa hiyo *flooding* ambayo ndiyo inaleta tatizo kubwa la bei ya mafuta ya kula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge mkubali mapendekezo hayo na Mheshimiwa Rais anawajali wakulima ndiyo maana anaweka uwekezaji mkubwa katika sekta hizo za kiliomo.

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge wengine waliongelea kuhusu kuboresha kuboresha mazingira ya kufanyia biashara, tumeyapokea ninayo orodha ndefu ya wale Wabunge ambao walisema mazingira yawe rafiki, tunaendelea na hayo ndio maana hata katika mapendekezo yetu kuna maeneo ambayo tumeyaboresha zaidi na tunaenda *full swing* kwenye utekelezaji wa *blue print. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Wabunge ambao waliongelea kuhusu Wakandarasi kulipwa, kuna walioongelea kuhusu makundi maalum, Sheria ile ya Manunuzi kutekelezwa, kuna wale walioongelea kuhusu kuwianisha mapato na matumizi. Tumeyapokea hayo na nadhani katika Bunge lijalo kama itakupendeza tunaleta Sheria ile ya Manunuzi ambayo itaangalia hivi vitu vyote, pia Serikali ya Mheshimiwa Samia iliona hilo tatizo ambalo linajitokeza kwenye upande wa riba zinazojitokeza kufatana na wakandarasi kutokulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la tatizo hilo ni pale ambapo miradi mingi inaingiwa mikataba kwa mara moja kwenda kwenye utekelezaji ambayo haioani, haiwiani na fedha ambazo zinapatikana za kulipa hiyo. Kwa hiyo, kama madai ni makubwa kuliko fedha zilizopo ni dhahiri kwamba watalipwa wachache na wengine ambao hawajalipwa watenda kwenye kudai riba. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais ameona afufue Tume ya Mipango na ijitegemee ili utekelezaji wa miradi uwiane na mipango iliyopo, kama utekelezaji wa miradi utawiana na mipango iliyopo ni dhahiri kwamba miradi inayotekelezwa itakuwa inawiana na uwezo wa Serikali wa kuilipia miradi ile na kama uwezo wa kuilipia

miradi ile utaweza kuendana na miradi inayotekelezwa ni dhahiri patakuwa hapana riba.

Mheshimiwa Spika, kinachojitokeza ni kama miradi inayotekelezwa kama *certificate* zilizoiva ni nyingi kuliko fedha zilizopo, ni dhahiri huwezi ukazilipia zote na wale ambao hawajalipwa ni dhahiri watadai riba. Kwa hiyo, hicho ni kitu ambacho Serikali imeenda kwenye utekelezaji wake lakini ndiyo maana pia Mheshimiwa Samia akaona aweke utekelezaji wa miradi ya barabara kwa *EPC+F* ambapo baada ya kukamilika kwa maridhiano ya Serikali na Benki inayotoa fedha hizo, fedha zitaanza kutolewa moja kwa moja kwenda kwenye mradi kwa hiyo hapatakuwepo na utaratibu wa fedha ambazo zilipangwa ziende kwenye mradi, kuweza kutumika labda katika maeneo mengine ambayo yanapunguza uwezo wa Serikali labda kulipa katika miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo tumekaa ndani ya Serikali tunaliangalia kwa ukaribu ni vile tuna madeni ya ambayo yalishazalishwa siku nyingi hatuwezi tukayaacha wala hatuwezi kuyakana tunaendelea kulipa mafungu kwa mafungu na tutaendelea kutoa taarifa hiyo kwenye Kamati ya Kisekta, Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengine aliyasema Mheshimiwa Mpina akiwa anapinga hatua ambazo Serikali inazichukua. Napenda kumshauri rafiki yangu jirani yangu maana Iramba na Meatu zinapakana. Si ubingwa na wala si ustaarabu kusema na kupinga kila kitu hata ambacho hakistahili kupingwa.

Mheshimiwa Spika, namuelewa sana Rais Samia anapoleta hatua hizi za kikodi namuelewa sana, mwenzangu asipokuwa anaelewa haya si mbaya pia ukimuona Mbunge mwenzako Kibunge tu ukamuuliza hili linamaana gani? kuliko aibu ya kusema jambo, unapinga jambo ambalo lina maana kubwa sana kwa mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Rais Samia anapendekeza kwamba tuache utaratibu wa kufunga biashara ama shughuli ya uzalishaji, kwa sababu shughuli ya uzalishaji mle ndani kwenye shughuli za

uzalishaji kuna watu ambao hata siyo wamiliki lakini maisha yao yanategemea hiyo shughuli ya uzalishaji. Tuache kufunga biashara kwa sababu huyo ni mtu anayeendesha biashara ni mtu ambaye ameamua kuisaidia Serikali, badala ya kukaa kutafuta ajira yeye ameamua kujiajiri na ameamua kuwatafutia ajira na Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anasema badala ya kufunga biashara, kama kuna makosa yapo tukae na yule anayetakiwa kutatua yale makosa na *penalty* imewekwa kwa mtu ambaye hatasikia taratibu za kisheria zichukue mkondo wake, lakini Mheshimiwa Mpina anaona jambo hilo halina maana anasema tuendelee kufunga biashara kwa sababu yeye kwa hulka yake anafurahia watu wakiumia.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka jinsi alivyokuwa anafanya sherehe kwa kuchoma nyavu bila kudhibiti nyavu zile kuingia, tunatambua jinsi alivyokuwa anafurahia kwenda kufunga viwanda anafika tu anakuta mchirizi hivi anasema hiki nimeshafunga mpaka mwezi ujao. Kwa nchi ambayo ina tatizo kubwa la ajira ambalo tunataka sekta binafsi ikue ili tupate kodi huo siyo utaratibu ambao mtu yeyote mwenye hekima anatakiwa kuupigia debe. Angalieni nchi ambazo zimeendelea zilizokuza sekta binafsi zinaishi vipi, ni watu ambao wana adabu kwenye sekta binafsi, watu wanaheshima kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Rais Samia anachotufundisha, anatufundisha kwamba sekta ya umma na sekta binafsi siyo maadui, hawa ni wabia wa kuendesha nchi. Hawa ni wabia siyo maadui, lazima tufanye mtu kufanya shughuli ya kujiajiri aione ni shughuli yenye heshima. Sasa hivi nchi nzima watu wanataka tu watoto wao waende kufanya kazi Serikali, kila mtu anataka watoto wake waende Serikalini na wengine wanakuwa *specific* zaidi wanataka tu watoto wao waende *TRA* kwa sababu gani? ukiwa Serikalini ndiyo shughuli pekee ambayo ina heshima, watu wote wanaheshimu hiyo peke yake, lakini Mheshimiwa Rais Samia anachotaka kutufundisha anataka kutufundisha shughuli yoyote ya uzalishaji iheshimiwe na yule anayefanya hiyo shughuli aheshimiwe, hata pale ambapo panapoonekana pana matatizo pawe na utaratibu wa kiungwana wa kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, sasa unafunga shughuli ya uzalishaji kuonesha tu ubosi unafika tu unafunga na kuondoka, umevaaa zako tai, hautambui hata kwamba hiyo tai uliyovaa pamoja na suti hiyo na mshahara unaopokea unaupokea kwa sababu ya huyo huyo uliyemfungia biashara yake. Mheshimiwa Mpina kwa uelewa wake hilo halioni kabisa, hajui kabisa kama Serikali hata Bunge tulipokaa hapa mchango wa sekta binafsi upo. Mchango wa sekta binafsi ili Bunge likae upo, hayajui haya.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono kama Waziri niliyepewa dhamana ya kusimamia uchumi, maoni haya ambayo Mheshimiwa Rais anataka kuyaweka ni maoni ya msingi yataikuza sekta binafsi yatakuza *tax base* na yataongeza ajira pamoja na hamu ya watu kujiajiri, lazima mtu ambaye hatma ya wenzake aheshimiwe na apewe jina lililojema ili aweze kuvutia na wengine waweze kujiandaa nalo kwenda na hilo wazo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tunasema tuache kukamata mizigo, tuache kushikilia mizigo na vitendeakazi vya watu. Mheshimiwa Mpina anasema na hilo ni baya tukamate tu anasema taasisi hizo zinafanya vizuri sana. Hebu niambieni Waheshimiwa Wabunge ninyi ni wawakilishi wa wananchi hebu fikiria mzigo ambao siyo mali haramu, eti tumetofautiana kodi siyo sumu, eti tumetofautiana kodi badala yake tunakaa nayo mwezi wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano, wa sita, mwaka wa kwanza, mwaka, wa pili, hebu niambieni. Je hivi tungepokea kodi ile ambayo hatubishani nayo halafu tuandikishiane ile ambayo tunatofautiana, halafu huyu mtu bidhaa yake apewe aendelee na biashara, niambieni kwa miaka mitatu ambayo tumeshikilia mzigo tungeshapokea kodi ngapi? Mheshimiwa Mpina anasema wakamatiwe tu huo utaratibu Serikali mnaotaka kuufanya ni mbaya. Ni lazima tuheshimu mitaji ya watu!

Mheshimiwa Spika, niambieni ni wafanyakazi wangapi unaweza ukashikilia mishahara yao kwa miaka miwili halafu wasilalamike ukae tu? Kwa sababu yule mwenye mtaji wake ile biashara ndiyo mshahara wake. Ili tuweze kukuza sekta binafsi kama wapo ambao hawajaelewa maoni, mawazo ya Mheshimiwa Rais kama Mheshimiwa Mpina tunawakosea sana

watoto wa Kitanzania ambao hatma yao inategemea sekta binafsi kukua.

Mheshimiwa Spika, ni lazima nchi hii na viongozi wote wa Serikalini walitambue hilo, lazima tuheshimu mitaji ya watu, huwezi ukakaa na mtaji wa mtu umeushikilia tu, wewe fikiria mtu amekopa amekopa akaenda kufuata bidhaa hiyo, bidhaa imefika wewe unaishikilia yeye amekopa ameweka rehani nyumba, nyumba inaenda kuuzwa wewe umeshikilia bidhaa yake. Umeshikilia tu kwa sababu unayomamlaka na uko ofisini na unalipwa mshahara halafu Rais anasema tuondoe huo utaratibu tutafute njia mbadala ya kushughulikia matatizo ambayo hayajakubalika, Mbunge anayelipwa kwa kodi ya sekta sinafsi anasema hili jambo siyo zuri, ninyi endeleeni kukamata tu. Sasa Mheshimiwa Mpina kwa sababu ni jirani yangu usikute yale mambo kaambiwa kule wanakoamini sana mambo yale kwambe wewe pinga kila kitu tu. Si kila kitu kinafaa kupingwa mambo mengine ni lazima tutumie *logic* ilipo.

Mheshimiwa Spika, tumeondoa pia utaratibu na tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge, Wabunge walikuwa wanasema kule kwenye Halmashauri kwa nini kila taasisi ya Serikali inakwenda yenyewe kudai? Tumeandaa *blueprint* imeeleza kwamba tukitaka kukuza sekta binafsi tuondoe ule utaratibu wa kuwafanya watu wa sekta binafsi siku nzima kusikiliza ama kuhudumia Serikalini tu. Anatoka wa *fire* anaenda wa OSHA, anatoka wa OSHA anaenda wa *TFDA,* anatoka wa *TFDA* anaenda wa *TBS*, anatoka wa *TBS* anaenda…, utitiri wa watu wote wanaotoka Serikalini. Tukasema tutengeneze dirisha moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo mifano ambayo tumefanikiwa kwenye hilo, tumeweza kufanikiwa kwenye upande wa mafuta, tunakusanya mara moja, tukishakusanya kuna fedha inaenda *REA,* kuna fedha inaenda reli, kuna fedha inaenda *TANROADS*, tuna fedha inaenda maji, tuna fedha inaenda *TARURA* lakini imekusanywa mara moja. Sio kila taasisi inaenda kukusanya maana yake na katika dunia hii ya kidijitali inawezekana. Hata zile kaguzi zilizo rasmi si vyema kila mtu anaenda kwa wakati wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wengine hawajaona sana tatizo tulilonalo kwenye nchi hii. Mimi namwelewa sana Rais Samia, watu wengine wanataka tuishi kama ile enzi niliielezea sana kwenye hotuba siku ile. Mheshimiwa Rais alitupa dira tatizo anavyoliona na jinsi anavyoona tunaweza kulitatua.

Mheshimiwa Spika, pale zamani Watanzania walikuwa wachache tuko milioni tisa, vyuo vikuu una wataalam 12; una wataalam wawili, una wanafunzi 42. Hao wanafunzi huna kuumiza kichwa kuhusu ajira zao, lakini mazingira ya sasa eneo pekee ambalo linaweza likaajiri Watanzania wengi ni sekta binafsi. Sasa tuna kazi, tuna kazi ya kuifanya sekta binafsi ikue, tuna kazi ya kuwafanya watu waone ni heshima kufanya kazi kwenye sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilivyo sasa kuna watu ambao hata wako sekta binafsi hawaoni kama wako kazini, kwa sababu ya jinsi ambavyo tunai–*treat* sekta binafsi na kwa jinsi ambavyo tunaweka majina kwa watu wa sekta binafsi, lakini kama wote tutaipa heshima sekta binafsi, kama wote tutakuwa na lengo la kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika kukuza sekta binafsi, naamini watu watakuwa wanaona ni heshima kwenda kufanya sekta binafsi na tutakuza *tax base*.

Mheshimiwa Spika, tusipokuza sekta binafsi kodi zote zitabebwa na wanyonge, kwa sababu hauwezi ukaleta kodi mpya bila shughuli mpya ya uzalishaji, maana yake kama hatutakuza sekta binafsi *tax base* yetu itaendelea kubakia wafanyakazi wataendelea kubakia wachache ambao wanalipa kodi. Niliona niseme na hiyo ili tuweze kuelewana.

Mheshimiwa Spika, kuna Wabunge ambao waliongelea kuhusu taasisi zetu za Maliasili, Wizara ya Kisekta ilishafafanua na kama walivyosema Wizara ya Kisekta tumekaa nao na kwa kweli kuna mapendekezo ambayo tumeyaweka ambayo yataenda kutusaidia tuweze kupiga hatua kubwa kuliko pale ambapo tulikuwa.

Mheshimiwa Kakoso hewa ya ukaa pamoja na wenzake tumelipokea, tutakaa na Ofisi ya Makamu wa Rais kuweza kukimbizana na hili ili liweze kuwahi kufika hatima njema.

Mheshimiwa Spika, jambo la *ETS* limeongelewa sana na lenyewe tulikubaliana kwenye kikao cha Kamati ya Uongozi na kikao ambacho Serikali ilikuwa inafanya mashauriano na Bunge, tumekubaliana tunapokuja Bunge lile lingine tunatarajia na Mungu atusaidie tutakuja na utaratibu ambao tunaamini itakuwa hatua nzuri ambayo itatutoa hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na maeneo mawili yaliongelewa kwa nguvu; eneo moja lilikuwa la mafuta, tozo ya shilingi 100 kwenye mafuta; mimi niwaombe Wabunge na Waheshimiwa Watanzania, Serikali inafanya *simulation*/inafanya ufuatiliaji wa ndani kuhusu Soko la Dunia kwenye masuala ya mafuta *(fuel),* kwenye suala la mafuta ya kutumia nishati ile ya mafuta. Tena Watanzania hata msiwe na hofu na hii shilingi 100; kwa sababu gani? Kuna wakati ambapo mafuta yalipanda kwenye Soko la Dunia sio hata kwa ajili ya shilingi 100, Serikali ikaweka ruzuku ili mwananchi asipate shida. Sasa ikitokea mafuta yanashuka kwenye Soko la Dunia, si mbaya Serikali ikikusanya fedha hizo na ikapeleka kwenye miradi ya kimkakati, kwa sababu hata ikipanda kwa sababu nyingine ambayo sio hii ya shilingi 100 Rais Samia amekuwa akiwapa nafuu wananchi. Kwa nini upate shida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wakati mafuta yamepanda hata sio kwa ajili ya shilingi 100 na Rais akatoa unafuu. Sasa kama Soko la Dunia mafuta yanashuka ile *difference* Serikali ikikusanya ikatekeleza kwenye miradi kuna shida gani. Wanasema huenda yakapanda kule mbele, sasa kama mafuta yakipanda na Rais amekuwa anatoa unafuu kwa wananchi wake, hofu yako ni nini? Angalieni kwa nchi zote za *SADC* na *EAC* muone jinsi tofauti ya Rais Samia na maeneo mengine ambavyo walifanya. Kwa hapa aliweza kuweka ruzuku shilingi bilioni 100 kila mwezi na hapo sio kwamba Serikali ilikuwa imepandisha, yalipanda kwenye Soko la Dunia kule. Maana yake kama sio mtu anayejali wananchi wake angekuwa na sababu ya kutosha kabisa kusema yamepanda kwenye Soko la Dunia, kwa hiyo tupambane na hizo hali, lakini

yeyye akasema wananchi wasipambane na hali zao, akawapambania kwa kuweka shilingi bilioni 100 kila mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo niwasihii wananchi wenzangu wa Tanzania kwamba hii ni jambo jema kwa maana linataka kutunisha mifuko ya Serikali katika kutekeleza miradi ya kimkakati. Niwakumbushe Watanzania na Waheshimiwa Wabunge miradi ambayo Tanzania inatekeleza, miradi ya maendeleo ambayo Tanzania inatekeleza, hakuna nchi nyingine yoyote, majirani zetu na ukanda wote huu wa Afrika wanaotekeleza miradi mikubwa kwa mara moja kama Tanzania inavyotekeleza, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo wala tusitoetoe sana mifano mingine mingine, tunaweza tukawa tunatolea mfano kwa watu ambao hawa mradi hata mmoja mkubwa. Unaweza ukasema mbona hawa wanaishi hivi, unaweza ukawa wale unaowatolea huo mfano hawana hata mradi mmoja wa maendeleo, lakini sisi tuna miradi mikubwa ambayo tunatakiwa tujionee heshima kutekeleza miradi ya aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ukubwa wa miradi hiyo unatuonesha sisi ni nchi ya aina gani na *vision* ile ya viongozi wetu katika kutekeleza shughuli zinazolenga kuwakwamua wananchi kimaendeleo na Waheshimiwa Wabunge miradi hii mtaiona faida yake ikikamilika. Tunapojenga barabara za lami hatuna maana kwamba barabara hiyo tutaenda kukusanya hela, lakini shughuli zile zinazorahisisha katika kutembeza zile shughuli za kimaendeleo ndizo ambazo zinatuletea tija kubwa.

Kwa hiyo, hata hii miradi yote, bandari, reli madaraja, linalolengwa ni hilo, twendeni tuunge mkono wala tusirudi nyuma ndio patakuwepo na mzigo mzigo hivi lakini tuubebe tunaubeba kwa ajili ya nchi yetu na maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Watanzania haya ni mambo mema yanatutofautisha na watu wengine. Tunataka tunapomaliza dira ile nyingine inayofuata nchi yetu iwe

imeshatoka kwenye zile nchi zinazokuwa kwenye lile kundi la nchi maskini zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo ilitokea kwenye upande *cement*; Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote naomba watuelewa Serikali kwenye jambo hili, iko namna hii, nchi yetu ilijengwa kwenye misingi ya ujamaa na kujitegemea, watu wengi hizi *concept* mbili huwa hawazielewi sawa sawa. Ujamaa ni undugu kwamba usifurahie tu wewe pekee yako kufanikiwa huku wengine wakiwa wanapata shida. Sisi tuliokulia kwenye maji, Mheshimiwa Doto anafahamu ile mkijifunika nguo mmoja ilikuwa inaitwa Japan ukiigusa tu hivi inafyatuka inawakimbia wote, kipande kimoja cha Japan mnajifunika watu watano. Kwa hiyo, hapo anapata faida ni yule wa katikati wanakuwa wanapambana hawa wa pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua usifurahie wewe kufanikiwa pekee yako, lazima umbebe na mwingine wa chini ni jukumu lako, hivyo ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Sasa niambieni Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukilia dakika zote hapa kuna watoto wanapangwa elimu ya kati pale, wanapangwa waende vyuo vya kati pale, niambieni ninyi wenyewe anapangwa mtoto wa maskini aende vyuo vya kati pale. Vyuo vingine vyote tumewapa waweze kupata mikopo wote, lakini kwa idadi tu ya wingi wa watoto wa Kitanzania kwamba hawawezi wote tena wakaenda kidato cha tano na sita, haujafikiwa huo uwezo labda kwa sababu ya ongezeko linaloongezeka. Hivi tunavyoanza hivi kutoka mwezi wa tano mpaka sasa hivi tangia matokeo yametokea tumelazimika kujenga madarasa ya kuweza kukidhi lile ongezeko, ongezeko la watoto waliofaulu wametoka 75,000 mpaka 192,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tuna maeneo mengine kama hivyo vyuo vya kati hivyo *MUST*, *Arusha Technical* pamoja na *DIT* vipo ni vyuo vinavyozalisha wataalam tena wanaotakiwa na uelekeo wa nchi yetu katika kukuza sekta ya ualishaji, lakini watoto wa kimaskini wakienda kule wanakutana na ada. Mheshimiwa Samia akasemaje tutafute kwa yeyote aliye na kaunafuu unafuu atoe shilingi 20 kwa kilo, atoe shilingi 20 tupeleke elimu bure kwenye

vyuo vyetu vya kati na tupeleke tuanze kutoa mkopo kwenye vyuo vya kati kwa sababu hata wanaokwenda kwenye vyuo vya kati ni watoto wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutatoa wapi fedha ya kusomesha watoto wetu wa Kitanzania wanaokwenda vyuo vya kati. Ni lazima Watanzania tutagusana tu, ni lazima tutagusana, ndio tutagusana tu. Ndio inaweza ikakuongezea ka gharama, lakini ni lazima tumjali mtoto huyo. *(Makofi)*

Mimi baba yangu alikuwa na uwezo wa kuuza ng'ombe mmoja naenda sekondari, lakini nilipofika Chuo Kikuu kama nisingepata dirisha lile la *grant*, nisingeweza kufika kule Chuo Kikuu. Familia za aina hiyo bado zipo, mzazi wa mtoto maskini wa kijijini akiambiwa atoe shilingi milioni tatu, shilingi milioni nne, milioni ngapi, tena wengine wanasomea masomo ambayo tunayahitaji sana, sekta za afya, sekta hizi za uzalishaji. Watanzania tutakuwa tumeonesha mfano mbaya sana wa kizazi hiki cha leo tukishindwa kuwalipia watoto hao kwa sababu tu tunataka tujilimbikizie sisi ambao tumeshapata nafasi hiyo, kwamba wewe uwe hata na nyumba tano, uwe na nyumba kadhaa, lakini wale pale uwaache kabisa kwa sababu tu tunaogopa kubeba mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto wa Watanzania ni watoto wetu ni lazima tubebe huo mzigo, nawaomba Watanzania wote tukubaliane na maoni hayo hata kama yanatuongezea mzigo, inatuongezea mzigo kwa ajili ya watoto wetu. Hizo ni fedha ambazo zinakwenda kwenye kutengeneza Taifa lililo bora katika sasa na miaka inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe Watanzania urithi tuliopewa wa kuthaminiana ni urithi mkubwa sana katika Taifa letu. Hicho ndicho Rais Samia anachokisisitizia kwamba kama una unafuu, haujenda mbali sana, lakini una unafuu wasaidie na wengine walioko chini waweze kupanda, hicho ndicho anachojaribu kutuelekeza kwa kutumia taritibu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatambua tunapoenda kuongeza tozo mahali ama kuongeza kodi mahali, ni kweli

tunatambua kiwango kile kinaweza kisibaki kile kile. Tunaomba Watanzania wote tuelewane, ni lazima tutekeleze miradi ya kimaendeleo na ni lazima watoto wetu waweze kupata fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchi hii imewahi kupita kipindi ambacho watoto walikuwa wanafaulu vizuri halafu wanaambiwa hawajachaguliwa. Wengi wa rika letu hili watafuteni rafiki zetu, wengi walikuwa na akili na walifaulu, lakini waliambiwa hawajachaguliwa kana kwamba kwenda kidato cha kwanza ama kidato cha tano ni uchaguzi, unaambiwa huyu hajachaguliwa.

Mheshimiwa Spika, watoto wameongezeka sana baada ya elimu bila malipo. Tusiirudishe nchi yetu kwenye upungufu wa miundombinu ama upungufu wa uwezo wa kuweza kuwasaidia watoto wanaokwenda elimu ya juu, ama vyuo vya kati, ama sekondari kwa sababu za kibajeti. Ni lazima tuwabebe watoto wetu wote wapate elimu, tena elimu inayolingana, hiyo ndio *future* ya Taifa letu, ndio maana Rais Samia akaongeza *boom* elimu ya juu, *boom* sio lilelile ameongeza, ameongeza elimu bila ada kidato cha tano na sita, ameongeza elimu bila ada kwenye vyuo vile vya sayansi na ameongeza vyuo vya kati viingie hatua kwa hatua kwenye mikopo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hata hilo la hatua kwa hatua wala msilichukulie kwa *negative* na Watanzania wala msilichukulie kama wazo hasi, ni wazo chanya hata sasa kwenye elimu ya juu, sasa hivi kwenye elimu ya juu tulianza kwanza na watoto waliopangiwa vyuo vya Serikali, ndivyo tulivyoanza. Hatukuanza anza tu siku ya kwanza tukaanza vyuo vyote, tulianza na wachache, lakini tukawatumeanza, ikapiga hatua tukaongeza idadi, ikafika hatua tukaongeza vyuo, ikafika hatua tukaenda vyuo vya sekta binafsi ndio wabia wetu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivi sasa tukianza na wachache hii ni bajeti moja ya mwaka huu, mwaka unaofuata ndio na hii hamasa tunayoijenga na hii kukuza sekta binafsi na miradi mingine itakuwa imeisha, miaka miwili ijayo hatutakuwa na *commitment* za Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tutakuwa tumemaliza, uzalishaji utaongezeka, ile *saving* ambayo

tunapeleka trilioni 1.6 kila mwaka haitakwenda tena kwenye bwawa, maana yake tutaongeza uwezo wa kuwapeleka watoto walioko vyuo vya kati vya Serikali na visiovyo vya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Samia aliona tuwe na mahali pa kuanzia, fikirieni lipi ni jema je, angesema uwezo hauruhusu tukaacha kabisa vile vyuo vyote vya sayansi tukaacha kabisa, vile vya kati tukaacha kabisa, ili tusibiri uwezo utakaporuhusu, la hasha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yeye akaona twendeni tuanze kidogo kilichopo tuanze hatua kwa hatua kama tulivyoanza zamani. Zamani mikopo ilikuwa inapatikana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *Allied Universities*, nadhani Muhimbili pamoja na *UCLAS* baadaye baadaye ikaja na Mzumbe, baadaye baadaye ikaja *UCLAS*. Ikaenda ikiwa inakuwa mpaka ikaenda na vyuo vya sekta binafsi. Niwaombe mridhie huu ni utaratibu mzuri utaenda kuwagusa watoto wa Watanzania. Tusiridhike tukiwa tumekosa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo hiyo *concept* na inatumika sana hata kwenye masuala ya uwekezaji. Siku moja niliona kikatuni cha Kipanya kile, nilikiona kikatuni kile ni kama vile kuna mama mmoja alikuwa anaulizwa, Kipanya anamuuliza hivi katika nchi hii kuna matajiri na kuna maskini, wewe unapendaje, upandishwe uwe tajiri au matajiri washushwe wote wawe maskini? Yule akawaza *it's sadistic mind* akasema, kwa kuwa kutajirika ni kugumu mimi naomba washushwe wote tuwe maskini tu. Hilo si wazo jema, kama wanaweza wakapata wachache waanze, tutaenda tukikuwa waanze tunaenda tukikuwa yule ambaye haukuguswa mwaka huu ama kile chuo ambacho hakikuguswa kwa maana labda ni cha sekta binafsi wajue ndivyo tulivyoanza hata vile vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaenda na miradi fulani fulani tunaimaliza kama nilivyosema Daraja la Busisi linaelekea kuisha na Bwawa la Mwalimu Nyerere linaelekea kuisha. Kwa hiyo, tutaenda tukimaliza miradi hiyo na tutakapokuwa tumemaliza maana yake uwezo wa Serikali utaongezeka. Yule ambaye anakuwa na mashaka kuhusu utekelezaji wa mambo haya ya Rais Samia

anajipa mashaka yeye mwenyewe tu. Miaka miwili tu aliyoingia Rais Samia mikopo ya elimu ya juu ilikuwa chini ya shilingi bilioni 500 ilikuwa bilioni mia nne naa, hivyo tunavyoongea imeshafika shilingi bilioni mia saba naa, hilo ni ongezeko kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na tunavyoongeza na hii ya vyuo vya kati hii inaenda kwenye shilingi bilioni 800 maana yake anavyomaliza miradi ile mama ni mama mpeni maua yake. Hatuna haja ya kuwa na mashaka. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, *Chief Whip* amesema nirudie. Mama ni mama, mama yuko kazini mama apewe maua yake. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Biblia wale walienda wakamtembelea Yohana Mbatizaji alipokuwa amefungwa kule wakaenda wakamuelezea kwamba amepita Yesu amefanya hivi na hivi halafu yeye akawatuma, nendeni mkamuulize; je, wewe ni yule tuliyekuwa tunakusubiri au tuendelee kumsubiri mwingine? Yesu hata hakupata shida kuwaelezea zaidi akasema tu, "Wagonjwa wanapona, viwete wanatembea; nendeni mkawaambie heri wale wasio na mashaka na mimi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wale wengine wote, wale wengine wote wanaojadili kuhusu 2025. Ndugu zangu nimewatajia miradi yote hii na mambo ambavyo yameongezeka kwa kiwango cha mvua ile ambayo hamuwezi mkaonana nae, kwa kiwango cha mafuriko, unajadilije kuhusu uchaguzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengine niliyoyataja hapa kuna mengine hata sikuyataja ambayo Rais anafanya. Unajua mzigo mzito ukibebwa na mwenye nguvu kuna wakati huwa unaweza kuanza kuonekana ni mwepesi. Mambo anayofanya Rais Samia siyo kila mtu anaweza kuyafanya, siyo kila mtu anaweza kuyafanya. Kuna mengine siyo fedha, siyo fedha, siyo fedha lakini kama Kiongozi wa Nchi amesimamia tu mtu apatae haki yake lakini faraja anayoitengeneza kwa watu hao ni kubwa sana na inawaongezea umri wa kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, demokrasia ndani ya nchi kwa sababu ni jambo la kikatiba na kwa sababu imeonekana wazi ni jambo linaloleta maendeleo, jinsi ambavyo Rais amewaunganisha Watanzania ni mtaji mkubwa sana wa maendeleo kwenye nchi yetu na hili watu wote wanapaswa kuliheshimu. Mambo mengine Mheshimiwa Rais anafanya kwa hekima yake yeye kama yeye. anafanya yeye kama yeye na Mungu alivyomjalia anafanya kama kiongozi lakini anasaidia kuiunganisha nchi, anasaidia kuvutia uwekezaji lakini pia anaisaidia nchi kueleweka hata kwenye taasisi za kifedha sisi tukienda kule tunasikilizwa na fedha zinakwenda kwenye majimbo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo anafanya kwa hulka yake. Ni mengi tu hata sitaweza kuyataja kwa hiyo ni vyema tukamuheshimu na ni vyema tukamuunga mkono tusije tukafanya kama majuzi ambavyo ilianza kuonekana watu wanaweka weka vimaneno maneno. Mheshimiwa Rais ameonesha mfano ambao ni wa kiongozi na ni wa upekee hata hapa kwenye ukanda achilia mbali Tanzania, hata kwenye ukanda tu wa nchi majirani hakuna ambaye amefanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Katiba ya Nchi iliyoweka vyama vingi hakuna sehemu iliposema Mwenyekiti wa chama tawala aende kwenye chama kingine kwenye shughuli ya chama kingine, ni hulka yake na upendo wake amefanya hivyo. Hata kiwango cha uhuru wa kutoa maoni alichokitoa na hata wengine wakaamua kumsema yeye mwenyewe ni hulka yake na mimi niwakumbushe Watanzania tusije tukafanya kazi ya kuwatengenezea viongozi roho mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapohama kwenye hoja, Mheshimiwa Rais anakaribisha sana hoja lakini unapoondoka kwenye hoja za maendeleo ukaenda kwenye *personalities* hizo ni jitihada za kutengeneza roho mbaya kwa kiongozi. Tunasahau mapema sana, tunasahau mapema sana kwamba Katiba hii haijabadilika ni hii hii kama kuna wakati umenyimwa uhuru ni Katiba hii hii na kama kuna wakati umepewa uhuru wa kuweza hata kunyoosha kidole namna hiyo na kusema chochote namna hiyo na kubeza namna hiyo na kubagua namna hiyo na kutumia lugha ya

kibaguzi namna hiyo ni Katiba ni hii kwenye Lugha ya Kiswahili. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, ni kwamba pamoja na Katiba kuwepo unatakiwa utambue kuwa kiongozi pia amekufanyia uungwana kwamba angeweza kufanya kingine lakini kakufanyia uungwana. Kwa hiyo, Lugha ya Kiswahili inasema, “Usitukane mamba kabla ya kuvuka mto.” Tusifanye jitihada, tusifanye jitihada za kutengeneza roho mbaya kwa viongozi wetu, tuwalipe uungwana. Tuwalipe uungwana, inapokuwepo hoja tujadili hoja kwa Lugha ya Wanairamba tunasema usimfuate mamba kwenye kina kirefu cha maji. Twendeni tuwe tunajikita kwenye hoja tumepewa fursa ya kujadili hoja tuwe tunajikita kwenye hoja. Tuache kuongelea, tuache kuvuka mipaka, tuache kuongelea hoja zinazoweza kuligawa Taifa letu. *(MakofiVigelegele)*

Mheshimiwa Spika, niliona nilipazie sauti hilo kwa sababu sisi wengine wa rika lako na wadogo zako hatujawahi kuijua nchi nyingine tunaijua Tanzania tu na Mtanzania wa kona yoyote ya nchi ni Mtanzania hakuna nusu Mtanzania na hakuna Mtanzania na nusu. Mtanzania aliyeko kona yeyote ya nchi hii ni Mtanzania. Twendeni tuwe tunajadili hoja zinazoweza kuboresha utekelezaji wa masuala ya maendeleo badala ya kujadili watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa sababu nimesikia kengele. Tumezipokea hoja zote, hoja za kisekta zingine zimejadiliwa na Mawaziri wa Kisekta. Hoja zingine Waheshimiwa Wabunge mmezitoa moja moja, sisi Wizara tutakaa na Wizara za wenzetu za kisekta tutajadili hoja moja moja na zingine Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkifanya kazi nzuri sana na Wapigakura wenu watambue mmekuwa mkifanya kazi nzuri sana za kwenda kwenye Wizara moja kwa moja, mmekuwa mkifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna Mbunge ambaye hajaenda kumwona Waziri wote mmekuwa mkifanya hivyo mnaenda kufuatilia hoja moja kwa moja kwenye Wizara za kisekta. Kwa hiyo, hata zingine ambazo hatujazijibu ninawatangazia wananchi wenu kwamba Wabunge tutaendelea kukaa kwenye *sectors* na zile ambazo zinahusu Wizara ya Fedha tutakutana Wizara pamoja

na Mbunge kwa eneo mahususi, mradi mahususi ili tuweze kutekeleza na hayo ndiyo ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akitutuma na mengine Mawaziri wa kisekta pamoja na watendaji watakuja kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisitize moja la mwisho, twendeni tuendelee kuhamasishana kwa ajili ya kulipa kodi na kule watendaji tuendelee kusimamia miradi kwa ukaribu ili fedha hizi ambazo zinakwenda kule ziweze kutimiza malengo yaliyokusudiwa. Watendaji wote wa Serikali mnapopokea kule kwenye wilaya zetu, mnapopokea fedha watendaji wote mnapopokea fedha wajulisheni Wabunge hawa ambao wanafuatilia fedha huku kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haikupi gharama kumwambia Mbunge fedha zile ulizokuwa unafuatilia zimeshakuja na tunaanza utekelezaji haina gharama. Ni uungwana, yeye kafuatilia, yeye kafikisha mpaka kwa Rais, Rais amemjibu, fedha zimekuja kwenye jimbo lake ni jambo dogo tu mjulishe kwa sababu fedha zinaweza zikaja kabla ya vikao vile rasmi ambavyo vinakaa, mjulishe. Mimi ndivyo ambavyo wenzangu kule Iramba wamekuwa wakiniambia, wanawaambia madiwani, wanawaambia Mwenyekiti wa halmashauri, wananijulisha na mimi nashiriki na nikifika kwenye vikao tunaenda sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watendaji wote, wakurugenzi wote wajulisheni Wabunge fedha zinapofika. Mama amewasikiliza Wabunge ameleta fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo, wajulisheni kama zimekuja kabla ya kikao, msisubiri kuja kusema wakati wa vikao ili waendelee kutafuta fedha zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge mpokee salamu za Mheshimiwa Rais, yuko nanyi bega kwa bega tulipokuwa tunapitisha, tulipokuwa tunatoa *briefing* ya kikao hiki alisema yuko nanyi bega kwa bega na anawaomba mkitoka hapa mpeleke salamu kwa wananchi wote na yeye anawatakia kila la kheri. Anawaunga mkono, mko naye pamoja mtakapokuwa mnaelekea majimboni mwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika na baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Kwa mujibu wa taratibu zetu hoja ikitolewa, ikishaungwa mkono huwa inabidi Bunge lihojiwe lakini sasa kwa matakwa ya kanuni zetu kwa aina ya hoja iliyo mbele yetu sasa ambayo nadhani sote tunafahamu Katiba yetu inatukumbusha nini cha kufanya kutoka kwenye Ibara ya 90(2)(b) inasema. "Rais hatakuwa na uwezo wa kulivunja Bunge wakati wowote isipokuwa tu, (b) kama Bunge limekataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali."

Waheshimiwa Wabunge, na kanuni yetu ya 126 kwa Bajeti Kuu ya Serikali inataka kila Mbunge aitwe jina lake na aitike akipiga kura ile ambayo yeye anaona inafaa. Sasa tutaanza huo utaratibu muda siyo mrefu na kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge niwaombe kila mmoja atulie sehemu yake ili zoezi hilo liweze kuanza.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**KUPIGA KURA**

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Mussa Azzan Zungu | – | Ndiyo |
| Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa | – | Ndiyo |
| Mhe. Job Yustino Ndugai | – | Ndiyo |
| Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | | |

**SPIKA:** Ngoja Katibu.

Nadhani *microphone* ya Mheshimiwa Ndugai ilikuwa imewaka kijani. Mheshimiwa Mbunge ukishabonyeza na kusema ndiyo bonyeza tena ili kisemeo kiweze kuwa wazi kwa ajili ya Mbunge anayefuata na pia kama inawezekana kipindi hiki

tukikaa kimya ili Mbunge anayehusika asikie jina lake kwa sababu kura hii ni ya muhimu sana, sana, sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Job Yustino Ndugai | – | Ndiyo*(Makofi)* |
| Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | – | Ndiyo |
| Mhe. Daniel Baran Sillo | – | Ndiyo |
| Mhe. David Mwakiposa Kihenzile | – | Ndiyo |
| Mhe. Najma Murtaza Giga | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi | – | Ndiyo |
| Mhe. Capt. Mstaafu George Huruma Mkuchika | - | Ndiyo |
| Mhe. Jenista Joakim Mhagama | – | Ndiyo |
| Mhe. George Boniface Simbachawene | - | Ndiyo |
| Mhe. Innocent Lugha Bashungwa | - | Ndiyo |
| Mhe. Selemani Saidi Jafo | - | Ndiyo |
| Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako | – | Ndiyo |
| Mhe. Ummy Ally Mwalimu | - | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji | – | Ndiyo |
| Mhe. Hussein Mohamed Bashe | – | Ndiyo |
| Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba | – | Ndiyo |
| Mhe. January Yussuf Makamba | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax | – | Ndiyo |
| Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Mabula | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro | – | Ndiyo |
| Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima | - | Ndiyo |
| Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana | – | Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Omar Mchengerwa | – | Ndiyo |
| Mhe. Jumaa Hamidu Aweso | - | Ndiyo |
| Mhe. Nape Moses Nnauye | – | Ndiyo |
| Mhe. Angellah Jasmine Kairuki | – | Ndiyo |
| Mhe. Abdallah Hamis Ulega | - | Ndiyo |
| Mhe. Deogratius John Ndejembi | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Festo John Dugange | – | Hakuwepo |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. David Ernest Silinde | – | Ndiyo |
| Mhe. Khamis Hamza Khamis | – | Ndiyo |
| Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga | – | Ndiyo |
| Mhe. Paschal Patrobass Katambi | - | Ndiyo |
| Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe | – | Ndiyo |
| Mhe. Antony Peter Mavunde | – | Ndiyo |
| Mhe. Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe | – | Ndiyo |
| Mhe. Atupele Fredy Mwakibete | – | Ndiyo |
| Mhe. Hamad Hassan Chande | - | Ndiyo |
| Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato | - | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa | – | Ndiyo |
| Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk | – | Ndiyo |
| Mhe. Geophrey Mizengo Pinda | - | Ndiyo |
| Mhe. Jumanne Abdallah Sagini | - | Ndiyo |
| Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete | – | Ndiyo |
| Mhe. Mary Francis Masanja | - | Ndiyo |
| Mhe. Omari Juma Kipanga | - | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel | - | Ndiyo |
| Mhe. Mwanaidi Ali Khamisi | - | Ndiyo |
| Mhe. Pauline Philipo Gekul | - | Ndiyo |
| Mhe. Eng. Maryprisca Winfred Mahundi | - | Ndiyo |
| Mhe. Eng. Andrea Mathew Kundo | – | Ndiyo |
| Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma | - | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama | - | Ndiyo |
| Mhe. Vita Rashid Kawawa | – | Ndiyo |
| Mhe. Dennis Lazaro Londo | - | Ndiyo |
| Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo | - | Ndiyo |
| Mhe. Ally Juma Makoa | – | Ndiyo |
| Mhe. Moshi Selemani Kakoso | - | Ndiyo |
| Mhe. Dunstan Luka Kitandula | - | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza | - | Ndiyo |
| Mhe. Jerry William Silaa | – | Ndiyo |
| Mhe. Jackson Gedion Kiswaga | - | Ndiyo |
| Mhe. Fatma Hassan Toufiq | – | Ndiyo |
| Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka | – | *Abstain* |
| Mhe. Halima James Mdee | – | *Abstain* |
| Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo | – | Ndiyo |
| Mhe. Timotheo Paul Mnzava | – | Ndiyo |
| Mhe. Florent Laurent Kyombo | - | Ndiyo |
| Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri | - | Ndiyo |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Vincent Paul Mbogo | – | Ndiyo |
| Mhe. Justin Lazaro Nyamoga | – | Ndiyo |
| Mhe. Riziki Said Lulida | – | Ndiyo |
| Mhe. Anna Richard Lupembe | – | Ndiyo |
| Mhe. Husna Juma Sekiboko | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile | – | Ndiyo |
| Mhe. Anne Kilango Malecela | – | Ndiyo |
| Mhe. Judith Salvio Kapinga | – | Hakuwepo |
| Mhe. Omari Mohamed Kigua | – | Ndiyo |
| Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan | – | Ndiyo |
| Mhe. Vuma Agustine Holle | - | Ndiyo |
| Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga | – | Ndiyo |
| Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara | - | Ndiyo |
| Mhe. Capt. Abbas Ali Mwinyi | – | Ndiyo |
| Mhe. Abdallah Dadi Chikota | – | Ndiyo |
| Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo | - | Ndiyo |
| Mhe. Abdi Hija Mkasha | – | Ndiyo |
| Mhe. Abdul Yussuf Maalim | - | Ndiyo |
| Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood | - | Ndiyo |
| Mhe. Abdullah Ali Mwinyi | - | Ndiyo |
| Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Juma | - | Ndiyo |
| Mhe. Abeid Ramadhani Ighondo | - | Ndiyo |
| Mhe. Abubakari Damian Asenga | - | Ndiyo |
| Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly | - | Ndiyo |
| Mhe. Agnes Elias Hokororo | - | Ndiyo |
| Mhe. Agnes Mathew Marwa | – | Ndiyo |
| Mhe. Agnesta Lambert Kaiza | – | *Abstain* |
| Mhe. Ahmed Ally Salum | - | Ndiyo |
| Mhe. Ahmed Juma Ngwali | - | Ndiyo |
| Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby | - | Ndiyo |
| Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil | – | Ndiyo |
| Mhe. Aida Joseph Khenani | - | Hakuwepo |
| Mhe. Aleksia Asia Kamguna | – | Ndiyo |
| Mhe. Alexander Pastory Mnyeti | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Alfred J. Kimea | – | Ndiyo |
| Mhe. Ali Hassan Omar King | – | Ndiyo |
| Mhe. Ali Juma Mohamed | – | Ndiyo |
| Mhe. Yahya Ali Khamis | – | Hakuwepo |
| Mhe. Ali Vuai Khamis | – | Ndiyo |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage | – | Ndiyo |
| Mhe. Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila | – | Ndiyo |
| Mhe. Ally Mohamed Kassinge | – | Ndiyo |
| Mhe. Yahya Ally Mhata | – | Ndiyo |
| Mhe. Aloyce Andrew Kwezi | – | Ndiyo |
| Mhe. Aloyce John Kamamba | – | Ndiyo |
| Mhe. Amandus Julius Chinguile | – | Ndiyo |
| Mhe. Ameir Abdalla Ameir | – | Ndiyo |
| Mhe. Amina Ali Mzee | – | Ndiyo |

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Amina Bakar Yussuf | – | Ndiyo |
| Mhe. Amina Daud Hassan | – | Ndiyo |
| Mhe. Amina Iddi Mabrouk | – | Ndiyo |

**SPIKA:** Ngoja Katibu.

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Amina Iddi Mabouk | – | Ndiyo |

Endelea Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Amour Khamis Mbarouk | – | Ndiyo |
| Mhe. Anastazia James Wambura | – | Ndiyo |
| Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest | – | Sijaamua |
| Mhe. Angelina Adam Malembeka | – | Ndiyo |
| Mhe. Antipas Zeno Mgungusi | – | Ndiyo |
| Mhe. Anton Albert Mwantona | – | Ndiyo |
| Mhe. Asha Abdullah Juma | – | Ndiyo |
| Mhe. Asia Abdukarimu Halamga | – | Ndiyo |
| Mhe. Assa Nelson Makanika | – | Ndiyo |
| Mhe. Asya Mwadini Mohammed | – | Sijaamua |
| Mhe. Asya Sharif Omar | – | Hakuwepo |
| Mhe. Athuman Almas Maige | – | Ndiyo |
| Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe | – | Ndiyo |
| Mhe. Bahati Keneth Ndingo | – | Ndiyo |
| Mhe. Bahati Khamis Kombo | – | Hakuwepo |
| Mhe. Bakar Hamad Bakar | – | Ndiyo |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa | – | Ndiyo |
| Mhe. Benaya Liuka Kapinga | – | Ndiyo |
| Mhe. Benardeta Kasabago Mushashu | – | Ndiyo |
| Mhe. Boniphace Mwita Getere | – | Ndiyo |
| Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo | – | Ndiyo |
| Mhe. Boniventura Destery Kiswaga | – | Ndiyo |
| Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli | – | Ndiyo |
| Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata | – | Ndiyo |
| Mhe. Catherine Valentine Magige | – | Ndiyo |
| Mhe. Cecil David Mwambe | – | Ndiyo |
| Mhe. Cecilia Daniel Paresso | – | Sijaamua |
| Mhe. Charles John Poul Mwijage | – | Ndiyo |
| Mhe. Charles Muguta Kajege | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Christina Christopher Mnzava | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishangoma | – | Ndiyo |
| Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka | – | Ndiyo |
| Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza | – | Sijaamua |
| Mhe. Condester Michael Sichalwe | – | Ndiyo |
| Mhe. Constantine John Kanyasu | – | Ndiyo |
| Mhe. Cosato David Chumi | – | Ndiyo |
| Mhe. Daimu Iddi Mpakate | – | Ndiyo |
| Mhe. Daniel Awack Tlemai | – | Ndiyo |
| Mhe. Njalu Daudi Silanga | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. David Mathayo David | – | Ndiyo |
| Mhe. Deo Kasenyenda Sanga | – | Ndiyo |
| Mhe. Deodatus Philip Mwanyika | – | Ndiyo |
| Mhe. Deus Clement Sangu | – | Ndiyo |
| Mhe. Dorothy George Kilave | – | Ndiyo |
| Mhe. Edward Olelekaita Kisau | – | Ndiyo |
| Mhe. Edwin Enosy Swalle | – | Ndiyo |
| Mhe. Elibariki Immanuel Kingu | – | Ndiyo |
| Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka | – | Ndiyo |
| Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai | – | Ndiyo |
| Mhe. Emmanuel Peter Cherehani | – | Ndiyo |
| Mhe. Eric James Shigongo | – | Ndiyo |
| Mhe. Ester Amos Bulaya | – | Sijaamua |
| Mhe. Esther Edwin Malleko | – | Ndiyo |
| Mhe. Esther Lukago Midimu | – | Ndiyo |
| Mhe. Esther Nicholas Matiko | – | Sijaamua |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa | – | Ndiyo |
| Mhe. Fakharia Shomar Khamis | – | Ndiyo |
| Mhe. Felista Deogratius Njau | – | Sijaamua |
| Mhe. Festo Richard Sanga | – | Ndiyo |
| Mhe. Flatei Gregory Massay | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Florence George Samizi | – | Ndiyo |
| Mhe. Florent Laurent Kyombo | – | Ndiyo |
| Mhe. Francis Isack Mtinga | – | Ndiyo |
| Mhe. Francis Kumba Ndulane | – | Ndiyo |
| Mhe. Francis Leonard Mtega | – | Ndiyo |
| Mhe. Fredrick Edward Lowassa | – | Ndiyo |
| Mhe. Furaha Ntengo Matondo | – | Ndiyo |
| Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe | – | Ndiyo |
| Mhe. George Natany Malima | – | Ndiyo |
| Mhe. George Ranwell Mwenisongole | – | Ndiyo |
| Mhe. Ghati Zephania Chomete | – | Ndiyo |
| Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi | – | Ndiyo |
| Mhe. Grace Victor Tendega | – | Sijaamua |
| Mhe. Haji Amour Haji | – | Ndiyo |
| Mhe. Hamida Mohamed Abdallah | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla | – | Ndiyo |
| Mhe. Hamisi Shabani Taletale | – | Ndiyo |
| Mhe. Hasan Seleman Mtenga | – | Ndiyo |
| Mhe. Hassan Zidadu Kungu | – | Ndiyo |
| Mhe. Hawa Mchafu Chakoma | – | Ndiyo |
| Mhe. Hawa Subira Mwaifunga | – | Sijaamua |
| Mhe. Hussein Nassor Amar | – | Ndiyo |
| Mhe. Iddi Kassim Iddi | – | Hakuwepo |
| Mhe. Innocent Edward Kalogeris | – | Ndiyo |
| Mhe. Innocent Sebba Bilakwate | – | Ndiyo |
| Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe | – | Ndiyo |
| Mhe. Issa Ally Mchungahela | – | Hakuwepo |
| Mhe. Issa Jumanne Mtemvu | – | Ndiyo |
| Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi | – | Ndiyo |
| Mhe. Jacqueline Kainja Andrea | – | Ndiyo |
| Mhe. Jafari Wambura Chege | – | Ndiyo |
| Mhe. Janejelly James Ntate | – | Ndiyo |
| Mhe. Janeth Elias Mahawanga | – | Ndiyo |
| Mhe. Janeth Maurice Massaburi | – | Ndiyo |
| Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi | – | Ndiyo |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Jesca David Kishoa | – | Sijaamua |
| Mhe. Jesca Jonathani Msambatavangu | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo | – | Ndiyo |
| Mhe. John Marko Sallu | – | Ndiyo |
| Mhe. Jonas Van Zeeland | – | Ndiyo |
| Mhe. Jonas William Mbunda | – | Ndiyo |
| Mhe. Joseph Anania Tadayo | – | Ndiyo |
| Mhe. Joseph George Kakunda | – | Ndiyo |
| Mhe. Joseph Kasheku Musukuma | – | Ndiyo |
| Mhe. Joseph Michael Mkundi | – | Ndiyo |
| Mhe. Joseph Zacharius Kamonga | – | Ndiyo |
| Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima | – | Hakuwepo |
| Mhe. Josephat Sinkamba Kandege | – | Ndiyo |
| Mhe. Josephine Johnson Genzabuke | – | Ndiyo |
| Mhe. Josephine Tabitha Chagula | – | Ndiyo |
| Mhe. Juliana Daniel Shonza | – | Ndiyo |
| Mhe. Juliana Didas Masaburi | – | Ndiyo |
| Mhe. Juma Hamad Omar | – | Ndiyo |
| Mhe. Juma Othman Hija | – | Ndiyo |
| Mhe. Juma Usonge Hamad | – | Ndiyo |

**SPIKA:** Katibu ngoja hii ndio ya mwisho ni ya nani? Juma Othman Hija hayupo? Yuko wapi Juma Othman Hija? Yuko Bungeni?

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, nipo.

**SPIKA:** Eeh sawa. Haya Katibu endelea kutokea kwa Mheshimiwa Juma Othman Hija.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Juma Othman Hija | – | Ndiyo |
| Mhe. Juma Usonge Hamad | – | Ndiyo |
| Mhe. Jumanne Kibera Kishimba | – | Ndiyo |
| Mhe. Kabula Enock Shitobelo | – | Ndiyo |
| Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni | – | Ndiyo |
| Mhe. Khamis Kassim Ali | – | Ndiyo |
| Mhe. Kassim Hassan Haji | – | Ndiyo |
| Mhe. Katani Ahmadi Katani | – | Ndiyo |

Mhe. Kavejuru Eliadory Felix – Ndiyo
Mhe. Kenneth Ernest Nollo – Ndiyo

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Khadija Hassan Aboud – Ndiyo
Mhe. Khadija Shaaban Taya – Ndiyo
Mhe. Khalifa Mohamed Issa – Sijaamua
Mhe. Khalifa Salum Suleiman – Ndiyo
Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda – Hakuwepo
Mhe. Kunti Yusuph Majala – Sijaamua
Mhe. Latifa Khamis Juwakali – Ndiyo
Mhe. Leah Jeremiah Komanya – Ndiyo
Mhe. Eng. Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho – Ndiyo
Mhe. Balozi Liberata Rutageruka Mulamula – Ndiyo
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde – Ndiyo
Mhe. Lucy John Sabu – Ndiyo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga – Ndiyo
Mhe. Luhaga Joelson Mpina – Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Maida Hamad Abdallah – Ndiyo
Mhe. Maimuna Ahmad Pathan – Ndiyo
Mhe. Maimuna Salum Mtanda – Ndiyo
Mhe. Haji Makame Mlenge – Ndiyo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta – Ndiyo
Mhe. Mariam Nassoro Kisangi – Ndiyo
Mhe. Mariam Madalu Nyoka – Ndiyo
Mhe. Martha Festo Mariki – Ndiyo
Mhe. Martha Nehemia Gwau – Ndiyo
Mhe. Maryam Azan Mwinyi – Hakuwepo
Mhe. Maryam Omar Said – Hakuwepo
Mhe. Masache Njelu Kasaka – Ndiyo
Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki – Ndiyo
Mhe. Maulid Saleh Ali – Ndiyo
Mhe. Mbarouk Juma Khatib – Ndiyo
Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani – Ndiyo
Mhe. Michael Costantino Mwakamo – Ndiyo
Mhe. Michael Mwita Kembaki – Ndiyo
Mhe. Minza Simon Mjika – Ndiyo
Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu – Ndiyo
Mhe. Mohamed Abdulrahman Mwinyi – Ndiyo

Mhe. Mohamed Lujuo Monni – Ndiyo
Mhe. Mohammed Maulid Ali – Ndiyo
Mhe. Mohamed Said Issa – Sijaamua
Mhe. Mohamed Suleiman Omar – Hakuwepo
Mhe. Mrisho Mashaka Gambo – Ndiyo
Mhe. Muharami Shabani Mkenge – Ndiyo
Mhe. Munde Tambwe Abdallah – Ndiyo
Mhe. Munira Mustapha Khatib – Ndiyo
Mhe. Salim Mussa Omar – Ndiyo
Mhe. Mussa Ramadhani Sima – Ndiyo
Mhe. Mustafa Mwinyikondo Rajab – Ndiyo
Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge – Ndiyo
Mhe. Mwanakhamis Kassim Said – Ndiyo
Mhe. Mwantakaje Haji Juma – Ndiyo
Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis – Ndiyo
Mhe. Mwantumu Mzamili Zodo – Hakuwepo
Mhe. Mwantumu Dau Haji – Ndiyo
Mhe. Mwita Mwikabe Waitara – Ndiyo
Mhe. Nancy Hassan Nyalusi – Ndiyo
Mhe. Nashon William Bidyanguze – Ndiyo
Mhe. Ndaisaba George Ruhoro – Ndiyo
Mhe. Neema Gerald Mwandabila – Ndiyo
Mhe. Neema Kichiki Lugangira – Ndiyo
Mhe. Neema William Mgaya – Ndiyo
Mhe. Ng’wasi Damas Kamani – Ndiyo
Mhe. Nicodemas Henry Maganga – Ndiyo
Mhe. Nicholaus George Ngassa – Ndiyo
Mhe. Noah Lemburis Saputu Mollel – Ndiyo
Mhe. Norah Waziri Mzeru – Hakuwepo
Mhe. Nusrat Shaaban Hanje – Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Oliver Daniel Semuguruka – Ndiyo
Mhe. Omar Ali Omar – Hakuwepo
Mhe. Omar Issa Kombo – Ndiyo
Mhe. Oran Manase Njeza – Ndiyo
Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo – Ndiyo
Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi – Ndiyo
Mhe. Prof. Patrick Aloyce Ndakidemi – Ndiyo
Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato – Ndiyo
Mhe. Philipo Augustino Mulugo – Ndiyo
Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya – Ndiyo

Mhe. Priscus Jacob Tarimo – Ndiyo
Mhe. Rashid Abdallah Rashid – Ndiyo
Mhe. Rashid Abdallah Shangazi – Ndiyo
Mhe. Ravia Idarus Faina – Ndiyo
Mhe. Regina Ndege Qwaray – Ndiyo
Mhe. Rehema Juma Migilla – Ndiyo
Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo – Ndiyo
Mhe. Dkt. Ritta Enespher Kabati – Ndiyo
Mhe. Robert Chacha Maboto – Ndiyo
Mhe. Rose Cyprian Tweve – Ndiyo
Mhe. Rose Vicent Busiga – Ndiyo
Mhe. Saada Monsour Hussein – Ndiyo
Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe –

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tazameni visemeo vyenu mvizime. Mheshimiwa Saashisha.

Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe – Ndiyo

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Salim Alaudin Hasham –

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ukishatumia kisemeo kizime ili anayefuata kiwake.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Salim Alaudin Hasham – Ndiyo
Mhe. Salma Rashid Kikwete – Ndiyo
Mhe. Salome Wycliffe Makamba – Ndiyo
Mhe. Salum Mohammed Shaafi – Sijaamua
Mhe. Samweli Xaday Hhayuma – Ndiyo
Mhe. Santiel Eric Kirumba – Ndiyo
Mhe. Jaffar Sanya Jussa – Ndiyo
Mhe. Sebastian Simon Kapufi – Ndiyo
Mhe. Seif Khamis Said Gulamali – Ndiyo
Mhe. Seif Salim Seif – Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Selemani Jumanne Zedi – Ndiyo
Mhe. Shabani Omari Shekilindi – Ndiyo

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Shally Josepha Raymond | – | Ndiyo |
| Mhe. Shamsia Azizi Mtamba | – | Hakuwepo |
| Mhe. Shanif Mansoor Jamal | – | Ndiyo |
| Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya | – | Ndiyo |
| Mhe. Silyvetry Francis Koka | – | Hakuwepo |
| Mhe. Simai Hassan Sadiki | – | Ndiyo |
| Mhe. Simon Songe Lusengekile | – | Ndiyo |
| Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda | – | Hakuamua |
| Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo | – | Ndiyo |
| Mhe. Soud Mohammed Jumah | – | Ndiyo |
| Mhe. Stella Ikupa Alex | – | Ndiyo |
| Mhe. *Eng.* Stella Martin Manyanya | – | Ndiyo |
| Mhe. Stella Simon Fiyao | – | Hakuamua |
| Mhe. Subira Khamis Mgalu | – | Ndiyo |
| Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | – | Ndiyo |
| Mhe. Suma Ikenda Fyandomo | – | Ndiyo |
| Mhe. Sylvia Francis Sigula | – | Ndiyo |
| Mhe. Tabasam Hamis Mwagao | – | Ndiyo |
| Mhe. Tamima Haji Abass | – | Ndiyo |
| Mhe. Tarimba Gulam Abbas | – | Ndiyo |
| Mhe. Taska Restituta Mbogo | – | Ndiyo |
| Mhe. Tauhida Gallos Cassian | – | Ndiyo |
| Mhe. Tecla Mohamedi Ungele | – | Ndiyo |
| Mhe. Toufiq Salim Turky | – | Ndiyo |
| Mhe. Tumain Bryceso Magessa | – | Ndiyo |
| Mhe. Tunza Issa Malapo | – | Hakuamua |
| Mhe. Twaha Ally Mpembenwe | – | Ndiyo |
| Mhe. Ussi Salum Pondeza | – | Ndiyo |
| Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo | – | Ndiyo |
| Mhe. Venant Daud Protas | – | Ndiyo |
| Mhe. Wanu Hafidh Ameir | – | Ndiyo |
| Mhe. William Vangimembe Lukuvi | – | Ndiyo |
| Mhe. Yahaya Omary Massare | – | Ndiyo |
| Mhe. Yustina Arcadius Rahhi | – | Ndiyo |
| Mhe. Zacharia Paulo Issaay | – | Ndiyo |
| Mhe. Zahor Mohammed Haji | – | Ndiyo |
| Mhe. Zainab Athman Katimba | – | Hakuwepo |
| Mhe. Zaytun Seif Swai | – | Ndiyo |
| Mhe. Zubeida Khamis Shaib | – | Ndiyo |
| Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka | – | Ndiyo |

Mhe. Zuena Athumani Bushiri – Ndiyo
Mhe. Zulfa Mmaka Omar – Ndiyo

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kura zimeshapigwa nitampa Katibu nafasi kidogo akafanye hesabu ya hizo kura halafu nitawatangazia kama bajeti yetu itakuwa imepita au la.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, mwongozo. Taarifa samahani. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo, tusikilizane kidogo. Mheshimiwa Ally Mchungahela.

Mhe. Issa Ally Mchungahela – Ndiyo *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo, tusikilizane kidogo, wakati Mheshimiwa Ally Mchungahela akiitwa hakuonekana, hakusikika akijibu, lakini sasa ndiyo maana nimepa nafasi. Sasa yeye kuitwa ameamua aitike moja kwa moja. Mheshimiwa Mchungahela kwa sababu zoezi la kupiga kura lilikuwa limeshahitimishwa hebu nieleze ili nipate maelezo halafu nifanye uamuzi Mheshimiwa Mchungahela. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niombe radhi, nilipatwa na changamoto ya tumbo la ghafla. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya sawa, sawa…

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Wakati ulivyokuwa ukiniita nilikuwa nimetoka nje…

**SPIKA:** Umeshasikika, umeshasikika…

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Haya, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kura ya bajeti ni kura ya muhimu sana. Kwa muktadha huo nilikuwa nimeshamtoa Katibu ili akafanye hesabu, Katibu hebu arejee hapa ndani ili tuihesabu kura ya Mheshimiwa Ally Mchungahela. *(Makofi)*

*(Hapa Katibu wa Bunge na Makatibu Mezani walirejea Ukumbini)*

**SPIKA:** Namba ngapi? Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela namba yake ni 215 na tulikuwa tumeweka kwenye hakuwepo na sasa kwa sababu ameshakuja hapa ndani, Katibu atamwita ili kura yake ihesabiwe.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

Mhe. Issa Ally Mchungahela – Ndiyo *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Mheshimiwa uliyesimama tafuta kiti uketi. Waheshimiwa mnaozungumza nimesimama nasubiri mmalize kuzungumza, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tukisuburi Katibu wa Bunge atuletee matokeo tunaweza kufanya jambo moja ama mawili. Jambo la kwanza ni kuhusu wageni ambao wameingia baada ya zoezi hili kuanza, lakini pia jambo lingine linahusu kura. Kwa sababu huwa linakuja mara moja kwa mwaka, kwa maana kura ya kuitwa lakini wakati wa kupiga kura unapaswa kusema tu neno lile ambalo linaihusu kura yako usiongeze maneno wala kupunguza, kwa sababu Taarifa Rasmi za Bunge tunakuwa hatuna sehemu ya kwenda kuondelea hayo halafu tuache ile kura pekee. Kwa hiyo wakati wa kura ni kura pekee ndiyo inayopigwa usiongeze maneno wala usipunguze. Kwa hiyo hilo ni muhimu pamoja na kwamba linakuja mara moja kwa mwaka, lakini tulifahamu jambo hilo lina sura hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, wageni ambao tuko nao ambao hawakupata nafasi ya kutangazwa ni:-

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango na hawa ni Dkt. Natu El-maamry Mwamba ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo Ndugu Lawrence Mafuru ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Uchumi; Ndugu Amina Shaaban ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Fedha za Umma; Ndugu Mwanyika Semroki ambaye ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali; Dkt. Mursali Milanzi ambaye ni Kamishna wa Idara ya Mipango ya Kitaifa; Ndugu Elijah Mwandumbya ambaye ni Kamishna Uchambuzi wa Sera; Ndugu Meshack Anyingisye Kamishna wa Bajeti; Ndugu Khajida Said, Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima *TIRA;* Ndugu Royal Lyanga ambaye ni Kamishna Msaidizi, Idara ya Mipango ya Kitaifa; na Ndugu Alphayo Kidata, Kamishna wa *TRA*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Elisha Shigella Kamishna Msaidizi wa *TRA;* Ndugu Michael Muhoja, Kamishna Msaidizi *TRA;* Ndugu Mursali Milanzi, Kamishna Mipango ya Kitaifa; Ndugu Moshi Kabengwe, Mkurugenzi wa Utawala *TRA;* Ndugu Rishade Bade, Kamishina wa Idara ya Fedha za Nje. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine:-

Mheshimiwa Mwigulu Nchemba anao wageni wengine 27 ambao ni Madiwani kutoka Iramba Magharibi, karibuni sana. Waheshimiwa Madiwani hawa wa Wilaya ya Iramba wanaongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Ndugu Innocent Msengi, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan kutoka Chakechake Kusini Pemba. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 83 wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na hawa ni mabingwa wa *Mkenda Cup,* Wanakikundi cha Agape, Viongozi wa CCM wa Mkoa na Wilaya kutoka Rombo, Wajumbe wa Bodi na Mashabiki Bora wa Mkenda *Cup.* Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 46 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni wanafunzi, Walimu, wazazi na viongozi kutoka Mlalo, Lushoto, Mkoa wa Tanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 105 wa Mheshimiwa Mariam Ditopile ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Wilaya ya Kondoa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ambao ni wanafunzi wa Uuguzi na Ukunga kutoka Taasisi ya Afya na Sayansi Shirikishi Tosamaganga, Mkoani Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu kutoka Arumeru Magharibi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo nao ni wanafunzi 32 na Walimu saba kutoka Shule ya Msingi *Destiny* ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 90 wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mikoa ya Mbeya na Songwe. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, inaonekana wapo wageni wengine ambao hawajapata pengine nafasi ya kuingia kwa sababu ya sehemu za kukaa, nao watakapoingia tutapata nafasi ya kuwatangazia wageni ambao wamekuja hapa.

Tangazo la ile semina iliyokuwa imetangazwa kufanyika mchana saa saba kwenye Ukumbi wa Msekwa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Utekelezaji wa Mpango Kazi wa *FATF* pamoja na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2022 imeahirishwa hadi hapo mtakapojulishwa tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tutasubiri Katibu aingie na matokeo.

*(Hapa Wabunge walisubiri Matokeo ya Upigaji wa Kura ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024)*

## MATOKEO YA KURA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Katibu ameshamaliza kazi ya kuhesabu kura. Sasa nitawasomea matokeo ya kura iliyopigwa

hapa, kura ya maamuzi kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali au Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Wabunge waliokuwepo Bungeni ni 374, hii 374 hainihesabu mimi, kwa sababu nina kura ya uamuzi kwa hiyo siyo sehemu ya hii idadi. Wabunge waliokuwepo 374, idadi ya Wabunge ambao hawakuwepo Bungeni ni 18. Kwa sababu hapa ukipiga hesabu vizuri utagundua ni 392 kwa hiyo na mimi nakuwa wa 393 ndiyo idadi yetu kamili.

Waheshimiwa Wabunge, kura za hapana zilizopigwa ni 0, kura ambazo hazikuwa za uamuzi walitumia neno la Kiingereza *abstain* ni kura 20, kura za ndiyo ni kura 354. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imepitishwa kwa kura 354 ambazo ni sawa na asilimia 95 ya Wabunge waliopiga kura. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya sasa nitangaze rasmi kwamba Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, imepitishwa rasmi na Bunge na kwa muktadha huo nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye alileta bajeti yake hapa kama Kiongozi wetu Mkuu wa Serikali na Bunge limeipitisha Bajeti hiyo.

Kwa hiyo, ninampongeza sana yeye pamoja na Wawakilishi wake humu Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamad Chande kwa uwakilishi mzuri sana wa bajeti hii ya Serikali. Pia mlianza uwakilishi huo mzuri kwenye ngazi ya Kamati, mmeisikiliza Kamati mabadiliko tumeshuhudia mengi sana kipindi hiki, kwa hiyo tunawashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmeutoa kwa Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo, niwapongeze pia Kamati yetu ya Bajeti kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya kipindi chote hiki, ni kipindi ambacho mnakuwa na kazi nyingi lakini mmezifanya zote kwa ufanisi mkubwa, tunawapongeza sana.

Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii mmefanya kazi nzuri. Kwa muktadha huo Kamati yetu ya Bajeti inafanya kazi kwa karibu kabisa na Kamati zetu zote za Kisekta. Kila mmoja amefanya kazi nzuri sana Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizo, hoja mlizoziibua huko mkazipeleka Kamati ya Bajeti zikafanyiwa kazi na Wizara na hatimaye tumeweza leo kupitisha jambo ambalo lina mawazo yenu.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo, pamoja na kwamba tunapitisha bajeti ya Serikali lakini bajeti hii imefanya marekebisho mengi kabisa yale ambayo yametokana na mawazo yenu Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, nawapongeza Wabunge wote kwa kazi nzuri ya kizalendo mliyoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya pongezi hizo pia ninawashukuru wasaidizi wangu maana jambo hili jamani kuhitimishwa leo siyo masihara. Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, pia na Wasaidizi wetu wengine Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, nakushukuru sana kwa kazi nzuri, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile nakushukuru sana kwa kazi nzuri, pia Mwenyekiti wetu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, tunakushukuru sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana wote kwa kweli kwa ushirikiano wenu katika hili zoezi zima na pia upande wa Serikali tunawashukuru sana Mawaziri wote na Naibu Mawaziri mmekuwa mkizisikiliza Kamati zetu za kisekta mmefanya kazi nzuri sana tunawapongeza na tunawashukuru sana kwa ushirikiano mlioutoa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho kwa maana ya kupiga kura na kura imeshatoka kura ya maamuzi tumepitisha bajeti hii ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na sasa ni kazi yetu kuiwekea sheria hiyo bajeti ambayo tumeipitisha na kwa hivyo tutaendelea na kutunga sheria hiyo ambayo inaweka hiyo mipaka ya hizi fedha.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa mwaka 2023 *(The Appropriation Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu

**NDG. BAKARI KISHOMA- KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2023 *(The Appropriation Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2023 *(The Appropriation Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumeshasomewa hatua zote tatu za upitishaji wa sheria hii na kwa utaratibu wetu sote tunafahamu, japokuwa linajitokeza jambo hili mara moja kwa mwaka, sheria hii huwa haina mjadala wala haina mambo mengine yote, kwa sababu inaeleza yale mambo ambayo tumeshahojiwa hapa na tumekubali. Kwa hiyo, inazungumzia kiasi kile tulichopitisha na mahali zinakokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge sheria hii tumeshatunga hapa lakini ili tuwe tumetunga lazima

niwahoji ndiyo utaratibu wetu. Kwa hiyo, nitawahoji na nikiwahoji ndiyo tumeshapitisha hii sheria.

Waheshimiwa Wabunge, ambao mnaafiki kupitisha Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023 *(The Appropriation Bill, 2023)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Wale wasaidizi ambao huwa mnawashusha wageni huko juu, nikishasimama na wao wanapaswa kusubiri. Wasaidizi mnaowashusha wageni huko juu hilo ni tangazo lenu linawahusu.

Sawa. Waheshimiwa Wabunge nitangaze sasa rasmi kwamba Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023 *(The Appropriation Bill, 2023)* umepitishwa rasmi na Bunge. Kwa hiyo, kama ilivyoada kwa sheria zetu zote utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili aweze kusaini na hivyo matumizi ya fedha hizo yataanza mwaka huu wa fedha kwa maana 2022/ 2023 yanapokamilika siku ya tarehe 30 Juni na tarehe 1 Julai, sheria hii itaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023
### *(The Finance Bill, 2023)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu unasomwa kwa mara ya pili na kwa hivyo nitumie fursa hii kumuita

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 *(The Finance Act, 2023)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri. Nawashukuru pamoja na Kamati nzima ambayo Mheshimiwa Daniel Baran anaiongoza.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya kamati. Aidha kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote waliochangia katika hotuba ya Bajeti ya Serikali iliyopitishwa hivi punde.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waandishi wa Sheria na Wataalam wote wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unarekebishwa kupitia jedwali la marekebisho ya Muswada kufanya marekebisho ya sheria 18 zinazohusu mfumo wa kodi, ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa nchini na sheria mbalimbali pamoja na taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umelenga kusaidia katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika sekta za kimkakati ikijumuisha viwanda, kilimo, ufugaji, uvuvi, uchukuzi,

usafirishaji pamoja na sekta ya elimu na afya, ili kuboresha uzalishaji na kukuza uchumi, jumla kukuza ajira na hatimae kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi. Hatua hizi zinalenga pia kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ndani na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, Muswada huu unapendekeza marekebisho kwenye sheria nyingine mbalimbali kwa lengo la kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato, kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni sheria ambazo zinapendekezwa kufanyiwa marekebisho: -

(i) Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura Namba 218;
(ii) Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura Namba 306;
(iii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Namba 147;
(iv) Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura Namba 196;
(v) Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura Namba 249;
(vi) Sheria ya Ushuru wa Magari ya Kigeni, Sura Namba 84;
(vii) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura Namba 41;
(viii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Namba 332;
(ix) Sheria ya Ardhi, Sura Namba 113;
(x) Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura Namba 289;
(xi) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura Namba 290;
(xii) Sheria ya Madini, Sura Namba 123;
(xiii) Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura Namba 437;
(xiv) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura Namba 220;
(xv) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura Namba 438;
(xvi) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura Namba 399;
(xvii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura Namba 148; na
(xviii) Sheria ya Mafunzo na Ufundi Stadi, Sura Namba 82;

Mheshimiwa Spika, Maudhui ya Muswada huu yamegawanyika katika sehemu 19.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza, yenye Ibara za 1 na 2 yanahusu masuala ya utangulizi yanayohusisha jina na tarehe ya kuanza kutumika. Sehemu ya Pili yenye Ibara ya 3 hadi 4 inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki. Sura Namba Tatu Ibara za 5 na 6, inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 164A cha Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura Namba 306.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Nne Ibara ya Namba 7 na 10 inafanya kupendekeza marekebisho Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Namba ya 147. Ibara Namba 8 inapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 124 ili kubadili utaratibu wa kurekebisha viwango. Ibara Namba 9 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 137(3) ili kujumuisha huduma katika mahitaji la uwasilishaji wa ritani. Lengo la hatua ikiwa ni kuboresha usimamizi wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 inarekebisha viwango vya Ushuru wa bidhaa kwenye saruji, mafuta ya lami, sigara zinazotumia mbadala wa tumbaku, kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu. Kuongeza *H.S Codes* zilizomo kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na zile zilizomo kwenye Kitabu cha viwango vya pamoja vya ushuru cha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano inarekebisha Ibara ya 11 na 12 kama ilivyorekebishwa kwenye mapendekezo ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi. Sehemu ya Sita inarekebisha Jedwali la Marekebisho Ibara ya 13 na 14 kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho. Ibara ya 15 hadi 19, inafanya marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane yenye Ibara ya 20 hadi 31 inafanya marekebisho ya jedwali la marekebisho yanayopendekeza Sheria ya Kodi ya Mapato Sura Namba 132 na maeneo yake na naomba taarifa yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa inarekebisha Ibara ya 32 na 33 inafanya marekebisho kupitia jedwali la marekebisho

linalopendekeza marekebisho ya ardhi Sura Namba 113 kwa kuongeza Kifungu cha 33A ili kuweka utaratibu utakaowezesha makusanyo ya kodi ya ardhi katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Ibara ya 35 ambayo ni sehemu ya Kumi hadi Ibara ya 38 kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 238 na Ibara zake ambazo zinaainisha viwango.

Mheshimiwa Spika, upande wa Sehemu ya 11 yenye Ibara za 38 na 42 kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura Namba 290 kwa kuzingatia marekebisho ya urejeshaji wa asilimia 20. Ibara ya 41 inarekebisha Kifungu cha 9A ili kuwezesha kampuni zenye leseni za huduma za mtandaoni kulipa tozo ya huduma *(service levy)*. Ibara ya 42 inapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 31A ili kujumuisha jukumu la kukusanya ada ambayo inatoka Mamlaka ya Mapato kwenda Ofis ya Rais - TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 12 yenye Ibara ya 43, 44, inarekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura Namba 123.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 13 yenye Ibara za 45 na 46 inafanya marekebisho ya Jedwali la Marekebisho inayopendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 46A. Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura ya 347.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 14 yenye Ibara za 47 na 49, kama ilivyorekebishwa, imefanya marekebisho ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220 ambapo Ibara ya 48 na 49 zinapendekeza kurekebisha kifungu cha 4A cha Jedwali la Pili.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 15 yenye Ibara za 50 hadi 58, ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 138 ambapo Ibara ya 51 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 35(9). Ibara ya 52 inapenda kurekebisha Kifungu cha 36(1) kufuta maneno "kwa kutumia mashine za kielektroniki". Ibara ya 53 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 44 (1) pamoja na vifungu vingine.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 16 inafanya marekebisho Ibara ya 59 na 60 ambayo inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 23A ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399 ili kuruhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania kuendelea kubakiza mapato yanayokusanywa kutokana na uchakataji wa nyaraka za uingizaji wa mizigo hapa nchini *(Customs Processing Fees)*. Lengo la marekebisho haya ni kuwasaidia Mamlaka ya Mapato kuendelea na ujenzi wa mifumo ya kodi ya elektroniki, ununuzi wa vitendea kazi, usimamizi wa walipakodi pamoja na shughuli zingine za Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 16 yenye Ibara za 59 hadi 68, kimefanya marekebisho kupitia Jedwali la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 kama ambavyo tumeainisha kwenye vifungu vyake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 17 yenye Ibara za 69 hadi 73, kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, Sura Namba 182 ambapo Ibara ya 70 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 14. Ibara ya 71 iliyokuwa inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 15 ambayo imeondolewa. Ibara ya 72 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 16 na Ibara ya 73 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya hatua nyingine za mapato zilizopo katika hotuba ya bajeti na ambazo hazijabainishwa kwenye Muswada wa Sheria ya 2023, zitarekebishwa na Mawaziri husika kupitia Kanuni na Matangazo ya Serikali *(Government Notices)* kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho yaliyopendekezwa ni utekelezaji kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya Mwaka 2023/2024. Kwa hiyo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa naomba sasa kutoa hoja.

**MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2023 (THE FINANCE BILL, 2023) – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 **(The Finance Act, 2023)** pamoja na marekebisho yake sasa **usomwe kwa mara ya pili.**

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini** kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri ili kuuboresha Muswada huu.

3. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni leo tarehe 26 Juni, 2023. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waandishi wa Sheria na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Aidha, nawashukuru wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao kuhusu Muswada huu.

4. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 15 Juni 2023.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** Muswada huu kama ulivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho unakusudia kufanya marekebisho

ya Sheria **Kumi na Nane** zinazohusu mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali pamoja na taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Muswada huu umelenga kusaidia katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, hususan, katika sekta za kimkakati ikijumuisha viwanda, kilimo, ufugaji na uvuvi, uchukuzi na usafirishaji pamoja na sekta za elimu na afya ili kuboresha uzalishaji na kukuza uchumi wa jumla, kukuza ajira na hatimaye kupunguza ukali wa maisha ya wananchi. Hatua hizi zinalenga pia kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato ya ndani ya nchi na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, Muswada huu unapendekeza marekebisho kwenye sheria nyingine mbalimbali kwa lengo la kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato ya ndani, kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na kuboresha mazingira ya biashara.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** zifuatazo ni Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho:-

i) Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura ya 218;
ii) Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura ya 306;
iii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
iv) Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196;
v) Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249;
vi) Sheria ya Ushuru wa Magari ya Kigeni, Sura ya 84;
vii) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
viii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;
ix) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;
x) Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289;
xi) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
xii) Sheria ya Madini, Sura ya 123;
xiii) Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura ya 437;
xiv) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220;
xv) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;
xvi) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399;
xvii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; na
xviii) Sheria ya Mafunzo na Ufundi Stadi, Sura ya 82;

**MAUDHUI YA MUSWADA:**

7. ***Mheshimiwa Spika***, Muswada huu umegawanyika katika sehemu **Kumi na Tisa** kama ifuatavyo: -

8. ***Mheshimiwa Spika*, Sehemu ya Kwanza,** yenye Ibara za 1 na 2 inahusu masuala ya utangulizi yanayojumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo Sheria itaanza kutumika tarehe 1, Julai 2023.

9. ***Mheshimiwa Spika*, Sehemu ya Pili** yenye Ibara za 3 na 4 inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sura ya 218** kwa kurekebisha kifungu cha 48A ili kutoza tozo ya asilimia 1.5 kwenye *vinyl, mini disc, compact disk (CD), digital versatile disk (DVD) na SD memory*. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha usimamizi wa hakimiliki katika kazi za ubunifu.

10. ***Mheshimiwa Spika*, Sehemu ya Tatu** yenye Ibara za 5 na 6, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 164A cha **Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura ya 306** ili kufuta tozo kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea matumizi ya kielektroniki katika miamala mbalimbali.

11. ***Mheshimiwa Spika*, Sehemu ya Nne** yenye Ibara ya 7 hadi 10 inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147** kama ifuatavyo:

(i) Ibara ya 8 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 124 ili kubadili utaratibu wa kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kuwa kila baada ya miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2023/24. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha nchi kuwa na Sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji.

    Marekebisho haya yanalenga kurekebisha viwango mahsusi vinavyotozwa kwenye bia na bidhaa za tumbaku pamoja na bidhaa nyingine zisizo za mafuta isipokuwa mvinyo, bia inayotengenezwa kwa kutumia shayiri inayolimwa nchini, pombe kali na bidhaa za sukari (sugar confectionaries). Lengo la marekebisho haya ni kulinda thamani ya viwango

mahsusi ili ziendane na kiwango cha mfumuko wa bei na viashiria vingine vya kiuchumi.

Aidha, marekebisho yanalenga kurekebisha kifungu cha 124(5A) na (5B) ili kutoza ushuru wa bidhaa kwenye magari ya abiria yanayotumia teknolojia ya kisasa (hybrid vehicles) yaliyotumika kwa zaidi ya miaka mitano tangu yalipotengenezwa ili kuwianisha na magari mengine yanayofanana yanayotozwa ushuru huo. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza uingizaji wa magari chakavu na kulinda usalama wa abiria;

(ii) Ibara ya 9 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 137(3) ili kujumuisha huduma katika hitaji la uwasilishaji wa ritani. Lengo la hatua hii ni kuboresha usimamizi wa kodi; na

(iii) Ibara ya 10 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha Jedwali la Nne ili-

(a) kubainisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye saruji, mafuta ya lami, sigara zinazotumia mbadala wa tumbaku, sigara za kieletroniki na shisha.

(b) kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu pamoja na kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye pombe kali zinazozalishwa nchini zenye kiwango cha kilevi kisichozidi asilimia 7. Lengo ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza wigo wa kodi pamoja na mapato ya Serikali.

(c) kuoanisha *H.S Codes* zilizomo kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na zile zilizomo kwenye Kitabu cha viwango vya pamoja vya ushuru cha Jumuiya ya Afrika Mashariki cha mwaka 2022.

12. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Tano** yenye ibara za 11 na 12 **kama ilivyorekebishwa** inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 3 cha **Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196** kwa kurekebisha kifungu cha 3 ili kusamehe asilimia 80 ya malipwani au dola za marekani 0.52 kwa kilo kwa kuzingatia kiwango kilicho kikubwa cha tozo kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa na wawekezaji waliopo kwenye Kanda za

Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZ) kwenda nje ya nchi. Lengo ni kupunguza gharama za usafirishaji wa ngozi ghafi nje ya nchi.

13. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Sita inaingizwa kupitia Jedwali la Marekebisho** ikiwa na Ibara za 13 na 14 ambapo inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 4 cha **Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249** ili kuweka sharti la utoaji wa vibali vya usafirishaji nje ya nchi na uingizaji nchini wa nafaka na mazao mchanganyiko yakiwemo ngano, shayiri na mchuzi wa zabibu baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana na kilimo. Lengo ni kuhakikisha kuwa mazao yanayolimwa na watanzania yananunuliwa kwanza kabla ya uagizaji kutoka nje ya nchi.

14. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Sita** yenye Ibara za 13 na 14, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 3 cha **Sheria ya Ushuru wa Magari ya Kigeni, Sura ya 84** ili kuruhusu kutoza magari ya nje ya nchi viwango tofauti na vilivyoainishwa katika Jedwali iwapo nchi husika itatoza viwango vilivyo juu kuliko vinavyotozwa kwenye Jedwali la Sheria. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa na kulinda maslahi ya nchi.

15. ***Mheshimiwa Spika*, Sehemu ya Saba** yenye Ibara za 15 hadi 19, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41** kama ifuatavyo:

(i) Ibara ya 16 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 ili kuongeza tafsiri ya misamiati mbalimbali ili kuleta maana sahihi iliyokusudiwa katika masharti ya Sheria;

(ii) Ibara ya 17 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 13 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (4) ili kuweka takwa kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania kutoa leseni za michezo ya kubahatisha kwa kampuni ambayo angalau asilimia 5 ya hisa zake inamilikiwa na watanzania. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ushiriki/uwekezaji wa watanzania katika biashara ya michezo ya kubahatisha;

(iii) Ibara ya 18 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 26 ili kuruhusu kuanzishwa kwa michezo ya meza isiyozidi miwili katika maeneo yenye mashine za sloti arobaini kwa mujibu wa kanuni. Lengo la marekebisho ni kupanua wigo wa kodi; na

(iv) Ibara ya 19 iliyokuwa inapendekeza kurekebisha Jedwali la Pili la Sheria imeondolewa na Serikali kufuatia mashauriano na Kamati ya Bunge ya Bajeti.

16. ***Mheshimiwa Spika,* Sehemu ya Nane** yenye Ibara za 20 hadi 31, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332** kama ifuatavyo:

(i) Ibara ya 21 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4 ili kuweka utaratibu wa ukadiriaji kodi ya mapato kwa walipa kodi binafsi ambao wanafanya biashara ya usafirishaji wa abiria na mizigo na hawana wajibu wa kisheria wa kuwasilisha ritani za kodi. Lengo ni kuweka utaratibu maalum kwa walipa kodi ambao hawawajibiki kuwasilisha ritani ili kuongeza uwajibikaji katika Sheria;

(ii) Ibara ya 22 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 56 ili kuondoa miamala ya utoaji wa hisa mpya (*allotment of new shares*) na uhamishaji milki ya kampuni unaofanywa na wanahisa wakaazi katika utozaji wa kodi ya mapato. Lengo la marekebisho haya ni kuvutia uwekezaji nchini;

(iii) Ibara ya 23 inapendekeza kufuta Divisheni ya Sita ya Sehemu ya Tano ya Sheria ili kuweka utaratibu wa kukadiria kodi ya mapato kwa kutumia viwango elekezi vya kodi kwa kila gari kwa walipakodi binafsi ambao hawana wajibu wa kisheria wa kuwasilisha ritani za kodi;

(iv) Ibara ya 24 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 69 katika aya ya (m) kwa kujumuisha malipo ya huduma za kielektroniki kwenye malipo yenye vyanzo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kulinda na kuongeza wigo wa kodi;

(v) Ibara ya 25 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 82 ili kuondoa wajibu kwa watu binafsi kukata kodi ya zuio kwenye upangishaji wa nyumba. Lengo ni kuondoa wajibu kwa wapangaji wasiofanya biashara kulipa kodi ya zuio kwa niaba ya wenye nyumba ili kuwapunguzia adha ya kukusanya na kuwasilisha kodi hiyo Serikalini;

(vi) Ibara ya 26 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 83 ili kutoza kodi ya mapato kwa wamiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji wa madini na wachimbaji wadogo. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu maalum wa utozaji kodi ya mapato kwa wachimbaji husika na kutatua changamoto zilizopo kwenye ukusanyaji kodi katika sekta hiyo.
Aidha, Kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa ili kutoza kodi kwenye malipo yanayofanyika kwenye upunguzaji wa hewa ukaa. Lengo la marekebisho haya ni kuleta usawa wa ulipaji kodi na kupanua wigo wa kodi;

(vii) Ibara ya 27 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 86 ili kujumuisha malipo yanayofanywa na wamiliki wa leseni ndogo za uchimbaji madini na wachimbaji wadogo na mapato yatokanayo na upunguzaji wa hewa ukaa kuwa malipo ya mwisho ya kodi ya zuio (final withholding tax). Lengo la marekebisho ni kuongeza ukusanyaji na kuboresha usimamizi wa mapato;

(viii) Ibara ya 28 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 90 ili kuweka kiwango cha kodi ya asilimia 3 ya thamani ya mauzo au thamani ya ardhi au jengo kwa wauzaji wasiokuwa na nyaraka za kuthibitisha gharama za ununuzi na uendelezaji. Lengo la marekebisho ni kuweka utaratibu rahisi wa ukokotoaji wa kodi kwa mauzo ya ardhi au jengo kwa wauzaji ambao hawana nyaraka;

(ix) Ibara ya 29 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 90A ili kuwezesha utozaji wa huduma za kidijitali zinazotolewa kupitia soko mtandao na kuongeza muda wa kuwasilisha ritani za kodi ya huduma ya kidijitali. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha uwajibikaji;

(x) Ibara ya 30 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Kwanza la Sheria ili kuweka viwango vya kodi kwa wamiliki wa leseni ndogo za uchimbaji wa madini na wachimbaji wadogo, wanufaika wa malipo yatokanayo na upunguzaji wa hewa ukaa na walipa kodi binafsi wanaojihusisha na usafirishaji wa abiria au mizigo; na

(xi) Ibara ya 31 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Pili la Sheria ili kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji kwenye ubadilishaji wa muundo wa ndani wa kampuni za madini unaofanywa kwa kuzingatia matakwa ya mikataba ya msingi (Framework Agreement) iliyosainiwa kati ya Serikali na wawekezaji.

Lengo la marekebisho haya ni kuharakisha utekelezaji wa miradi ya ubia na kuiwezesha Serikali kutimiza jukumu la kimkataba kwa wakati. Inapendekezwa pia kurekebisha Jedwali la Pili ili kusamehe kodi ya mapato yanayotokana na uwekezaji unaofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwenye amana, hati fungani za muda mfupi au mrefu au gawio litokanalo na uwekezaji kwenye hisa. Lengo la marekebisho ni kuongeza pato kwa Mfuko ili kutoa huduma kwa ufanisi.

17. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Tisa** yenye Ibara za 32 na 33, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura 113 kwa kuongeza kifungu kipya cha 33A ili kuweka utaratibu wa kuwezesha makusanyo kodi ya ardhi kuwekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

18. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Kumi** yenye Ibara za 35 hadi 38, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289** kama ifuatavyo:

(i) Ibara ya 35 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 6 ili kujumuisha maeneo yote ya Wilaya katika utozaji wa kodi ya majengo isipokuwa majengo yaliyosamehewa katika Sheria. Lengo ni kuweka usawa katika kulipa kodi;

(ii) Ibara ya 36 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 ili kuongeza maeneo ambayo hayatahusishwa na utozaji wa kodi ya majengo ambayo ni pamoja na nyumba za tope, fito, tembe, nyasi na nyumba zinazofanana na hizo kwa ajili ya makazi. Lengo ni kuleta usawa katika kulipa kodi; na

(iii) Ibara ya 37 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 16 ili kuongeza kodi ya majengo kwa mwaka kutoka shilingi 12,000/= hadi shilingi 18,000/= kwenye majengo yasiyo ya ghorofa, na kutoka shilingi 60,000/= Kwenda shilingi 90,000/= kwa kila sakafu ya ghorofa. Lengo la hatua hii ni kuakisi kodi na thamani halisi ya majengo. Aidha, marekebisho yanafanyika katika kifungu hicho kwa kuwezesha asilimia 20 ya mapato kurejeshwa Halmashauri ili kuziwezesha katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi hizo.

19. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Kumi na Moja** yenye Ibara za 38 hadi 42, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290** kama ifuatavyo:

(i) Kwa kuzingatia marekebisho ya urejeshwaji wa asilimia 20 ya mapato katika Halmashauri kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa katika **Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289**, Ibara ya 39 na 40 zinapendekeza kurekebisha kifungu cha 6 na 7 mtawalia, ili kubainisha urejeshwaji huo kama sehemu ya vyanzo vya mapato kwenye mamlaka za miji na halmashauri za wilaya mtawalia;

(ii) Ibara ya 41 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 9A ili kuwezesha kampuni zenye leseni za huduma za fedha mtandaoni kulipa tozo ya huduma (service levy) kwenye Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambayo itagawanya makusanyo yatokanayo na tozo hiyo kwenye kila Halmashauri husika badala ya utaratibu wa sasa ambapo Kampuni hizo hupaswa kulipa kwenye kila Halmashauri ambapo wanafanya shughuli. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uwajibikaji kwa Kampuni husika na pia

kupunguza gharama za ufuatiliaji wa tozo hiyo kwa halmashauri; na

(iii) Ibara ya 42 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 31A ili kuhamisha jukumu la kukusanya ada ya mabango kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenda Ofis ya Rais - TAMISEMI. Vilevile, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa ili kuhamisha jukumu la kukusanya kodi ya pango kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenda Ofisi ya Rais – TAMISEMI ifikapo tarehe 1 Januari, 2024. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa ada ya mabango kwa kutumia Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambayo muundo wake wa kiutawala umefika hadi ngazi za kata, vijiji na mtaa, hivyo kurahisisha masuala ya ufuatiliaji na usimamizi.

20. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Kumi na Mbili** yenye Ibara za 43 na 44**, kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Madini, Sura 123** kama ifuatavyo:

(i) Ibara ya 44 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 90A(5) ili kutoa msamaha kwa vituo vya kusafishia madini (refineries) wa kulipa ada ya ukaguzi ya asilimia 1. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea kasi ya ukuaji wa sekta ndogo ya usafishaji wa madini nchini na kuvutia uwekezaji zaidi, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali; na

(ii) Ibara mpya ya 45 inaingizwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kurekebisha kifungu cha 87(1) ili kupunguza kiwango cha mrabaha kwenye chumvi kutoka asilimia 3 hadi asilimia 1.

21. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Kumi na Tatu** yenye Ibara za 45 na 46 **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 46A cha **Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura ya 437** ili kufuta tozo ya miamala kwenye kila muamala wa kutuma fedha na badala yake kubakiza tozo kwenye miamala ya kielekroniki ya kutoa fedha. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utozaji wa tozo ya

muamala mara mbili kwenye miamala mmoja pamoja na kuchochea ufanyaji wa miamala kwa njia za kielektroniki (cashless transactions).

22. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Kumi na Nne** yenye Ibara za 47 hadi 49, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220** ambapo Ibara ya 48 na 49 zinapendekeza kurekebisha kifungu cha 4A na Jedwali la Pili la Sheria ili kuongeza ushuru wa barabara na mafuta kwa kiasi cha shilingi 100/= kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli. Lengo la marekebisho haya ni kupata vyanzo vya uhakika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo.

23. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Kumi na Tano** yenye Ibara za 50 hadi 58, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438** kama ifuatavyo:

(i) Ibara ya 51 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 35(9) ili kuboresha tafsiri ya msamiati "primary data server" ili kujumuisha seva mtandao au aina yoyote ya kifaa maalumu kwa lengo la kuhifadhi taarifa za kielektroniki za mlipa kodi hapa nchini. Lengo la marekebisho haya ni kutambua aina nyingine za seva zinazoweza kutumika na mlipa kodi kwa ajili ya kuhifadhi taarifa, kupunguza gharama za usimikaji wa seva na kurahisisha utoaji wa taarifa pindi zinapohitajika.

    Aidha, kifungu kidogo cha (10) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza muda unaohitajika kutekeleza takwa hili la kisheria kuanzia tarehe 1 Januari, 2024. Lengo la marekebisho haya ni kuwapa Walipakodi muda wa ziada wa kukamilisha maandalizi kabla ya kuanza kutekeleza takwa hili la sheria;

(ii) Ibara ya 52 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 36(1) ili kufuta maneno "kwa kutumia mashine za kielektroniki" ili kuruhusu utoaji wa risiti kwa vifaa au teknolojia nyingine mbali na mashine za kielektroniki za kutolea risiti. Lengo la

marekebisho ni kutambua matumizi ya vifaa au teknolojia nyingine zinazotumika kutoa risiti za kielektroniki;

(iii) Ibara ya 53 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 44A (1) ili kuweka muda wa uwasilishwaji wa taarifa za mikataba ya ukandarasi ya ujenzi na uchimbaji (construction and extractive industry) kwa Kamishna Mkuu. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwajibikaji wa mlipa kodi na kuboresha usimamizi wa kodi;

(iv) Ibara ya 54 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 45A ili kuongeza kifungu kidogo cha (4) kwa lengo la kutoa tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi na kurahisisha usimamizi wa sehemu za kuhifadhia mizigo (storage facilities);

(v) Ibara ya 55 inayopendekeza kurekebisha kifungu cha 51 imeondolewa na Serikali kufuatia mashauriano baina yake na Kamati ya Bunge ya Bajeti;

(vi) Ibara ya 56 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 71(3) ili kutambua mazingira mengine yanayoweza kupelekea Mlipakodi kuomba marejesho ya kodi baada ya miaka mitatu (3) tangu kodi kulipwa. Lengo la marekebisho haya ni kuleta usawa na kuboresha misingi ya utoaji haki katika usimamizi wa kodi;

(vii) Ibara ya 57 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 86(1) na (4) ili kurekebisha adhabu zitokanazo na kutotoa au kutodai risiti. Lengo la marekebisho haya ni kuweka adhabu inayowiana na kosa lililotendeka; na

(viii) Ibara ya 58 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Kwanza la Sheria ili kuongeza ritani zinazotokana na tozo ya kitanda kwa siku inayotozwa kupitia Kanuni za Tozo ya Maendeleo ya Utalii ya mwaka 2013. Lengo la marekebisho haya ni kujumuisha ritani hizo miongoni mwa ritani zinazopaswa kuwasilishwa kwa Kamishna Mkuu.

24. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu mpya ya Kumi na Sita inaingizwa kupitia Jedwali la Marekebisho** ikiwa na Ibara za 59 na

60 ambapo inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 23A cha **Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399** ili kuruhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania waendelee kubakisha mapato yanayokusanywa kutokana na uchakataji wa nyaraka za uingizaji wa mizigo hapa nchini (Customs Processing Fees). Lengo la marekebisho haya ni kuwasaidia Mamlaka ya Mapato Tanzania kuendeleza ujenzi wa mifumo ya kodi ya kielektroniki, ununuzi wa vitendea kazi, usimamizi wa walipakodi pamoja na shughuli nyingine za Mamlaka.

25. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Kumi na Sita** yenye Ibara za 59 hadi 68, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148** kama ifuatavyo;

(i) Ibara ya 60 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 2 ili kuongeza tafsiri ya risiti za kodi za kielektroniki na kuweka tafsiri sahihi iliyokusudiwa;

(ii) Ibara ya 61 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha kifungu cha 6 ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye malighafi za kutengenezea vifungashio vya madawa.

Vilevile, Kifungu cha 6 kinarekebishwa ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye hema za chuma zitakazoagizwa kutoka nje ya nchi au hema za chuma zilizozalishwa nchini zinaponunuliwa na wafugaji wa kuku. Lengo la hatua hizi ni kuwapunguzia gharama wazalishaji na kukuza sekta husika;

(iii) Ibara ya 62 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 11 ili kuruhusu ahirisho la kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa za mitaji zilizozalishwa nchini na kusitisha utaratibu wa kutoa ahirisho la kodi kwa bidhaa za mtaji zinazoingizwa kutoka nje ya nchi baada ya miaka mitatu. Lengo la marekebisho haya ni kuvutia uwekezaji wa kuzalisha bidhaa za mtaji ndani ya nchi, kuongeza uzalishaji, ajira na mapato ya serikali;

(iv) Ibara ya 63 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 51 ili kupanua wigo wa kodi kwa kujumuisha huduma nyingine za kielektroniki kwenye orodha ya huduma za kielektroniki zinazotozwa kodi;

(v) Ibara ya 64 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha kifungu cha 55A ili kuongeza muda wa kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye mbolea inayozalishwa nchini hadi kufikia mwezi Juni, 2024 kwa lengo la kuleta unafuu kwa wakulima na walaji;

(vi) Ibara ya 65 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 55B ili kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa nchini ili kukuza uzalishaji wa viwanda vya ndani na kuwapunguzia gharama watumiaji;

(vii) Ibara ya 66 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 69 ili kuainisha matumizi sahihi ya vifungu vya sheria za kodi na kurahisisha usimamizi wa kodi;

(viii) Ibara ya 67 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 86 ili kutambua risiti za kielektroniki kwa kuwianisha na tafsiri iliyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi;

(ix) Ibara ya 68 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha Jedwali la Sheria ili-

(a) kuakisi mawanda ya bidhaa zilizosamehewa na kuoanisha *H.S Codes* zilizomo kwenye Sheria na zile zilizomo kwenye kitabu cha viwango vya pamoja vya ushuru cha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki cha mwaka 2022.

(b) kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyumba za gharama nafuu zenye thamani isiyozidi shilingi milioni 50, ili kutoa unafuu kwa wanunuaji wa nyumba hizo na kuboresha maisha ya watanzania.

(c) kusamehe kodi ya VAT kwenye huduma za “software za gaming na gaming odds” ili kupunguza gharama kwa Waendeshaji wa michezo ya kubahatisha

(d) kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye uuzaji na ukodishaji wa ndege, injini za ndege na vifaa vyake pamoja na ukarabati ili kuleta unafuu kwa waendeshaji wa shughuli za usafiri wa anga kwa kuwawezesha kununua bidhaa husika nchini au kuagiza kutoka nje ya nchi na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta ya usafiri wa anga.

(e) kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye uuzaji wa madini ya thamani, madini ya vito na madini mengine ya thamani kwenye masoko ya madini, vituo vya uuzaji wa madini na vituo vya kusafisha dhahabu (refineries) kwa lengo la kuchochea uuzaji wa madini katika masoko na vituo vilivyo rasmi na kuongeza mchango wa sekta ya madini;

(f) kuongeza muda wa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho yaliyotokana na mbegu zilizozalishwa nchini hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024. Aidha, Jedwali linarekebishwa ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vinavyotumika kubadilisha mfumo wa magari kutoka kutumia mafuta kwenda utumiaji wa gesi au umeme.

26. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Kumi na Saba** yenye Ibara za 69 hadi 73, **kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, Sura ya 82** kama ifuatavyo:

(i) Ibara ya 70 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 14 ili kupunguza kiwango cha tozo ya ufundi stadi kutoka asilimia nne hadi asilimia tatu pointi tano. Lengo la hatua hii ni kuwapunguzia waajiri gharama za uendeshaji wa shughuli zao;

(ii) Ibara ya 71 iliyokuwa inapendekeza kurekebisha kifungu cha 15 imeondolewa baada ya mashauriano baina ya Kamati ya Bunge ya Bajeti na Serikali;

(iii) Ibara ya 72 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 16 ili kuondoa jukumu la kuwasilisha ritani kwa waajiri ambao hawana wajibu wa kulipa tozo ya ufundi stadi; na

(iv) Ibara ya 73 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 19 ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana na fedha baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana na elimu kutoa hati ya msamaha wa tozo ya ufundi stadi baada ya kujiridhisha kuwa msamaha husika ni kwa maslahi ya umma.

27. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, baadhi ya hatua nyingineza za mapato zilizopo katika Hotuba ya Bajeti na ambazo hazijabainishwa kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023, zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia Kanuni na Matangazo ya Serikali (*Government Notices*) kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika.

**HITIMISHO:**

28. ***Mheshimiwa Spika***, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24. Kwa hiyo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake.

29. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Mheshimiwa Waziri ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimuite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo aje awasilishe maoni ya Kamati.

**MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba tarehe 20 Juni, 2023 uliuelekeza muswada huo kuletwa katika Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa ajili ya kuufanyia kazi na kutoa maoni yake Bungeni. Aidha, kama zilivyo Kanuni za Bunge, muswada huo uliwasilishwa rasmi kwenye Kamati tarehe 20 Juni, 2023 kwa niaba ya Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba.

Mheshimiwa Spika, muswada huu unakusudia kufanya marekebisho mbalimbali yenye lengo la kurekebisha mfumo wa kodi, viwango vya kodi, ada na tozo chini ya sheria mbalimbali pamoja na kuboresha utaratibu wa ukusanyaji na usimamizi wa mapato ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 Kamati ilifanya mkutano na wadau *(public hearing)* kwa siku mbili tarehe 22 na 23 Juni, 2023 ili kupokea maoni yao kwa lengo la kuboresha muswada huo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue wadau waliofika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa maoni ambao ni Chama cha Wawindaji wa Kitalii, Chama cha Wazalishaji wa Chumvi, Chama cha Mabenki Tanzania, Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Tanzania, Chama cha Waendesha Michezo ya Kubahatisha, Kampuni ya Saruji ya Mbeya *(Mbeya Cement)*, Shirikisho la Viwanda Tanzania, Kampuni za Bia za *TBL* na Serengeti, Kampuni ya *Asas Dairies*, Kampuni ya Madini ya Barrick, Shirikisho la

Wachimba Madini, na Kampuni ya Sigara Tanzania. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kukutana na Mawaziri kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Elimu. Aidha, Kamati ilikutana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Mwandishi wa Sheria, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha na Ofisi ya Hakimiliki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati Kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023. Sheria zinazofanyiwa mabadiliko; muswada huu unafanya mabadiliko katika sheria 18 zifuatazo:-

(i) Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki;

(ii) Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki;

(iii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa;

(iv) Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi;

(v) Sheria ya Ushuru wa Magari ya Kigeni;

(vi) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha;

(vii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;

(viii) Sheria ya Ardhi;

(ix) Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo;

(x) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa;

(xi) Sheria ya Madini;

(xii) Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa;

(xiii) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta;

(xiv) Sheria ya Usimamizi wa Kodi;

(xv) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani;

(xvi) Sheria ya Usalama wa Chakula;

(xvii) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania; na

(xviii) Sheria ya Mafunzo na Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mabadiliko; muswada huu unafanya mabadiliko katika sheria hizo kwa malengo makuu yafuatayo:-

i. Kupanua wigo wa kodi kwa kuanza kutoza kodi kwa baadhi ya bidhaa na huduma ambazo zilikuwa hazitozwi;

ii. Kuongeza uwajibikaji wa mlipa kodi;

iii. Kuongeza mauzo ya nje ya nchi;

iv. Kuchachua shughuli za uzalishaji mali ndani ya nchi;

v. Kuweka usawa wa utozaji kodi pamoja na kulinda maslahi ya nchi;

vi. Kuimarisha usimamizi wa hakimiliki katika kazi za ubunifu;

vii. Kuchochea matumizi ya kielektroniki;

viii. Kufuta kodi na tozo zinazoonekana kuwa kero;

ix. Kuboresha usimamizi wa kodi pamoja na kuondoa mianya ya ukwepaji wa kodi;

x. Kuchochea ukuaji wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na kuvilinda viwanda vya ndani; na

xi. Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya sheria ambayo Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali; Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki; sheria hii inapendekeza kuongeza bidhaa zinazotumika kuhamishia, kutunzia, kudurufu na kusambaza bidhaa na huduma za sanaa zinazoingizwa nchini kutozwa tozo ya asilimia 1.5 ya thamani. Hatua hii ina lengo la kupanua wigo wa kodi na kuweka usawa katika utozaji ili kuendeleza na kulinda sekta ya michezo na burudani.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki; Serikali inakusudia kufuta tozo kwa kila laini ya simu na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji. Hatua hii imetokana na ukweli kwamba kifungu hiki kimeshindwa kutekelezeka kwa sababu ya kuongezeka kwa matumizi ya kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi; mabadiliko ya sheria hii yanalenga kusamehe asilimia 80 ya tozo kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa na wawekezaji waliopo kwenye Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(EPZ)* kwenda nje ya nchi. Hatua hii ina lengo la kuchochea mauzo ya ngozi mbichi nje ya nchi na hivyo kuongeza fedha za kigeni. Aidha, mapendekezo haya yanalenga wachakataji wa nyama waliopo maeneo ya *EPZ* kwa ajili ya mauzo nje ya nchi katika maeneo ya *EPZ*.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Magari; katika sheria hii mabadiliko yanalenga kutoza ushuru wa magari ya nje ya nchi sawa na viwango vya ukanda wa *EAC, SADC* na *COMESA*. Endapo viwango vinakavyotozwa katika nchi zilizopo katika kanda hizo utakuwa mkubwa kuliko ule unaotozwa nchini basi viwango vinavyotozwa katika nchi hiyo vitatumika pia nchini *(reciprocity)*. Pendekezo hili lilitolewa na Kamati ya Bajeti katika Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka wa fedha 2022 wakati Kamati inawasilisha taarifa yake kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi ule ule wa *reciprocity*, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuanzisha tozo nyingine zinazotozwa na nchi nyingine kwa magari ya nje ya nchi kama vile *park fee*, *carbon emission fee* na *toll gate*. Vyanzo hivi vinaweza kuongeza wigo wa mapato ya Serikali kwa sababu, nchi nyingine za jirani hutoza tozo hizo kwa magari ya Tanzania yanapotumia barabara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini, Sura ya 123; mapendekezo ya Serikali yanalenga kusamehe ada ya ukaguzi ya asilimia moja katika vituo vya kusafishia madini *(refineries)*. Hatua hii itaenda kuchochea kasi ya ukuaji wa sekta ndogo ya usafishaji wa madini nchini na kuvutia uwekezaji. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kupunguza mrahaba kwenye madini ya chumvi kutoka asilimia tatu hadi asilimia moja kutokana na ukweli kwamba chumvi ni madini, lakini pia ni chakula, hivyo si sawa kutozwa sawasawa na madini mengine. Serikali ilikubali mapendekezo hayo kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa; katika sheria hii Serikali inapendekeza kufuta tozo ya miamala kwenye miamala yote ya kielektroniki isipokuwa kwenye miamala ya kielekroniki ya kutoa fedha. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utozaji wa tozo ya muamala mara mbili kwenye muamala mmoja yaani mtumiaji kukatwa na mpokeaji kukatwa. Aidha, mabadiliko hayo yalienda sambamba na kuongeza kiwango cha tozo wakati wa kutoa kwa asilimia 50. Baada ya mashauriano Kamati ilikubaliana na pendekezo la Serikali la kuondoa tozo kwenye miamala yote na viwango vya kutoa vitabaki kama vilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Mafuta; Kamati imefanya uchambuzi wa pendekezo la Serikali kuongeza kiwango cha shilingi 100 kwenye mafuta ya petroli na dizeli kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati. Ongezeko hilo halitakuwa na athari hasi kwenye bei ya mafuta kwa sababu Kamati imejiridhisha kwamba mwenendo wa bei za mafuta kwenye soko la dunia zitashuka kwa kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2023. Hivyo, Kamati inaunga mkono pendekezo hili ambalo litaenda

kupunguza utegemezi wa mikopo na fedha kutoka nje katika kutekeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati. Kamati inapendekeza kiasi hicho cha fedha kitumike katika matumizi yaliyokusudiwa na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi; Serikali Kamati inafanya marekebisho katika Sheria hii yenye lengo la kupunguza kiwango cha tozo ya ufundi kutoka asilimia 0.5 kutoka asilimia nne na kuwa asilimia 3.5, ili kuwapunguzia gharama waajiri. Aidha, mapendekezo haya pia yanaenda kuweka utaratibu maalum wa mgao wa mapato yatokanayo na tozo ya ufundi stadi. Mapendekezo haya pia yanaenda kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya fedha baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya elimu kutoa hati ya msamaha wa tozo ya ufundi stadi baada ya kujiridhisha kuwa msamaha husika ni kwa maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, Sheria ambazo Kamati ilifanya Marekebisho; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha kalenda ya kodi ambayo inaenda kubadilisha utaratibu wa awali wa kubadili viwango vya ushuru wa bidhaa kila mwaka. Hatua hii inaenda kuifanya nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika, kuweka mazingira bora ya uwekezaji na hivyo kuvutia uwekezaji. Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kuwa na sera hii ambayo kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara sera hii inatekelezwa nchini Msumbiji na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyohitaji maelezo ya kina kutoka kwa Serikali ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuanzisha utaratibu wa kutoza shilingi 20 kwa kila kilo ya saruji sawa na shilingi 1,000 kwa mfuko wa kilo 50.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuanzisha tozo ya shilingi 20 kwa kila kilo ya saruji kwa saruji zinazozalishwa ndani na zile zinazoagizwa kutoka nje. Ongezeko hili ni sawa na shilingi 1,000 kwa mfuko wa saruji wa kilo 50. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba, uzalishaji wa saruji nchini kwa mwaka 2022 ulikuwa ni tani milioni 7.6 sawa na kilo bilioni 7.6. Hivyo mapato

yanayotarajiwa kwa chanzo hiki ni shilingi bilioni 151.96 kwa mwaka kwa kutumia takwimu za uzalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na hoja zifuatazo ambazo zilihitaji majibu ya Serikali:-

(i) Uwezo wa Serikali kudhibiti bei ya saruji isipande zaidi ya kiwango kitachoongezwa.

(ii) Mtumiaji wa saruji mkubwa ni Serikali na hivyo itaongeza gharama za miradi.

(iii) Kuna uwezekano mauzo ya bidhaa hii kwenda nje yakashuka endapo bei ya saruji inayozalishwa nchini itakuwa aghali ukilinganisha na bei ya saruji inayozalishwa nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa saruji wa ndani na mapato yanayotarajiwa ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Taarifa yetu, na ninaomba Taarifa yetu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa baada ya mashauriano Kamati ilikubaliana na pendekezo la Serikali kwa kuongeza shilingi 20 kwenye kila kilo ya saruji kwa saruji inayozalishwa nchini. Aidha, kwa saruji inayoagizwa kutoka nje, Kamati ilipendekeza zitozwe shilingi 30 kwa kila kilo ya saruji. Lengo ni kuhakikisha kunakuwa na ushindani ulio sawa. Hivi sasa Tanzania inaagiza tani 566.8 kwa mwaka sawa na kilo milioni 566.8. Pamoja na makubaliano hayo, Serikali imeahidi kukutana na wazalishaji wa ndani na kuweka mkakati wa kutopandisha bei zaidi ya ongezeko la shilingi 1,000 kwa mfuko wa saruji.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa bidhaa wa asilimia 20 kwenye bidhaa za bia zinazozalishwa nchini kwa kutumia asilimia 100 ya shairi inayozalishwa ndani; Kamati iliishauri Serikali kutokupandisha ushuru wa bidhaa kwa bia zinazozalishwa hapa nchini kwa kutumia asilimia 100 ya kimea kinachozalishwa ndani. Hatua hii itawezesha kuendelea na uwekezaji wa kiwanda cha bia kilichopo Moshi, Mkoani Kilimanjaro. Serikali imekubaliana na

ushauri wa Kamati kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41; katika sheria hii Kamati ilishauri masuala yafuatayo na Serikali iliridhia. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu ushiriki wa Watanzania katika Michezo ya Kubahatisha; Serikali inapendekeza kuweka takwa la kisheria kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania kutoa leseni za michezo ya kubahatisha kwa Kampuni ambayo angalau asilimia 25 ya hisa zake zinamilikiwa na Watanzania. Kamati ilipendekeza kiwango cha asilimia tano badala ya asilimia 25 kwani kiwango hiki kingeleta ugumu katika utekelezaji wake na hivyo kuathiri uwekezaji na ukuaji wa sekta hii. Baada ya mashauriano, Serikali ilikubali kushusha kiwango hicho hadi asilimia tano kama inavyonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

Pili, kiwango kinachotozwa kwenye mapato ya Michezo ya Kubahatisha; Serikali ilipendekeza kupunguza kiwango cha kodi kutoka asilimia 25 hadi asilimia 18 kwenye mapato ghafi ya michezo ya kubahatisha kwenye maeneo ya uendeshaji wa mashine arobaini za sloti. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kuendelea na kiwango kilichopo hivi sasa kutokana na uraibu unaosababishwa na michezo hiyo. Baada ya majadiliano Serikali ilikubali pendekezo la Kamati kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332; Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanya mabadiliko kwenye sheria hii yanayolenga maeneo yafuatayo:-

i. Kupunguza viwango vya kodi kwa walipa kodi wasiolazimika kutunza mahesabu waliopo katika sekta ya usafirishaji.

ii. Kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji kwa mabadiliko yanayofanyika ndani ya kampuni kwa kuuziana hisa baina ya kampuni za wakazi.

iii. Kusamehe kodi ya mapato kwenye uwekezaji unaotokana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

iv. Kutoza kodi ya zuio ya asilimia mbili kwa wachimbaji wadogo wa madini wasiotunza hesabu kuepusha usumbufu kwa sababu kodi hiyo itakuwa ya mwisho na itawahusu wachimbaji wadogo.

v. Kupunguza kodi ya ongezeko la mtaji kutoka asilimia 10 hadi asilimia tatu kwa wauzaji wa ardhi na nyumba wasiotunza kumbukumbu za gharama za kuendeleza ardhi.

vi. Kujumuisha malipo ya huduma za kielektroniki kwenye malipo yenye vyanzo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuwezesha utozaji wa huduma za kidijitali zinazotolewa kupitia soko la mtandao.

vii. Kufuta wajibu kwa watu binafsi kukata kodi ya zuio kwenye upangishaji wa nyumba ili kuwaondolea adha wapangaji ambao sio wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi, Sura 113; Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali ya mabadiliko ya sheria hii yenye lengo la mapato yote yanayokusanywa kwenye chanzo cha kodi ya pango la ardhi kuwekwa katika akaunti ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu wa ukusanyaji na urejeshwaji wa mapato yaliyotokana na chanzo hichi utakubaliwa kati ya Waziri wa Ardhi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kifungu hiki kimefanyiwa mabadiliko kwenye jedwali la mabadiliko la Serikali ili kuakisi mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289; katika sheria hii Serikali inapendekeza kufanya maboresho yafuatayo:-

i. Kutambua maeneo yote ya Wilaya katika utozaji wa kodi ya majengo ili yajumuishwe katika ulipaji na ukusanyaji kodi ya majengo isipokuwa majengo

yaliyosamehewa katika sheria ambayo ni pamoja na nyumba za tope, fito, tembe, nyasi na nyumba zinazofanana na hizo kwa ajili ya makazi. Hatua hii inaenda kuweka usawa pamoja na kuongeza wigo.

ii. Kuongeza kodi ya majengo kwa mwaka kutoka shilingi 12,000 hadi shilingi 18,000 kwenye majengo yasiyo ya ghorofa na kutoka shilingi 60,000 hadi shilingi 90,000 kwa kila sakafu ya ghorofa. Marekebisho yanafanyika katika kifungu hicho ili kuwezesha asilimia 20 ya mapato kurejeshwa katika Halmashauri ili kuziwezesha katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi hizo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mabadiliko haya utaanza tarehe 1 Januari, 2024 ambapo Halmashauri nchini zitaanza kutekeleza jukumu la kukusanya kodi hii ya majengo kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Aidha, mabadiliko hayo ni kutokana na Takwimu za Sensa ambazo zilionyesha majengo takribani milioni tano hayako kwenye wigo wa kodi hii.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290; Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali la kuwezesha kampuni zenye leseni za huduma za fedha mtandaoni kulipa ushuru wa huduma kwenye Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo itagawanya mapato yatokanayo na ushuru huo kwenye kila Halmashauri, ushuru wa huduma badala ya utaratibu uliopo sasa ambapo kampuni hizo hupaswa kulipa kwenye kila Halmashauri kulingana na shughuli za kampuni katika Halmashauri husika. Hii ni hatua njema iliyoamriwa na Serikali ambayo inaenda kuwapunguzia adha wafanyabiashara, kupunguza gharama za uwajibikaji kwa kampuni husika na pia kupunguza gharama za ufuatiliaji wa tozo hiyo kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta usawa Kamati ilishauri takwa hili la kisheria pia lijumuishe kampuni nyingine tofauti na zile za huduma za fedha mtandaoni. Mfano kampuni za mafuta, utalii na usafirishaji yenye shughuli katika Halmashauri zaidi ya moja. Hivyo basi, Kamati inashauri kifungu hiki kimpe mamlaka Waziri mwenye dhamana kuruhusu kampuni ambazo zinaendesha shughuli zake zaidi ya Halmashuri moja kulipa gharama za huduma kwa pamoja

kwenye Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo itagawanya makusanyo yatokanayo na tozo hiyo kwenye kila Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano na Serikali, Serikali iliridhia pendekezo la Kamati na kuahidi kulifanyia kazi. Hatua hii italeta matokeo chanya nchini na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara. Maeneo mengine yaliyofanyiwa maboresho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho la Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali katika sheria hii inaenda kuhamisha jukumu la kukusanya ada ya mabango kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenda Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Kamati inaipongeza Serikali kwa maamuzi haya ambayo yanalenga kuongeza ufanisi kati ukusanyaji wa ada ya mabango kwa kutumia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo muundo wake wa kiutawala umefika hadi ngazi za kata, vijiji na mitaa, hivyo kurahisisha masuala ya ufuatiliaji na usimamizi. Itakumbukwa kuwa jukumu hili awali lilifanywa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kabla kuhamishiwa *TRA* mwaka 2016 na lilikuwa linafanywa kwa ufanisi ukilinganisha na ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438; katika Sheria hii Serikali inapendekeza kufanya maboresho mbalimbali ambayo Kamati ilikubaliana nayo. Maboresho hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Kuboresha tafsiri ya msamiati "*primary data server*" ili kujumuisha *server* mtandao au aina yoyote ya kifaa maalum kwa lengo la kuhifadhia taarifa za kielektroniki za mlipakodi hapa nchini. Marekebisho haya yana lengo la kutambua aina nyingine za *server* zinazoweza kutumika na mlipakodi kwa ajili ya kuhifadhi taarifa, kupunguza gharama za usimikaji wa *server* na kurahisisha utoaji wa taarifa pindi zinapohitajika. Vilevile inapendekezwa kuongeza muda unaohitajika kutekeleza takwa hili la kisheria ambapo muda umeongezwa hadi tarehe 1 Januari, 2024 ili kuwapa

walipakodi muda wa ziada wa kukamilisha maandalizi kabla ya kuanza kutekeleza takwa hili la kisheria.

ii. Kuruhusu utoaji wa risiti kwa vifaa au teknolojia nyingine mbali na mashine za kielektroniki za kutolea risiti ili kutambua matumizi ya vifaa au teknolojia nyingine zinazotumika kutoa risiti za kielektroniki mbali na mashine za *EFD*.

iii. Kuweka muda wa uwasilishwaji wa taarifa za mikataba ya ukandarasi ya ujenzi na uchimbaji kwa Kamishna Mkuu ili kuongeza uwajibikaji wa mlipa kodi na kuboresha usimamizi wa kodi.

iv. Kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yanayotumika katika kifungu hicho kama vile sehemu za kuhifadhia mizigo, ili kuondoa mkanganyiko uliopo na kurahisisha usimamizi.

v. Kuwapunguzia adhabu wanunuzi kwa kutodai risiti na kuweka adhabu kwa wauzaji wasiotoa risiti ya kielektroniki kwa kuangalia thamani ya mzigo waliouza.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yalijadiliwa kwa kina katika sheria hii ni mapendekezo ya kutoa tafsiri ya maneno "*storage facility*" na "*store owner*". Kamati imebaini kwamba tafsiri ya maneno hayo inaenda kuondoa mkanganyiko uliojitokeza katika utekelezaji wa usimamizi wa maeneo ya kuhifadhia mizigo uliojitokeza awali. Hivyo, Kamati inasisitiza kwamba kanuni zitakazotungwa ziende sambamba na maudhui yaliyopo kwenye tafsiri ya maneno hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148; mabadiliko yaliyofanyika katika sheria hii yana malengo yafuatayo:-

i. Kuoanisha *HS Code*s zilizopo katika kiambatisho cha kwanza cha Protokali ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

ii. Kutoa misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyumba zenye thamani chini ya shilingi milioni 50.

iii. Kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vinavyotumika katika kubadili mfumo wa gari kutoka mfumo wa mafuta kwenda kwenye mfumo wa kutumia gesi asilia iliyogandamizwa au mfumo wa umeme.

iv. Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha 0% kwenye mbolea inayozalishwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa lengo la kuleta unafuu wa bei ya mbolea kwa wakulima.

v. Kuruhusu ahirisho la kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa za mitaji zilizozalishwa nchini na kusitisha utaratibu wa kutoa ahirisho la kodi kwa bidhaa za mitaji zinazoingizwa kutoka nje ya nchi baada ya miaka mitatu.

vi. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye uuzaji na ukodishaji wa ndege, *engine* za ndege na vifaa vyake ili kuleta unafuu kwa waendeshaji wa shughuli za usafiri wa anga kwa kuwawezesha kununua bidhaa husika nchini au kuagiza kutoka nje ya nchi na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta ya anga na utalii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano na Serikali Kamati ilikubaliana na Serikali kufanya maboresho katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kujumuisha matengenezo ya ndege kwenye msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani;

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye hema za chuma zinazotengenezwa nchini;

(iii) Kufuta marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za *software* za *gaming* na *gaming odds;* na

(iv) Kurekebisha kifungu cha 6 ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi za kutengenezea vifungashio vya madawa. Vilevile, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye hema za chuma zitakazoagizwa kutoka nje ya nchi na wafugaji wa kuku.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sheria nyingine zilizofanyiwa maboresho; Sheria ya Usalama wa Chakula Sura ya 249. Marekebisho yanayopendekezwa kwenye sheria hii yanakusudia kudhibiti uagizaji na usafirishaji nje ya nchi wa mazao ya ngano, shayiri, mchuzi wa zabibu na mafuta ghafi ya kula. Lengo la maboresho hayo ni kuhakikisha kwamba mazao ya wakulima yanayozalishwa ndani ya nchi yanapata masoko ya uhakika. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura ya 399; Serikali inapendekeza kuboresha kifungu cha 23A cha Sheria hiyo kwa lengo la kuiruhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoza na kukusanya ada kwenye programu, machapisho, semina, huduma za ushauri na huduma nyingine ambazo zitatolewa na mamlaka hiyo. Lengo la mabadiliko haya ni kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato kwenye Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla; misamaha ya kodi. Kamati inaunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali kama vile utoaji wa misamaha ya kodi kwa nia ya kuchochea shughuli za kiuchumi nchini na kupunguza gharama kwa wananchi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya misamaha inayotolewa ili kuona endapo imeleta matokeo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, tathmini hii itaisaidia Serikali kujua ni kwa kiasi gani misamaha inayotolewa inachangia katika ukuaji wa uchumi na kama kuna haja ya misamaha hiyo kuendelea kuwepo, kuongezewa muda ama kusitishwa au kuboreshwa. Hivyo, Kamati inapendekeza kufanyika kwa tathmini ya misamaha ya kodi yote na kujua ufanisi wake.

Mheshimiwa Spika, Marejesho ya Kodi *(VAT Refunds);* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuboresha misingi ya utoaji haki katika usimamizi wa kodi ikiwa ni pamoja na kuweka muda wa upokeaji na utoaji wa marejesho ya mapingamizi ya kodi. Aidha, Kamati inashauri maboresho haya yaende sambamba na urejeshaji wa kodi kwa wakati pale tu maamuzi yanapokuwa yamefanyika ili kuwaondolea adha wafanyabiashara kusubiri marejesho kwa muda mrefu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kusimamia vyema utekelezaji wa kifungu cha 84 kifungu kidogo cha 3 kipengele A cha Sheria ya Kodi la Ongezeko ya Thamani, Sura 148 ambacho kinaelekeza marejesho yafanyike ndani ya siku 90.

Mheshimiwa Spika, uwasilishaji wa Muswada wa Sheria ya Fedha kila mwaka Bungeni; Muswada wa Sheria ya Fedha ni muswada unaowasilishwa Bungeni kila mwaka na hauwasilishwi kwa Hati ya Dharura. Muswada huu ni muhimu kwa maslahi ya Taifa na kwa mujibu wa Ibara ya 138 ya Katiba. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Muswada unawasilishwa Bungeni mapema zaidi walau mwezi mmoja kabla haujapitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukushukuru wewe, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, kwa miongozo yenu na uendeshaji wa vikao vya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango; Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango; Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na Ndugu Onerius Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, kwa ushirikiano wao

walioutoa kwa Kamati wakati wote wa uchambuzi wa muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dkt. Natu Mwamba; Ndugu Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Ndugu Elijah Mwandumbya, Kamishna wa Sera na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Kamati pia inawashukuru wadau wote kwa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa umakini na ushirikiano wao katika kuchambua Muswada huu na kuweza kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba kuwatambua Wajumbe na majina yao yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba nimshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndugu Michael Kadebe, akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati pamoja na Wanasheria wa Ofisi ya Bunge, kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2023 *(THE FINANCE BILL, 2023)* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa

maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** utakumbuka kwamba tarehe 20 Juni, 2023 uliuelekeza Muswada huo kuletwa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa ajili ya kuufanyia kazi na kutoa maoni yake Bungeni. Aidha, kama zilivyo Kanuni za Bunge, Muswada huo uliwasilishwa rasmi kwenye Kamati tarehe 20 Juni, 2023 kwa niaba ya Serikali na Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb).

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho mbalimbali yenye lengo la kurekebisha mfumo wa kodi, viwango vya kodi, ada na tozo chini ya Sheria mbalimbali pamoja na kuboresha utaratibu wa ukusanyaji na usimamizi wa mapato ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yalihitaji maboresho. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 Kamati ilifanya Mkutano na Wadau *(Public Hearing)* kwa siku 2 tarehe 22 na 23 Juni, 2023 ili kupokea maoni yao kwa lengo la kuboresha Muswada huo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba niwatambue Wadau waliofika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa maoni ambao ni: Chama cha Wawindaji wa Kitalii (TAHOA), Chama cha Wazalishaji wa Chumvi (TASPA), Chama cha Mabenki Tanzania (TBA), Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Tanzania (FEMATA), Chama cha Waendesha Michezo ya Kubahatisha (TSBA), Kampuni ya Saruji ya Mbeya (Mbeya Cement), Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI), Kampuni za Bia za TBL na Serengeti (SBL), Kampuni ya Asas Dairies, Kampuni ya Madini ya Barrick, Shirikisho la Wachimba Madini (Tanzania Chamber of Mines), Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC). Aidha, Kamati ilipata fursa ya kukutana na Mawaziri kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Elimu. Aidha, Kamati ilikutana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Muandishi wa Sheria, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha na Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA).

## 2.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2023

### 2.1. Sheria zinazofanyiwa Mabadiliko

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unafanya mabadiliko katika Sheria 18 zifuatazo: -

i) Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki SURA 218;
ii) Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306;
iii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;
iv) Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196;
v) Sheria ya Ushuru wa Magari ya Kigeni, SURA 84;
vi) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41;
vii) Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;
viii) Sheria ya Ardhi, SURA 113;
ix) Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289;
x) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, SURA 290;
xi) Sheria ya Madini, SURA 123;
xii) Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, SURA 437;
xiii) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220;
xiv) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;
xv) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;
xvi) Sheria ya Usalama wa Chakula, SURA 249;
xvii) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, SURA 399;na
xviii) Sheria ya Mafunzo na Ufundi Stadi, SURA 82.

### 2.2. Malengo ya Mabadiliko

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unafanya mabadiliko katika Sheria hizo kwa malengo makuu yafuatayo :-

i. Kupanua wigo wa kodi kwa kuanza kutoza kodi kwa baadhi ya bidhaa na huduma ambazo zilikuwa hazitozwi;
ii. Kuongeza uwajibikaji wa mlipa kodi;
iii. Kuongeza mauzo ya bidhaa nje;
iv. Kuchachua shughuli za uzalishaji mali ndani ya nchi;
v. Kuweka usawa wa utozaji kodi pamoja na kulinda maslahi ya nchi;
vi. Kuimarisha usimamizi wa hakimiliki katika kazi za ubunifu;

vii. Kuchochea matumizi ya kielektroniki;
viii. Kufuta kodi na tozo zinazoonekana kuwa kero;
ix. Kuboresha usimamizi wa kodi pamoja na kuondoa mianya ya ukwepaji wa Kodi;
x. Kuchochea ukuaji wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na kuvilinda viwanda vya ndani; na
xi. Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (Blueprint).

**2.3. Mabadiliko ya Sheria ambayo Kamati imekubaliana na Mapendekezo ya Serikali.**

**i.Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, SURA 218**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii inapendekeza kuongeza bidhaa zinazotumika kuhamishia, kutunzia, kudurufu na kusambaza bidhaa na huduma za sanaa zinazoingizwa nchini kutozwa tozo ya **asilimia 1.5** ya thamani. Hatua hii ina lengo la kupanua wigo wa kodi na kuweka usawa katika utozaji ili kuendeleza na kulinda Sekta ya Michezo na Burudani.

**ii. Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufuta tozo kwa kila laini ya simu na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji. Hatua hii imetokana na ukweli kwamba kifungu hiki kimeshindwa kutekelezeka kwa sababu ya kuongezeka kwa matumizi ya kielektroniki.

**iii. Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196**

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya Sheria hii yanalenga kusamehe **asilimia 80** ya tozo kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa na wawekezaji waliopo kwenye Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZ) kwenda nje ya nchi. Hatua hii ina lengo la kuchochea mauzo ya ngozi mbichi nje ya nchi na hivyo kuongeza fedha za kigeni. Aidha, mapendekezo haya yanalenga wachakataji wa nyama walio maeneo ya EPZ kwa ajili ya mauzo nje ya nchi katika maeneo ya EPZ.

**iv. Sheria ya Ushuru wa Magari, SURA 84**

**Mheshimiwa Spika,** katika sheria hii mabadiliko yanalenga kutoza ushuru wa magari ya nje ya nchi sawa na viwango vya ukanda

wa EAC, SADC na COMESA. Endapo viwango vitakavyotozwa katika nchi zilizopo katika Kanda hizo utakuwa mkubwa kuliko ule unaotozwa nchini basi viwango vinavyotozwa katika nchi hiyo vitatumika pia nchini (*reciprocity*). Pendekezo hili lilitolewa na Kamati ya Bajeti katika Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka wa fedha 2022 wakati Kamati inawasilisha taarifa yake kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi ule ule wa *reciprocity*, Kamati bado inaendelea kushauri Serikali kuanzisha tozo nyingine zinazotozwa na nchi nyingine kwa magari ya nje ya nchi kama vile *Park Fee*, *Carbon emmision fee* na*Toll gate*. Vyanzo hivi vinaweza kuongeza wigo wa mapato ya Serikali kwa sababu nchi nyingine za jirani hutoza tozo hizo kwa magari ya Tanzania yanapotumia barabara zao.

**v. Sheria ya Madini, SURA 123**

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya Serikali yanalenga kusamehe ada ya ukaguzi ya **asilimia 1** katika vituo vya kusafishia madini *(refineries)*. Hatua hii itaenda kuchochea kasi ya ukuaji wa Sekta ndogo ya usafishaji wa madini nchini na kuvutia uwekezaji. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kupunguza mrahaba kwenye madini ya chumvi kutoka **asilimia 3** hadi **asilimia 1** kutokana na ukweli kwamba chumvi ni madini lakini pia ni chakula, hivyo si sawa kutozwa sawa sawa na madini mengine**.** Serikali ilikubali mapendekezo hayo kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho la Serikali.

**vi. Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, SURA ya 437**

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Serikali inapendekeza kufuta tozo ya miamala kwenye miamala yote ya kielektroniki isipokuwa kwenye miamala ya kielekroniki ya kutoa fedha. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utozaji wa tozo ya muamala mara mbili kwenye muamala mmoja, yaani mtumiaji kukatwa na mpokeaji kukatwa. Aidha, mabadiliko hayo yalienda sambamba na kuongeza kiwango cha tozo wakati wa kutoa kwa **asilimia 50.**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya mashauriano Kamati ilikubaliana na pendekezo la Serikali la kuondoa tozo kwenye miamala yote na viwango vya kutoa vitabaki kama vilivyo hivi sasa.

**vii. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa pendekezo la Serikali kuongeza kiwango cha **shilingi 100** kwenye mafuta ya petroli na dizeli kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati. Ongezeko hilo halitakuwa na athari hasi kwenye bei ya mafuta kwa sababu Kamati imejiridhisha kwamba mwenendo wa bei za mafuta kwenye soko la Dunia zitashuka kwa kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2023. Hivyo, Kamati inaunga mkono pendekezo hili ambalo litaenda kupunguza utegemezi wa mikopo na fedha kutoka nje katika kutekeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati. Kamati inapendekeza kiasi hicho cha fedha kitumike katika matumizi yaliyokusudiwa na si vinginevyo.

**viii. Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, SURA 82**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inafanya marekebisho katika Sheria hii yenye lengo la kupunguza kiwango cha tozo ya ufundi stadi kwa **asilimia 0.5** kutoka **asilimia 4** na kuwa **asilimia 3.5** ili kuwapunguzia gharama waajiri. Aidha, mapendekezo haya pia yanaenda kuweka utaratibu maalum wa mgao wa mapato yatokanayo na tozo ya ufundi stadi. Mapendekezo haya pia yanaenda kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na fedha baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana na elimu kutoa hati ya msamaha wa tozo ya ufundi stadi baada ya kujiridhisha kuwa msamaha husika ni kwa maslahi ya Umma.

**3.0. Sheria Ambazo Kamati Ilifanya Marekebisho**

**3.1. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha kalenda ya kodi ambayo inaenda kubadilisha utaratibu wa awali wa kubadili viwango vya ushuru wa bidhaa kila mwaka. Hatua hii inaenda kuifanya nchi kuwa na Sera za kodi zinazotabirika, kuweka mazingira bora ya uwekezaji na hivyo kuvutia uwekezaji. Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kuwa na Sera hii ambayo kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara sera hii inatekelezwa nchini Msumbiji na Afrika ya Kusini.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo yaliyohitaji maelezo ya kina kutoka kwa Serikali ni yafuatayo: -

a) **Kuanzisha utaratibu wa kutoza Shilingi 20 kwa kila kilo ya saruji sawa na shilingi 1000 kwa mfuko wa Kilo 50**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inakusudia kuanzisha tozo ya **Shilingi 20** kwa kila kilo ya saruji kwa saruji zinazozalishwa ndani na zile zinazoagizwa kutoka nje**.** Ongezeko hili ni sawa na **Shilingi 1000** kwa mfuko wa saruji wa **Kilo 50.** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba uzalishaji wa saruji nchini kwa mwaka 2022 ulikuwa **Tani milioni 7.6** sawa na kilo **bilioni 7.6.** Hivyo, mapato yanayotarajiwa kwa chanzo hiki ni **shilingi bilioni 151.96** kwa mwaka kwa kutumia takwimu za uzalishaji wa ndani. Kamati ilikuwa na hoja zifuatazo ambazo zilihitaji majibu ya Serikali:-

i. Uwezo wa Serikali kudhibiti bei ya saruji isipande zaidi ya kiwango kitachoongezwa;

ii. Mtumiaji wa saruji mkubwa ni Serikali na hivyo itaongeza gharama za miradi; na

iii. Kuna uwezekano mauzo ya bidhaa hii kwenda nje yakashuka endapo bei ya saruji inayozalishwa nchini itakuwa aghali ukilinganisha na bei ya saruji inayozalishwa nchi za jirani.

**Uzalishaji wa Saruji ya Ndani na Mapato yanayotarajiwa**

| SARUJI | TANI | KG | MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| Kutoka Nje | 566,826 | 566,826,000 | 11,336,520,000.00 |
| Uuzaji Nje | 632,726 | 632,726,000 | 12,654,520,000.00 |
| Uzalishaji wa Ndani | 7,598,073 | 7,598,073,000 | 151,961,460,000.00 |
| Matumizi | 7,532,173 | 7,532,173,000 | 150,643,460,000.00 |

**Chanzo:*Wizara ya Fedha na Mipango***

**Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano Kamati ilikubaliana na pendekezo la Serikali kwa kuongeza **shilingi 20** kwenye kila kilo ya saruji kwa saruji inayozalishwa ndani. Aidha, kwa saruji inayoagizwa kutoka nje, Kamati ilipendekeza zitozwe **shilingi 30** kwa kila kilo ya saruji. Lengo ni kuhakikisha kunakuwa na ushindani ulio sawa. Hivi sasa Tanzania inaagiza **Tani 566,826** kwa mwaka sawa na **Kilo milioni 566.8**. Pamoja na makubaliano hayo, Serikali imeahidi kukutana na wazalishaji wa ndani na kuweka mkakati

wa kutopandisha bei zaidi ya ongezeko la **shilingi 1000** kwa mfuko wa saruji.

b) **Ushuru wa bidhaa wa asilimia 20 kwenye bidhaa za bia zinazozalishwa nchini kwa kutumia asilimia 100 ya shairi inayozalishwa ndani**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kutokupandisha ushuru wa bidhaa kwa bia zinazozalishwa hapa nchini kwa kutumia **asilimia 100** ya kimea kinachozalishwa ndani. Hatua hii itawezesha kuendelea na uwekezaji wa kiwanda cha bia kilichopo Moshi, Mkoani Kilimanjaro. Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho.

**3.2. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41**

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Kamati ilishauri masuala yafuatayo na Serikali iliridhia. Maeneo hayo ni:-

i. **Ushiriki wa Watanzania Katika Michezo ya Kubahatisha**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kuweka takwa la kisheria kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania kutoa leseni za michezo ya kubahatisha kwa Kampuni ambayo angalau **asilimia 25** ya hisa zake inamilikiwa na watanzania. Kamati ilipendekeza kiwango cha **asilimia 5** badala ya **asilimia 25** kwani kiwango hiki kingeleta ugumu katika utekelezaji wake na hivyo kuathiri uwekezaji na ukuaji wa Sekta hii**.** Baada ya mashauriano, Serikali ilikubali kushusha kiwango hicho hadi **asilimia 5** kama inavyonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

**ii. Kiwango kinachotozwa kwenye mapato ya Michezo ya Kubahatisha (*Forty Machine*)**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipendekeza kupunguza kiwango cha kodi kutoka **asilimia 25** hadi **asilimia 18** kwenye mapato ghafi ya michezo ya kubahatisha kwenye maeneo ya uendeshaji wa mashine arobaini za sloti. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kuendelea na kiwango kilichopo hivi sasa kutokana na uraibu unaosababishwa na michezo hiyo. Baada ya majadiliano Serikali ilikubali pendekezo la Kamati kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

### 3.3. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya mabadiliko kwenye Sheria hii yanayolenga maeneo yafuatayo: -

i. Kupunguza viwango vya kodi kwa walipa kodi wasiolazimika kutunza mahesabu waliopo katika Sekta ya usafirishaji;

ii. Kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji kwa mabadiliko yanayofanyika ndani ya kampuni kwa kuuziana hisa baina ya Kampuni za wakazi;

iii. Kusamehe kodi ya mapato kwenye uwekezaji unaotokana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF);

iv. Kutoza kodi ya zuio ya **asilimia 2** kwa wachimbaji wadogo wa madini wasiotunza hesabu kuepusha usumbufu kwa sababu kodi hiyo itakuwa ya mwisho na itawahusu wachimbaji wadogo;

v. Kupunguza kodi ya ongezeko la mtaji kutoka **asilimia 10** hadi **asilimia 3** *(Capital gains)* kwa wauzaji wa ardhi na nyumba wasiotunza kumbukumbu za gharama za kuendeleza ardhi;

vi. Kujumuisha malipo ya huduma za kielektroniki kwenye malipo yenye vyanzo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuwezesha utozaji wa huduma za kidijitali zinazotolewa kupitia soko mtandao; na

vii. Kufuta wajibu kwa watu binafsi kukata kodi ya zuio kwenye upangishaji wa nyumba ili kuwaondolea adha wapangaji ambao sio wafanyabiashara.

### 3.4. Sheria ya Ardhi, SURA 113

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali ya mabadiliko ya Sheria hii yenye lengo la mapato yote yatayokusanywa kwenye chanzo cha kodi ya pango la ardhi *(Land Rent)* kuwekwa katika akaunti ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu wa ukusanyaji na urejeshwaji wa mapato yaliyotokana na chanzo hichi utakubaliwa kati ya Waziri wa Ardhi na Waziri wa

Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Kifungu hiki kimefanyiwa mabadiliko kwenye jedwali la mabadiliko la Serikali ili kuakisi mabadiliko hayo.

### 3.5. Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Serikali inapendekeza kufanya maboresho yafuatayo:-

i. Kutambua maeneo yote ya Wilaya katika utozaji wa kodi ya majengo ili yajumuishwe katika ulipaji na ukusanyaji kodi ya majengo isipokuwa majengo yaliyosamehewa katika Sheria ambayo ni pamoja na nyumba za tope, fito, tembe, nyasi na nyumba zinazofanana na hizo kwa ajili ya makazi. Hatua hii inaenda kuweka usawa pamoja na kuongeza wigo; na

ii. Kuongeza kodi ya majengo kwa mwaka kutoka **shilingi 12,000** hadi **shilingi 18,000** kwenye majengo yasiyo ya ghorofa, na kutoka **shilingi 60,000** Kwenda **shilingi 90,000** kwa kila sakafu ya ghorofa. Marekebisho yanafanyika katika kifungu hicho ili kuwezesha **asilimia 20** ya mapato kurejeshwa Halmashauri ili kuziwezesha katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mabadiliko haya utaanza tarehe 1 Januari, 2024 ambapo Halmashauri nchini zitaanza kutekeleza jukumu la kukusanya kodi hii ya majengo kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanzia. Aidha, mabadiliko hayo ni kutokana na Takwimu za Sensa ambazo zilionyesha kuna majengo takribani **milioni 5** hayako kwenye wigo wa kodi hii.

### 3.6. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, SURA 290

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali la kuwezesha Kampuni zenye leseni za huduma za fedha mtandaoni kulipa ushuru wa huduma *(service levy)* kwenye Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambayo itagawanya mapato yatokanayo na ushuru huo kwenye kila Halmashauri ushuru wa huduma badala ya utaratibu uliopo sasa ambapo Kampuni hizo hupaswa kulipa kwenye kila Halmashauri kulingana na shughuli za Kampuni katika Halmashauri husika. Hii ni hatua njema iliyoamriwa na Serikali ambayo inaenda kuwapunguzia adha wafanyabiashara, kupunguza gharama za uwajibikaji kwa Kampuni husika na pia kupunguza gharama za ufuatiliaji wa tozo hiyo kwa Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuleta usawa Kamati ilishauri takwa hili la kisheria pia lijumuishe Kampuni nyingine tofauti na zile za huduma za fedha mtandaoni. Mfano Makampuni ya mafuta, utalii na usafirishaji yenye shughuli katika Halmashauri zaidi ya moja. Hivyo basi, Kamati inashauri kifungu hiki kimpe mamlaka Waziri mwenye dhamana kuruhusu Kampuni ambazo zinaendesha shughuli zake zaidi ya Halmashuri moja kulipa gharama za huduma kwa pamoja kwenye Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambayo itagawanya makusanyo yatokanayo na tozo hiyo kwenye kila Halmashauri husika. Baada ya mashauriano na Serikali, Serikali iliridhia pendekezo la Kamati na kuahidi kulifanyia kazi. Hatua hii italeta matokeo chanya nchi na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara. Maeneo mengine yaliyofanyiwa maboresho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Serikali katika Sheria hii inaenda kuhamisha jukumu la kukusanya ada ya mabango kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenda Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kamati inaipongeza Serikali kwa maamuzi haya yanaenda kuongeza ufanisi kati ukusanyaji wa ada ya mabango kwa kutumia Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambayo muundo wake wa kiutawala umefika hadi ngazi za kata, vijiji na mitaa, hivyo kurahisisha masuala ya ufuatiliaji na usimamizi. Itakumbukwa kuwa jukumu hili awali lilikuwa linafanywa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kabla kuhamishiwa TRA mwaka 2016 na lilikuwa linafanywa kwa ufanisi ukilinganisha na ilivyo hivi sasa.

### 3.7. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Serikali inapendekeza kufanya maboresho mbalimbali ambayo Kamati imekubaliana nayo. Maboresho hayo ni :-

i. Kuboresha tafsiri ya msamiati **"*primary data server*"** ili kujumuisha seva mtandao au aina yoyote ya kifaa maalumu kwa lengo la kuhifadhi taarifa za kielektroniki za mlipa kodi hapa nchini. Marekebisho haya yana lengo la kutambua aina nyingine za seva zinazoweza kutumika na mlipa kodi kwa ajili ya kuhifadhi taarifa, kupunguza gharama za usimikaji wa seva na kurahisisha utoaji wa taarifa pindi zinapohitajika. Vilevile, inapendekezwa kuongeza muda unaohitajika kutekeleza takwa hili la kisheria ambapo muda

umeongezwa hadi tarehe 01 Januari, 2024 ili kuwapa walipakodi muda wa ziada wa kukamilisha maandalizi kabla ya kuanza kutekeleza takwa hili la Sheria;

**ii.** Kuruhusu utoaji wa risiti kwa vifaa au teknolojia nyingine mbali na mashine za kielektroniki za kutolea risiti ili kutambua matumizi ya vifaa au teknolojia nyingine zinazotumika kutoa risiti za kielektroniki mbali na mashine za EFD;

**iii.** Kuweka muda wa uwasilishwaji wa taarifa za mikataba ya ukandarasi ya ujenzi na uchimbaji *(construction and extractive industry)* kwa Kamishna Mkuu ili kuongeza uwajibikaji wa mlipa kodi na kuboresha usimamizi wa kodi;

**iv.** Kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika kifungu hicho kama vilevile sehemu za kuhifadhia mizigo (storage facilities) ili kuondoa mkanganyiko uliopo na kurahisisha usimamizi; na

**v.** Kuwapunguzia adhabu wanunuzi kwa kutodai risiti na kuweka adhabu kwa wauzaji wasiotoa risiti ya kielektroniki kwa kuangalia thamani ya mzigo waliouza.

**Mheshimiwa Spika**, maeneo ambayo yalijadiliwa kwa kina katika Sheria hii ni mapendekezo ya kutoa tafsiri ya maneno ***"Storage facility***" na ***"Store owner*". Kamati imebaini kwamba tafsiri ya maneno hayo inaenda kuondoa mkanganyiko uliojitokeza katika utekelezaji wa usimamizi wa maeneo ya kuhifadhia mizigo uliojitokeza awali. Hivyo, Kamati inasisitiza kwamba kanuni zitakazotungwa ziende sambamba na maudhui yaliyopo kwenye tafsiri ya maneno hayo.

### 3.8. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria hii yana malengo yafuatayo;

i. Kuoanisha *HS codes* zilizopo katika kiambatisho cha kwanza cha Protokali ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022;

ii. Kutoa misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyumba zenye thamani chini ya shilingi milioni 50;

iii. Kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vinavyotumika katika kubadili mfumo wa gari kutoka mfumo wa mafuta kwenda kwenye mfumo wa kutumia gesi asilia iliyogandamizwa *(Compressed Natural Gas – GNG)* au mfumo wa umeme;

iv. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye mbolea inayozalishwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa lengo la kuleta unafuu wa bei ya mbolea kwa wakulima;

v. Kuruhusu ahirisho la kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa za mitaji zilizozalishwa nchini na kusitisha utaratibu wa kutoa ahirisho la kodi kwa bidhaa za mitaji zinazoingizwa kutoka nje ya nchi baada ya miaka mitatu; na

vi. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye uuzaji na ukodishaji wa ndege, injini za ndege na vifaa vyake ili kuleta unafuu kwa waendeshaji wa shughuli za usafiri wa anga kwa kuwawezesha kununua bidhaa husika nchini au kuagiza kutoka nje ya nchi na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta ya anga na utalii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya mashauriano na Serikali Kamati ilikubaliana na Serikali kufanya maboresho katika maeneo yafuatayo;

i. Kujumuisha matengenezo ya ndege kwenye msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani;

ii. Kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye hema za chuma zinazotengenezwa nchini;

iii. Kufuta marekebisho ya Sheria ya kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za “***software za gaming na gaming odds”***; na

iv. Kurekebisha kifungu cha 6 ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye malighafi za kutengenezea vifungashio vya madawa. Vilevile, kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani

kwenye hema za chuma zitakazoagizwa kutoka nje ya nchi na wafugaji wa kuku

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa na Serikali.

## 4.0. SHERIA NYINGINE ZILIZOFANYIWA MABORESHO

### 4.1. Sheria ya Usalama wa Chakula SURA ya 249

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yanayopendekezwa kwenye Sheria hii yanakusudia kudhibiti uagizaji na usafirishaji nje ya nchi wa mazao ya Ngano, Shayiri, Mchuzi wa Zabibu na Mafuta ghafi ya kula. Lengo la maboresho hayo ni kuhakikisha kwamba mazao ya wakulima yanayozalishwa ndani ya nchi yanapata masoko ya uhakika. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii

### 4.2. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania SURA ya 399

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kuboresha kifungu cha 23A cha Sheria hiyo kwa lengo la kuiruhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoza na kukusanya ada kwenye programu, machapisho, semina, huduma za ushauri na huduma nyingine ambazo zitatolewa na Mamlaka hiyo. Lengo la mabadiliko haya ni kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato kwenye Mamlaka ya Mapato.

## 5.0. MAONI YA JUMLA

### 5.1. Misamaha ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali kama vile utoaji wa misamaha ya kodi kwa nia ya kuchochea shughuli za kiuchumi nchini na kupunguza gharama kwa wananchi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya misamaha inayotolewa ili kuona endapo imeleta matokeo yaliyokusudiwa. Tathmini hii itaisaidia Serikali kujua ni kwa kiasi gani misamaha inayotolewa inachangia katika ukuaji wa uchumi na kama kuna haja ya misamaha hiyo kuendelea kuwepo, kuongezewa muda ama kusitishwa au kuboreshwa. Hivyo, Kamati inapendekeza kufanyika kwa tathmini ya misamaha ya kodi yote na kujua ufanisi wake.

### 5.2. Marejesho ya Kodi (*VAT Refunds)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuboresha misingi ya utoaji haki katika usimamizi wa kodi ikiwa ni pamoja na kuweka muda wa upokeaji na utoaji wa marejesho ya mapingamizi ya kodi. Aidha, Kamati inashauri maboresho haya yaende sambamba na urejeshaji wa kodi kwa wakati pale tu maamuzi yanapokuwa yamefanyika ili kuwaondolea adha wafanyabiashara kusubiri marejesho kwa muda mrefu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kusimamia vyema utekelezaji wa kifungu cha 84 kifungu kidogo cha 3 kipengele A cha Sheria ya Kodi la Ongezeko ya Thamani, SURA 148 ambacho kinaelekeza marejesho yafanyike ndani ya **siku 90**.

### 5.3. Uwasilishaji wa Muswada wa Sheria ya Fedha Kila Mwaka Bungeni

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Fedha ni Muswada unaowasilishwa Bungeni kila mwaka na hauwasilishwi kwa Hati ya Dharura. Muswada huu ni muhimu kwa maslahi ya Taifa na kwa mujibu wa Ibara ya 138 ya Katiba, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba muswada unawasilishwa Bungeni mapema zaidi walau mwezi mmoja kabla haujapitishwa na Bunge.

## 6.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mhe. Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa miongozo yenu na uendeshaji wa vikao vya Bunge. Aidha, napenda kuwashukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Jaji. Eliezer Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ndg. Onerius Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati wakati wote wa uchambuzi wa Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Dkt. Natu Mwamba, Ndg. Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ndg. Elijah Mwandumbya Kamishna wa Sera na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania

pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Kamati pia inawashukuru wadau wote kwa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa umakini na ushirikiano wao katika kuchambua Muswada huu na kuweza kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba kuwatambua Wajumbe yao kama ifuatavyo wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Zainab Katimba, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba nimshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati pamoja na Wanasheria wa Ofisi ya Bunge kwa kuipatia

Kamati ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo,
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
26 Juni, 2023

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kutuwasilishia maoni hayo ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, naongeza nusu saa ili tuweze kumalizia ratiba iliyo mbele yetu.

Hoja imeshawasilishwa na Mheshimiwa Waziri, lakini pia Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeeleza yale ambayo Serikali imewasikia na yale ambayo bado wanaendelea kupendekeza, wameeleza.

Hapa, kama ilivyo ada, nimeletewa majina ya Wabunge ambao wanataka kuchangia hoja hii. Hawa Wabunge nitawapa nafasi ya kuchangia halafu nitampa nafasi mtoa hoja aje ahitimishe.

Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Ali Hassan King ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye hoja hii ambayo inahusu Muswada wa Sheria ya Fedha. Mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ile ya Bajeti, na kwa hiyo kilichosomwa na Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Daniel Sillo, ni jambo ambalo naafiki na ni zuri sana, na tulichambua kwa kina sana na ninaamini kwamba watu hawatakuwa na mengi sana ya kusema kwa sababu huu ni Muswada ambao ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, na niseme hivi; kabla sijaenda kwenye Muswada huu kabisa niseme kwamba lazima tuipongeze Wizara ya Fedha na tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kutuletea bajeti miaka hii ya kwake ambazo zimeboreka kwa kuongeza usahihi wake na uhakika wake.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Dunia imetoa vigezo vya kuweza kupima *budget reliability* ambao ni uhakika na usahihi wa bajeti. Na uhakika huu unapimwa kwa kuangalia nakisi inajitokeza katika makusanyo ya mapato ukilinganisha na ile ambayo tulikuwa tumepitisha kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, utaoa kwamba katika mwaka 2017/2018 nakisi ilikuwa asilimia 16 ya mapato tuliokisia kwenye bajeti hayakupatikana. Mwaka uliofuata 2018/2019, nakisi ilikuwa asilimia 11, pungufu ya mapato tuliokusanya ukilinganisha na bajeti ambayo tulitegemea.

Mheshimiwa Spika, utaangalia kwamba baada ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuingia kwenye madaraka, nakisi hiyo ilipungua kutoka asilimia hizo nilizosoma na kufikia asilimia sita tu. Niseme hivi; katika mwaka 2021/2022, sasa ukiwa mwaka ule ambao alishika hatamu kwenye kutengeneza bajeti hii hapakuwa na nakisi, tulikusanya mapato asilimia mbili zaidi ya tulizokadiria kwenye bajeti; hili jambo huwa halitokei sana, kwamba unakusanya zaidi kuliko ulivyokisia. Ninataka tuipongeze sana Wizara kwa sababu ina maana kwamba makisio yao yamekuwa ya uhakika na usahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini pia kwamba muswada huu tunaokwenda kupitisha kuwa Sheria ya Fedha ya mwaka 2023/2024 utakuwa hivyohivyo, kwamba tutaona makisio haya yatapitwa katika ukusanyaji na ina maana kwamba kweli tumeweka mikakati ya kukusanya na viwango vya kodi ambavyo tumeweka viko *realistic* kidogo. Na ninaamini kwamba hiyo itakwenda kutokea na ndiyo sababu tunaunga mkono mapendekezo yaliyoletwa na Wizara baada ya kutoa maoni yetu na wakakubali maoni yale na wakaenda kuyatekeleza kwenye marekebisho waliyoleta.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba tulikuwa tunaimba sana *issue* ya *budget calendar.* Kalenda ya *budget* tulikuwa tunasema ni njia pekee nzuri ya kuweza kumhakikishia mwekezaji kwamba makisio yake ya kweli atakayolipa ndani ya kipindi fulani hayatabadilika badilika. Na naamini kwamba sasa Wizara na Serikali ya Samia Suluhu Hassan imekubali kwamba sasa tuingie kwenye mchakato huo na wameanza sasa kwa vitendo kutengeneza mikakati ya kukusanya kodi ambayo inatupa *predictability* na naamini kwamba hiyo itaweza kuongeza pia wawekezaji ambao wataona ukweli kwamba sisi tunaweza tukakaa miaka mitatu bila kubadilisha badilisha hizi kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ni jambo la busara limefanyika, na tunalishangilia sana kwa sababu ni jambo ambalo Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania pia walikuwa wanalifuatilia sana kwenye Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna vitu kwa mfano ambavyo wamerahisisha, na kodi zilizo rahisi ni zile ambazo zinaeleweka za wale walipa kodi na pia yule mkusanyaji wa ile kodi anaelewa vigezo ambavyo viko *straightforward.* Na hilo ni jambo ambalo limeanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano hili la wachimbaji wadogo wadogo ambao ni vigumu sana wao kutengeneza *accounts* zao, kubadili *statements* zao, na kuweka risiti zao na kuweza kuwasilisha kwenye mamlaka zinazohusika. Wamerahisisha kwa kusema kwamba sasa watalipa tu asilimia mbili wakishalipa hiyo ni mwisho, hawatalipa kitu kingine na Serikali haitawafutailia, na ninaamini kwamba *compliance* itakuwa kubwa na tutaona ongezeko la mapato yetu kutoka kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pia tunaona kwamba kuna bidhaa, na ugumu wa kuanza mchakato wa kutengeneza bajeti kwa kuzingatia *predictability,* ni suala zima la kwamba unapoanza huu mchakato unakuta kwamba miaka mitatu hutaongeza. Kwa hiyo, inakuwa kwamba sasa ili uweze kulinda thamani ya fedha, kulinda thamani ya makusanyo yako, lazima u-*predict* na uweze ku-*fight a lot* sehemu ya hiyo sheria za zamani ya ile ...

itakayofuata katika miaka hiyo. Kwa hiyo, ndiyo sababu utaona kwamba kuna viwango vimeongezeka vikawa juu kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kuna bidhaa ambazo sasa zimeongezeka kwa *excise duty* ambayo itakuwa ni asilimia 20 kwa sababu zilikuwa tu hazijafanyiwa marekebisho kwa miaka mitatu iliyopita. Kwa mfano bia, watu wanazinywa lakini ukweli ni kwamba tulihoji sana lakini baadaye tukaona kwamba kwa sababu miaka hii mitatu inayokuja hawatakuwa na fursa ya kubadilisha hivyo viwango, basi kwa kuanzia kulinda thamani hiyo basi tukubali kwamba *rate,* hicho kiwango kiongezeke kwa staili hiyo ya asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, kuna bia na vinywaji vingine lakini naamini kwamba ni kitu ambacho ni busara na kwamba tuelewe Wabunge wote tunaposimama hapa tunatafuta miradi ya maendeleo na tunapata. Sasa tuelewe pia hiyo inaashiria kwamba ni lazima tukubali pia kodi zikusanywe, kama Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anahimiza, na ziongezwe kodi mpya ili ziweze pia kuchangia katika miradi hiyo ambayo inakwenda kuboresha mazingira ya biashara na mazingira ya uzalishaji katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini hilo ni jambo ambalo pia wananchi watalipokea kwa kuelewa kwamba hatutabadilisha kwa miaka mitatu ijayo lakini pia ni sehemu yetu sisi wananchi kuchangia na maendeleo tunaona nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na utata kidogo kwenye suala zima la bidhaa ya *cement.* Imeongezeka, tumeweka shilingi 1,000 kwa mfuko wa kilo 50. Lakini tumegundua kwamba kusema ukweli sisi bei zetu ziko chini sana ukilinganisha na bei zilizo kwenye masoko ya nchi jirani. Kwa hiyo, pia hiyo tukaona kwamba itakuwa ni vyema kwa sababu kiasi cha fedha ambazo tunatarajia kupata kwenye hicho chanzo ni takribani shilingi bilioni 200, kwa hiyo, ikawa ni vigumu sana kuigusa. Naamini pia kwamba hiyo ni njia moja wapo pia ya kusaidia hii *cement* ichangie, viwanda vichangie kwenye hiyo, na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la tozo za miamala, hii sasa siyo tozo ya miamala lakini tulikuwa tumenuwiya kwenye Muswada wa mwaka jana tuliweka tozo kwenye *airtime usage,* matumizi ya muda wa maongezi kwenye simu. Sasa hiyo imetufurahisha kwamba sababu Mheshimiwa Waziri amefuta hiyo tozo, haitakuwepo. Ilikuwa kwenye sheria, haikuwa *implemented* lakini imefutwa na ninaamini kwamba wananchi watafurahia sasa kwamba tunajua kilichopo kwenye tozo hazitabadilika tena na mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho sijui kwa nini najiskia kukuita Mwenyekiti, kumbe wewe ni Spika mkubwa sana na tunakuombea Mungu akubariki sana kwa sababu hata kule tunakoelekea utakuwa mtu wa kimataifa sana kwa hiyo, unastahili zaidi ya cheo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwamba sheria imejaribu kulinda wasanii wetu ambao wamekuwa wanaibiwa ubunifu wao na watu ambao ni wajanja ambao wanakuja wanachota nyimbo, wanachota maigizo halafu wanapeleka bila kulipa chochote. Kwa hiyo, nashukuru kwamba ili waweze kubana kila mtu anayeweza kufanya kitu hicho asiweze, wameongeza aina ya vifaa ambavyo vitalipiwa ule ushuru wa asilimia 1.5 na hivyo vifaa ni kama vile *compact discs* kama *DVDs* na *CDs* n.k., vimeongezwa pia. Kwa hiyo, sasa tunaweza kubana zaidi watu kuongeza huo mfuko wa kusaidia wasanii wetu ambao wanatupa burudani za kutosha na pia wanatangaza kimataifa.

Mheshimiwa Spika, upande mwingine nimefurahia pia kwamba unajua *excise duty* inalenga zaidi kuzuia au kupunguza uhitaji wa bidhaa fulani, kwa hiyo, hata kwenye sigara ambazo zinaletea watu madhara wameongeza pia sigara aina nyingine, kumbe kuna na *electronic cigars,* kuna shisha, wanaruhusu utumie lakini utalipia.

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Subira Mgalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa asubuhi ya leo kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Fedha wa mwaka huu, 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa namna ambavyo ametuwezesha miezi yote hii minne tangu tumeanza kwenye Kamati mpaka sasa, na leo tumehitimisha kwa kuipigia kura ya kishindo Bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024, asilimia 95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri, na kuwezesha kutuwasilishia Muswada huu wa Fedha. Lakini nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na watendaji wote kwa namna ambavyo mmefanya kazi nzuri kuanzia utayarishaji wa bajeti, uwasilishaji na hatimaye uwasilishaji wa Muswada huu wa Sheria ya Fedha, ili Bunge liwape mamlaka sasa mkakusanye kiwango kinachotakiwa cha trilioni 44.39 na muweze kutumia kiwango hicho kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kipekee nikupongeze wewe binafsi kwa kazi nzuri uliyofanya Bunge lote hili la bajeti, umetuongoza vizuri, ni Spika wa viwango, umetoa maelekezo ya mara kwa mara, na hakika nakutakia kila la heri kwa safari unayoendelea ya kuweza kuchaguliwa kwenye Bunge la dunia kwa sababu unaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono huu hii sheria ambayo umewasilishwa. Sisi kama Kamati ya Bajeti tulipata fursa ya kuwasikiliza wadau mbalimbali. Lakini nataka niseme wadau wote waliokuja kwenye Kamati ya Bajeti kwa namna moja au nyingine, na mara zote, wametanguliza shukrani za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa namna ambavyo imepanga bajeti yake, kwa namna ambavyo inachukua hatua mbalimbali za kikodi, lakini kwa kipekee kwa mazingira wezeshi ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli walitupa wepesi katika kujadili Muswada huu, na kwa usikivu wa Serikali, pale ambao palikuwa na hoja ya maboresho mbalimbali, Serikali hii ilitekeleza na ndiyo maana leo kuna *schedule of amendments. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza ka kusema kwamba kwa kuwa Serikali imejipangia na tumeshaipitisha bajeti ya trilioni 44 na katika hizo trioni zaidi ya 14 ni kwa ajili ya fedha za maendeleo na katika trilioni 14, trilioni 10 zinatokana na mapato ya ndani. Kwa hiyo niko hapa kuunga mkono hatua zote za kikodi. Na kwa kuwa pia tumewasilisha taarifa yetu, yote ambayo ameisoma na taarifa yetu naiunga mkono nampongeza sana Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na majadiliano marefu kwenye Sheria ya ushuru wa barabara na mafuta wa hilo ongezeko la shilingi mia, lakini tulikubali kuiunga mkono Serikali na ninalishawishi Bunge, tuiunge mkono Serikali yetu ya Awamu ya Sita baada ya kuanza kuiona dhamira ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, pale ambapo aliamua Serikali yake itoe ruzuku ili kushusha bei ya mafuta, na takribani bilioni 400 zilitumika. Kwa hiyo tukaona kweli ni dhamira na mazingira ambayo yaliletea lazima Serikali iwatizame Watanzania wake na kuleta ahueni kwenye bei ya mafuta. Pia licha ya bilioni 400 kabla ya ruzuku hiyo ziliondolewa tozo mbalimbali za mamlaka ya udhibiti kwenye sekta hii ya mafuta, zaidi ya bilioni 102.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nachukua fursa hii kuwashawishi Watanzania wenzangu; na kwa kuwa bajeti hii zaidi ya trilioni kumi zinatakiwa zitoke kwenye mapato ya ndani kwenda kwenye miradi ya maendeleo, na kwa kuwa tuna ona kazi inayoendelea na ukiiangalia wimbi hili la bajeti utaona kwa mara ya kwanza, wameaninisha kabisa, Bwawa la Mwalimu Nyerere Trilioni 1 na bilioni 500, SGR trilioni 1 na bilioni mia moja na wameweka ulipaji wa madeni zaidi ya milioni 500.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unaona kabisa fedha zetu za hii kodi, na kwa kuwa wamesema ni kwa ajili ya miradi ya kimkakati, na tunaona kazi inaendelea hakuna kilichosimama,

nimeshawishika kwamba hii tozo iendelee na Kamati tumesisitiza ikatumike kama ilivyokusudiwa kwenye miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya pili ya mfumo wa malipo ya kitaifa Sura 437; nipongeze Serikali kwa kuja na pendekezo la kufuta tozo ya miamala kwenye miamala yote ya ki-*electronic* kasoro ile miamala ya kutoa fedha. Hatua hii ni kubwa itawapunguzia Watanzania gharama. Ilikuwa ukituma gharama, ukitoa gharama kwa hiyo sasa inabaki ni masuala ya kutoa fedha na kwa viwango vile vile. Tunaiona dhamira ya Mheshimiwa Rais lakini tunashukuru tozo hii imefanya mambo makubwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kulikuwa na tozo ya shilingi elfu moja kwenye mfuko wa simenti. Kamati tumejadiliana sana, pamoja na wadau tumewasikia lakini tumeshukuru Serikali imetutaarifu pamoja na Wizara yenyewe ya Viwanda, kazi kubwa waliyofanya ya mazungumzo na wenye viwanda imefanyika; na tukasema sana tunaojenga ni wale wenye vipato vya kati, wenye vipato vya juu na wenye vipato vya chini, lakini tuchukue kodi hii tuchangie maendeleo kwa kuwa kuna hatua mbalimbali zilizopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninasimama hapa kuliunga mkono ni suala zima la kuendelea kutoza kodi ya ongezeko la thamani ya kiwango cha zero kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi. Tumeona licha ya kutoza kiwango cha zero lakini Serikali itaendelea kutoa ruzuku kwenye masuala ya mbolea. Tumeona tija ya ruzuku ya mbolea awamu hii, wakulima wengi wameipata na hasa wanawake wa Tanzania ambao sisi Wabunge wanawake tunawawakilisha.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hii, zaidi ya bilioni 211; tumeona uzalishaji wa mazao mbalimbali ulivyoongezeka na tunaona hatua ambazo zinachukuliwa ili mazao hayo yaweze kupata masoko nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuunga mkono muswada huu wa Sheria na sababu za kuunga mkono na mimi namuunga mkono Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Rais lazima apewe maua yake, tunaona bajeti zake utekelezajio wake, tunaona kwa mara

ya kwanza fedha za maendeleo zinazo enda kwenye maeneo yetu. Tunaona tunavyoendelea sasa hivi mradi wa boost unaendelea zaidi ya bilioni 260, shule za msingi mpya zinajengwa lakini sisi wanawake tunaona huduma za afya. Kwa mara ya kwanza ujenzi wa *ICU* zaidi ya 70 na ngazi ya Wilaya tumepata.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza ujenzi wa wodi za dharula 111 kutoka 5 tu tulizokuwa nazo. Kwa mara ya kwanza ukarabati, uwepo wa vifaa vya *Ct scan* hospitali zetu za Mikoa zaidi ya 30. Kwa hiyo tunaona tija ya bajeti zinazowasilishwa ndani ya Bunge na kazi mbalimbali zinazoendelea. Sisi kama wanawake, wazazi wa vijana watakaoenda vyuo vya kati ambako Serikali inaenda kutoa mikopo. Kwa vijana watakao chaguliwa kutoka *form four* kenda vyuo vingine ambako Serikali imefuta ada. Tunayo sababu ya kuunga mkono Muswada huu na Mheshimiwa Rais tunakutakia kila la kheri. Tunakuunga mkono, tunakupenda na tunakupongeza sana. Umeonesha uongozi madhubuti na unaweza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kuna wageni ambao nimeambiwa wako humu ndani. Wageni wa Mheshimiwa Jerry Silaa, nimeambiwa yupo Dkt. Samwel Njoka ambaye ni Mwenyekiti wa *Neema Gospel Choir*, lakini yupo Dkt. Baraka Makaya ambaye ni Makamu Mwenyekiti, pia yupo Mariam Protas ambaye ni Afisa Uhusiano. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Jerry Silaa wanatoka *Neema Gospel Choir*. Na Mheshimiwa Jerry Silaa ameleta taarifa ya ziada hapa anasema viongozi hawa wa hii *Neema Gospel Choir*, Kwaya yao inajiandaa kufanya tukio moja kwa ajili ya kuchangia huduma za kijamii, litafanyika tarehe 22 Julai  Ukumbi wa *The Super Don* Masaki Dar es Salaam. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, mnakaribishwa huko mkachangie huduma za kijamii kupitia nyimbo za injili, ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilisha mtaja Mheshimiwa Alli Hassan King, mtoa hoja ajiandae na wakati huo huo mtoa hoja atakapokuwa anahitimisha Wabunge waliopo nje wapigiwe kengele ili waweze kuingia ndani. Mheshimiwa Ali Hassan King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante na awali ya yote kwanza shukrani ni kwake Mwenyezi Mungu aliyetupa uhai lakini pia ametupa uzima leo tumekuja hapa.

Mheshimiwa Spika, kingine, nishukuru sana kupata hii nafasi. Tunataka leo tuwawakilishe Watanzania walio wengi katika nchi yetu hii ambao ni vijana. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa sikivu na kuendelea kuwasikiliza wananchi ambao wanawakilishwa na Wabunge wao ambao tupo hapa kuwasilisha mawazo yao na maono yao. Tunaishuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwenye ile hotuba yake ya mwanzo, ukurasa wa 142 alizungumzia kuhusiana na kufanya mgawanyo wa *one third* kutoka katika tozo ya *skills development levy* kwenda katika Wizara unayoshughulikia vijana na ajira. *One third* iende kule, *one third* itakwenda katika mfuko wa mikopo ya elimu ya juu na *one third* itakwenda katika mfuko wa elimu ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, sasa alivyozungumza vile alisema kuwa mabadiliko hayo ya Sheria aliyafanya katika Ibara ya 71 ya hii Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ya Fedha, kwa hiyo alitaka kubadilisha kifungu cha 15 aliweka. Lile wazo la kubadilisha kifungu kile cha 75 ni wazo ambalo lilitokana na Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii. Na kwa nini tuliona vile? Tuliona vile kwa sababu kuna makubaliano ya hii *skilled development levy, one third* iende katika Wizara inayoshughulikia ajira na vijana na kwa sababu tumeliona wimbi la vijana la kukosa ajira.

Mheshimiwa Spika, na yote haya yametokana na kwamba ulifanyika utafiti. Utafiti uligundua kwamba tuna nguvu kazi ambayo ni zaidi ya vijana milioni 23. Lakini katika nguvu kazi hii ni asilimia 3.6 pekee ndiyo nguvu kazi ambayo ina kiwango cha juu cha ujuzi. Na kiwango cha juu cha ujuzi kinatakiwa *at least* kufikia

asilimia 12. Na Wizara ambayo ina ratibu nguvu kazi tunajua kwamba ni Wizara hii ya vijana. Kwa hiyo lile wazo la mwanzo la kuleta Sheria ya kwamba *one third* iende kule lilikuwa ni ombi. Na kwa sababu kule kuna vijana wengi sana wanashindwa ku-*cope* kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, leo hii tukienda katika *SGR* utakuta kwamba wafanyakazi wengi ambao wanakiwango cha ujuzi cha juu au kati ni wa kutoka nje wakati vijana wetu wapo. Kama tuungewafunza na tungewasimamia ingekuwa haina haja ya hizo ajira kuchukuliwa na watu wengine. Lakini isitoshe, tukitazame leo, tumekwenda zetu kule Arusha tuliangalia tukakuta kwamba watu wamefundishwa jinsi ya kulima kupitia halmashauri, wanaita *green house*, lakini ukitizama katika *Green House* zile imefanyika katika Halmashauri chache sana na sisi tuna halmashauri nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, lakini isitoshe sasa hivi utalii umekuwa ni mkubwa sana. Watalii wengi sana na hatuna watu wa kuweza kwenda kuwahudumia. Kwa hiyo ilikuwa ni muhimu hii *one third*. Mheshimiwa Waziri angeliacha kule kule. Maelezo ya leo ya Mheshimiwa Waziri, alisema kwamba kifungu hicho kwamba kinaondolewa, kwamba haya mabadiliko ya kwenda kwenye *one third* yanaondolewa.

Mheshimiwa Spika, mimi pendekezo langu, Waheshimiwa Wabunge, sisi tuna vijana wengi ambao leo tunatamani wawe na ujuzi, ujuzi huo uwasaidie katika kupata ajira. Hawa vijana ndio nguvu kazi yetu sisi. Sisi leo tunakwenda mbele lakini ni kwa sababu ya vijana, matukio yote ni vijana. Sasa hii nguvu kazi ambayo kwamba leo tunakataa kwenda kuisimamia kupata ujuzi kwa ajili ya kujiajiri, tukisema tunaondosha *one third* tunaiacha vile vile ina maana kwanza hizi fedha hazitawafikia.

Mheshimiwa Spika, niseme neno moja, ilikubalika tangu mapema kwamba *one third* iende kule kwa sababu *two third* inakwenda Katika mfuko wa elimu ya juu. Sasa *two third* kule kupeleka *one third* ilikuwa haiendi zinakwenda bilioni tisa tu peke yake, sasa zikienda bilioni tisa vijana wanaokwenda kule kupata yale mafunzo wanakuwa ni vijana wachache, ndiyo maana tulipendekeza iwepo hiyo *one third*. Nimwombe Mheshimiwa

Waziri, mabadiliko ambayo anataka kuyafanya katika kifungu cha 71 cha kwamba bado *two third* ibakie kule katika elimu ya juu arudishe huku kwa sababu kuna vijana tunawatarajia.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo mmoja ambao unasemwa kwamba thamaa amalal mousa ila dhuriyah, hakuna watu waliomwamini Musa isipokuwa vijana. Vijana ndio waliomwamini Musa na vijana ndio waliompa Musa nguvu na sisi tuna vijana. Hawa vijana wakitukimbia sisi tunaelekea wapi? Hawa vijana hii fedha wanapelekewa ikawatengenezee ajira zao wapate ujuzi. Leo zinazalishwa *product* lakini *product* ziko finyu, ni kwa sababu vijana hawana ujuzi, sasa leo tumetenga fedha kwa ajili ya kuwapa vijana ujuzi tukaenda tukaiondosha.

Mheshimiwa Waziri naomba uirejeshe, hii *schedule of amendment* ni sawa utaleta *schedule of amendment* lakini *one third* ibakie pale pale, unasema umekubaliana na Kamati ya Bajeti lakini Kamati hii ya Ustawi wa Jamii tumepita maeneo mengi tumeona hawa vijana na mahitaji hayo yapo kwa sababu vijana wapo. Tuna vijana milioni 23, leo waliokuwa *skilled* ni asilimia tatu tu, tunakwenda katika viwanda hivyo tutaviendeaje kama watu wetu wana ujuzi wa kiwango cha chini? Watu wa kiwango cha chini ujuzi wao ni zaidi ya asilimia 70, leo tunataka kukuza ujuzi kwa vijana, kwamba tunataka kupunguza hiyo fedha.

Mheshimiwa naomba hii fedha uiache kwa vijana, hawa vijana hata mama naye anawategemea, na mimi pia nawategemea hawa vijana na ninyi Majimboni kwenu Waheshimiwa mnawategemea hawa vijana. Mheshimiwa Mwigulu hii *one third*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** … ibakishe iende kwa vijana maana tuna tatizo la ajira kwa vijana. Hawa vijana hawawezi wote kwenda Serikalini. Hapa kila mmoja kapigiwa simu ya ajira na vijana, sasa fedha ziko zinaweza zika-*mobolize* vijana wetu wakapata ajira sasa leo unaziondoshaje? Tunaomba tuachie hii *one third* ije.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja lakini Mheshimiwa hili lifanye kwa ajili ya vijana wetu. Nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba uje uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja; na katika kuhitimisha hoja niseme tu mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, nikianzia na hili ambalo amemalizia Mheshimiwa King, ni kwamba katika majadiliano tulipokaa na Kamati ni moja ya eneo ambalo ndani ya Serikali tulikuwa bado hatujalimaliza. Kwa maana hiyo lilikuwa na mapendekezo ambayo yalikuwa yanahusisha Wizara ya Kazi na kulikuwepo na yanayohusisha Wizara ya Elimu pamoja na eneo lingine lilikuwa linahusisha Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, busara ambayo tuliipata, tulisema tu *maintain status quo* ili tuweze kukubaliana ndani ya Serikali kuhusu ule mgao namna ya Kwenda; kwa sababu ikibaki namna ilivyokuwa bado kwenye utekelezaji fedha zitakwenda vile zile zinazotakiwa kwenda kwa vijana na zile zinazotakiwa kwenda elimu ya juu zitakwenda. Na hili tutakapokuwa tumekubaliana labda Bunge linalokuja lingine linaloshughulikia mambo ya *finance bill* kama muda huu, tuweze kutekeleza tukiwa tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine pia ambalo hatukuwa tumemaliza na Kamati lilikuwa ni lile la masuala ya *software*, kwa hiyo na yenyewe tumeshauriana ndani ya Serikali twende na *position* ya Kamati ili tuweze kuhitimisha jambo lenyewe vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya mengine yote, tumekubaliana na Kamati naomba sasa Bunge lako Tukufu likubaliane kupitisha Muswada huu pamoja na Marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, Katibu.

**NDG: BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi, Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023**
***(The Finance Bill, 2023)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya13
Ibara ya14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hizi namba tutaenda kuzibadilisha zote baadae kwa hiyo kitahojiwa kifungu, tutarejea hiyo namba 13 na 14 lakini ni kile kifungu ambacho kilikuwepo kabla. Kwa hiyo tutazisoma hizo namba na baadae tutarekebisha hizo namba zote kwa pamoja.

Ibara ya13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27
Ibara ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 42

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara Mpya ya 45
Ibara ya 45

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 46

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 47

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 48

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 53
Ibara ya 54

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA:** Kifungu cha 55 kimefutwa.

Ibara ya 55

**MWENYEKITI:** Katibu, hebu simama kwanza.

Mheshimiwa Waziri hiki ni kifungu cha ngapi? Waheshimiwa Wabunge, subirini kidogo. Kitafute tu ukipate tusije tukawa tumekipita hapa. Ni kile Kifungu ambacho alichangia Mheshimiwa Kimei au sio hicho?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kifungu kinachohusisha *software* na *odds* ambazo Mwenyekiti wa Kamati alikichangia. Hivyo, ni hicho pamoja na alichokichangia Mheshimiwa King. Kwa hiyo, hiki ninachokisemea ni kile alichangia cha *odds*.

**MWENYEKITI:** Kama ni hicho basi hakijafikiwa ni Kifungu Na. 68. Hebu kitazame Kifungu Na. 68 hapo kwako. Unayo ile nakala ya Muswada wenyewe hapo?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ninayo.

**MWENYEKITI:** kama unao hebu nenda kwenye Kifungu Na. 68. Umekwishapafikia?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Huko hatujafika bado.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, hatujafika bado lakini nataka niwe na uhakika ni hicho Kifungu unachokizungumzia? Kwa sababu hapa kwenye Kifungu Na.68 mwanzo mlipendekeza kufuta baadaye mmerejesha. Ni hicho ama sio hicho?

*Item* 12 iko ukurasa wa 44 wa huu Muswada na inasema *"Deleting item 20 and substituting for it the following: -*

*(i) Supply of gaming activities including supply of gaming software and odds"*

Umepapata? Ndiyo unazungumzia Kifungu hiki?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes.* Mwanzoni hakikuwepo, tulikuwa tuna *move amendment* ku-*withdraw.*

**MWENYEKITI:** Basi ngoja tukifika hapo tutaweka vizuri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Kwa hiyo, tume- *withdraw amendment.*

**MWENYEKITI:** Sawa, ngoja tufike hapo, halafu tutaweka sawasawa. Katibu.

**NDG ASIA MINJA – KATIBU MEZANI**

Ibara ya 55

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 56

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 57

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 58
Ibara Mpya ya 59
Ibara Mpya ya 60
Ibara ya 59
Ibara ya 60

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 61

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 62
Ibara ya 63

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 64

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 68

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Ibara hii ya 68 ndiyo yenye shida nafikiri. Sasa nikupe nafasi, ulitaka kutoa maelezo ya ziada hapa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hicho Kifungu hatukumaliza na Kamati, lakini tumefanya *consultation*. Tulitaka ku-*move schedule* of *amendment*. Kwa hiyo tuna-*withdraw amendment* ambayo tulitaka kuiweka. Maana yake tuna-*withdraw exemption* tuliyotaka kutoa.

**MWENYEKITI:** Sawa. Unao ule Muswada na unayo marekebisho yenu mliyoyaleta?

Ndiyo.

Sawa, sasa mimi hapa mbele ninao Muswada, ninayo marekebisho mliyokuwa mmeyatoa jana, halafu Kamati ikaleta mapendekezo ambayo Serikali mkawa mmeonesha kwenye hiki Kifungu Na. 68 kwamba, mnaondoa hiki Kifungu Kidogo cha 12, ukurasa wa 44 kwenye Muswada ambacho ndicho kinasema; *"Deleting Item 20 and substituting for it the following: -*

*20. Supply of gaming activities including supply of gaming software and odds."*

Kwa hiyo, mwanzoni Serikali ilikuwa inasema mnaondoa hicho kilichokuwepo huko zamani halafu mnaweka hiki si ndiyo? Mlipokwenda kwenye Kamati mkapeleka marekebisho hayo ambayo mliyapeleka jana kilikuwa kinaonesha kwamba, mnafuta hii 20 na mnaiondoa. Kwa hiyo, mnaondoa hii *Supply of gaming activities including supply of gaming software and odds*. Hiyo ni ya jana.

Marekebisho ambayo yamekuja leo yanaonesha mnataka Kifungu hiki kisiondolewe kibaki hivi hivi kilivyo. Ninazo *set* mbili hapa za marekebisho; marekebisho yenu ya jana na marekebisho mliyoleta leo. Marekebisho mliyoleta leo kama nimeelewa vizuri ni kwamba, mnarudi kwenye Muswada ulivyo.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO**. Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, tuna-*withdraw* hiki tulichotaka kurekebisha.

**MWENYEKITI:** Mna-*withdraw* mlichokubaliana na Kamati?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyokuwa na Kamati tulikubaliana kuondoa ibaki kama ilivyokuwa mwanzo. Leo asubuhi tulitaka kubadilisha *position* ambayo tulikuwa na Kamati. Kwa hiyo, tuna-*withdraw schedule of amendment* ambayo tulikuwa tuna-*introduce* leo ili ibaki kama ambavyo tulikubaliana na Kamati ili ibaki kama ilivyokuwa kwenye Sheria. Tunaondoa marekebisho.

**MWENYEKITI:** Ngoja ili twende sawa. Muswada huu kama unapita namna ulivyo kwenye Kifungu hiki maana yake ni kwamba, Serikali inasema *"Deleting item 20 and substituting for it the following: - "Huu* ndiyo Muswada mlioleta. Kwa hiyo, mmeweka sasa ikishafutwa ile (20) ya zamani, hii mpya itakuwa inasema hivi "*Supply of gaming activities including supply of gaming software and odds*."

Wakati mkikubaliana na Kamati, ile ya jana kwenye hiki Kifungu nadhani Mwenyekiti sijui yupo? Kamati inaonekana mlikuwa na mjadala hapo. Kwa hiyo, kama nakuelewa vizuri, kwa sababu marekebisho mliyoleta leo yanaondoa haya marekebisho

yenu. Kwa hiyo, Muswada unabaki kama ulivyo kwenye kifungu hicho. Mheshimiwa Waziri nimeelewa sawasawa?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunabakiza *position* ambayo tulikuwa sawa na Kamati.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, Mjumbe wa Kamati ya Bajeti.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakumbuka tuliuliza kwamba, kwa nini *software* za *Gaming* na *Odds* ziwe *exempted* wasilipe *VAT* wakati *software* zote zinalipiwa *VAT*? Benki zinalipia *VAT* na kadhalika. Wanasema wasiingize hayo marekebisho.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa Mjumbe wa Kamati nisaidie, maana yake ni kwamba, Kamati ya Bunge mnataka hiki Kifungu kwa namna kilivyoletwa kwenye Muswada kifutwe? Ndiyo wazo la Kamati? Weka kisemeo Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ndicho mlichokubaliana. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama alivyosema Mjumbe wa Kamati, baada ya mashauriano na Serikali tuliwaambia kipengele hicho kifutwe. Ndiyo maana hata *amendment* iliyokuja walifuta, hiyo *clause 68(12)* ilifutwa na sasa iliyokuja leo asubuhi kipengele hiki kimerudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama Kamati tunaomba jambo hili lifutwe kwa sababu halina maslahi mapana kwa Taifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa baada ya kuelewa upande huo, Mheshimiwa Waziri, Kamati inasema mapendekezo yake kwa Serikali ni kwamba Muswada huu ulivyokuwa umeletwa Kifungu hiki kifutwe ili kibaki kile cha zamani. Ninyi leo asubuhi na yale ya jana kuna mabadiliko kidogo. Mabadiliko yenu ya jana ndiyo ambayo Kamati inayakubali. Mabadiliko ya leo ambayo hayaweki kufuta hiki Kifungu Kamati inasema hapana. Sasa nieleze wewe ulikuwa unasema mnataka kukubaliana na Kamati kufuta hiki Kifungu ama?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na Kamati kwenye *position* ile ya kufuta Kifungu ambayo inatuondoa kwenye ile hofu aliyoisema Mjumbe. Kwa hiyo tuna-*withdraw* hiki cha leo tunarudisha kile cha kufuta ambacho tulikubaliana na Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kwa hiyo, haya mabadiliko yaliyoletwa leo, nipe muda kidogo.

Haya, Mheshimiwa Waziri kama niko sahihi kwa sbabu tunavipitisha vifungu na marekebisho ambayo Serikali imeyaleta. Mabadiliko ambayo yalikuwa yamewekwa kwenye hivi vifungu ambayo tunahojiwa sasa, tutumie ile ya jana ama hii ya leo kuna mahali popote ambapo ya leo yanarekebisha yale ya jana ukiacha hiki Kifungu cha 68?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hiki tu ndicho ambacho tulikuwa hatujamaliza na Kamati. Kwa hiyo tuna-*withdraw* tubakize *position* ile ambayo tulikubaliana na Kamati.

**MWENYEKITI:** Sawa. Kwa hiyo, mabadiliko yaliyoletwa leo na upande wa Serikali sio sehemu ya hii hoja. Hoja hii tunahoji na mabadiliko yaliyoletwa jana na Serikali ambayo mlikubaliana na Kamati yetu ya kudumu ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tulikuwa hapa kwenye Kifungu cha 68 na baada ya Mheshimiwa Waziri kuondoa

haya mabadiliko yaliyoletwa leo, tunarejea sasa kwenye yale mabadiliko ambayo Serikali pamoja na Kamati walishakubaliana ya kukiondoa hiki Kifungu ambacho kingekuwa kinatoa unafuu kwa sekta moja halafu sekta nyingine zinaendelea kuwa na hiyo athari. Kwa hiyo, tunapowahoji tunatumia Muswada ambao umefuta hicho kifungu.

Sasa nawahoji Ibara ya 68 pamoja na Marekebisho ya Serikali inaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 69

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 70

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 71

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 72
Ibara ya 73

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpangilio sasa wa namba za ibara unabadilika kutoka iliyokuwa Ibara ya 13 mpaka 73 kuwa 15 mpaka 75.

**MWENYEKITI:** Mabadiliko ya namba ya hivi Vifungu kama alivyosoma Katibu vinaafikiwa?

*(Mabadiliko ya namba za Ibara yalipitishwa pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja, taarifa

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya fedha wa mwaka 2023 *(The Finance Bill, 2023)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na Marekebisho yake. Naomba kutoa hoja kwamba Taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023 *(The Finance Bill, 2023)*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kutunga Sheria Itakayotoza au Kubadilisha Baadhi ya Kodi, Ushuru, Tozo na Ada Mbalimbali. Kufanya Marekebisho kwenye Sheria Mbalimbali Zinazohusu Ukusanyaji na Usimamizi wa Mapato ya Umma *(A Bill for an Act to impose and Alter Certain Taxes, Duties, Levies, Fees and to Amend Certain Written Laws relating to the collection and Management of Public Revenues)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023 (The Finance Bill, 2023 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusoma Muswada mara ya tatu kwa sehemu yetu tumemaliza utaratibu wa utungaji wa sheria. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba Bunge limepitisha Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023 *(The Finance Bill, 2023)* na tunatarajia kuupeleka kwa Mheshimiwa Rais ili na yeye afanye kwa sehemu yake kama Katiba inavyomtaka kwa maana ya kusaini na sasa iwe sheria inayoweza kutumika.

Nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wanaofanya kazi chini yao kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuleta Muswada huu wa Fedha wa Mwaka 2023 ambao Bunge imeuridhia kwa sababu umezingatia maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bajeti. Kwa hiyo, tunawapongeza, lakini pia tunawashukuru kwa kuwa wasikivu na kwa kukubaliana na mawazo ambayo yanatolewa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Kwa muktadha huo huo, tunatarajia kwamba Mheshimiwa Rais ataweka saini yake na tunawatakia utekelezaji mwema kwa yale ambayo mmewaeleza Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, leo tumefanya kazi hizo mbili ya kupitisha Bajeti pia kupitisha Sheria hii ambayo inakwenda kuipa Serikali mamlaka ya kukusanya kodi katika maeneo ambayo

inataka kukusanya na yale ambayo Serikali inaacha kukusanya kodi Sheria imekwishapitishwa na Bunge. Hivyo, baada ya kumaliza utaratibu uliopo basi itaanza kufanya kazi. kwa hiyo na sisi tuwe sehemu ya kuwaelimisha wananchi katika maeneo yetu ya uwakilishi kulingana na yale mabadiliko ambayo sheria hii imeyafanya.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaahirisha shughuli zetu niombe upande wa Serikali hapa kwa Makatibu pia hapa Mezani, tunapokuwa tunatunga Sheria kila sehemu hizi tatu kuwe na nakala ya Sheria hii Mama ambayo ipo, Sheria ambayo inarekebisha na Jedwali la Marekebisho. Inarahisisha kuzisoma zote kwa pamoja ili ujue sheria itasomeka namna gani. Kwa sababu bila hivyo ndiyo tunakwenda mbele, tunarudi nyuma, halafu tutagundua kwamba kuna mahali tulisahau kutoa koma halafu tuanze kumpa kazi AG akaanze kuzitafuta hizo koma na nukta.

Kwa hiyo, ni muhimu hivi vitu vyote vitatu viwepo mara zote tunapotunga Sheria. Sheria iwepo, marekebisho yale yanayofanywa na pale kunapokuwa na jedwali la marekebisho basi na jedwali liwepo katika sehemu hizi tatu. Kama ni Waziri anayehusika ama ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali awe nazo pale na sisi tuwe nazo Mezani. Inarahisisha zoezi la utungaji wa Sheria na kufanya marekebisho ya sheria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), inaendelea na zoezi la ukusanyaji wa maoni yenu juu ya ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo ya Tanzania Bara. Katika kufanikisha zoezi hilo TAMISEMI imeandaa dodoso la ujenzi wa ofisi hizo ili kupata maoni ya Waheshimiwa Wabunge ili kusaidia kufanya maamuzi ya suala hilo. Dodoso hilo limekwishagawiwa kwa kila Mbunge na baada ya kujazwa lirejeshwe kwa wahudumu hapa ukumbini na Waheshimiwa Wabunge wote wa Tanzania Bara ambao bado hamjarejesha fomu hizo mnaombwa kujaza na kurejesha dodoso hilo.

Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu sana, kwa sababu wakati mwingine hata wananchi wanaweza kusema Mbunge haonekani Jimboni kwa sababu hawajui Ofisi yako iko wapi na wakutafute wapi. Kwa hiyo, ni muhimu sana tushiriki kwenye hili zoezi ili tujue Ofisi zetu ziwe wapi. Kama tunataka ziwe Dodoma au kwenye majimbo yetu ni sehemu ya wewe kutoa mawazo yako. Ni muhimu sana kujibu maswali yaliyoulizwa kwenye dodoso kikamilifu ili tuondokane na yale maswali ambayo tunaulizana mara kwa mara kuhusu Ofisi za Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana kwa uvumilivu wenu na sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 8.03 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 27 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*